

MUUNDO NA UAMILIFU WA KIELEZI KATIKA KISHAZI CHA

KISWAHILI

TASNIFU

YA

CHELANGAT WINNY CHERUIYOT

C50/25842/2013

**ILİYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI KWA
MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

JUNI 2017

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na wala haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi _____ Tarehe _____

CHELANGAT WINNY CHERUIYOT

C50/25842/2013

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi: _____ Tarehe: _____

DAKTARI LEONARD CHACHA MWITA

Sahili: _____ Tarehe: _____

DAKTARI ALICE NYAMBURA MWIHAKI

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu: Wilson na Esther Cheruiyot. Mlinihimiza kila wakati nilenge juu. Mungu awatunuku Baraka zisizo na mwisho.

SHUKRANI

Shukrani kwa Mola kwa kunipa nguvu na uwezo wa kuona mwisho wa kazi hii. Daima nitakutukuza.

Shukrani za dhati pia ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Leonard Chacha na Dkt. Alice Mwihaki. Niliona uwajibikaji wa hali ya juu kwenu kama wasimamizi wangu kwa kunihimiza, kunielekeza na kunikosoa. Mungu awazidishie wema na kupanua mipaka yenu kwa hali na mali.

Nawashukuru wahadhiri wengine katika idara ya Kiswahili: Prof. K. King'ei, Prof. Mbaabu, Dkt. R. Wafula, Dkt. J. Gakuo, Dkt. E Masinde, Dkt. J. Onyango, Dkt. T. Arege, Dkt. P.Y. Ngugi, Dkt. M. Osore, Mw. E. Mudhune, na Dkt. P. Mwangi katika idara ya Kiingereza. Mungu awabariki.

Nawashukuru wazazi wangu Bw. Wilson na Bi. Esther Cheruiyot kwa malezi yenu mema. Kila wakati mlinihimiza kuomba na kutegemea Mungu. Vilevile nawashukuru ndugu zangu kunitia moyo katika masomo haya. Shukrani za dhati pia zimwendee mume wangu mpendwa Vincent kwa kujitolea kwake kwa hali na mali. Kukulipa siwezi ila nakuombea tu Rabuka akufikishie heri na shari kukuepushia kabisa. Kwa watoto wangu wapenzi, Stacy na Alaine wacha usomi wa mama yenu uamshe ari na msukumo wa kuyathamini masomo.

Nawashukuru vilevile wasomi wenzangu Wambua, Kirui, Wamalwa, Judy, Lucy, Tabitha, Doris, Adelaide, Brenda, Ngetich, Juma, Kehongo, na Christine, kwa kunitia moyo. Tuendeleo kuhimizana hadi kufikia kiwango cha uzamifu.

Kwa hakika niliupata msaada kutoka watu mbalimbali ingawa sikuweza kuwataja kwa majina lakini sijawasahau, nawashukuruni mno.

ABSTRACT

This research endeavoured to analyse the **structure and functions of the adverb in the Kiswahili clause**. An adverb is a word used to modify a verb, an adjective or another adverb. It is an important part of speech because it conveys information about how things happen as well as when, where and to what extent. The adverb is also taught in both primary and secondary schools in Kenya as one of the categories of Kiswahili words. However, studies on analysis of the Kiswahili adverb have proved to be challenging for four main reasons. Firstly, the Kiswahili adverb is traditionally termed descriptive. It is not clear what the defining features of this category are, since borders with neighbouring categories such as nouns, adjectives and prepositions are vague. Secondly, there seems to be many different structures functioning as adverbs in Kiswahili including morphemes, particles and phrases. These structures need to be explained vividly. Thirdly, the categorization of the adverb in Kiswahili also seems unclear as there are adverbs that cannot be categorized according to the already existing four sub-categories. Lastly, Kiswahili grammar has little to say about the syntax of adverbs for instance, the tendency of the Kiswahili adverb for multiple occurrence in the same clause and the range of possible positions in a Kiswahili clause structure. This research therefore aimed at analyzing the classification of the Kiswahili adverb, investigating the morphological form and syntactical structure of the Kiswahili adverb, and identifying the semantic roles of the adverb in the Kiswahili clausal structure. Independent clauses were used as the main data. Data was collected through the use of questionnaires and also through listening and recording Kiswahili language conversation. The clauses were analyzed within the Minimalist theoretical framework. The morphological study reveals that Kiswahili distinguishes between pure and derived adverbs. Pure adverbs have a simple structure while derived adverbs have a compound structure and are formed through three processes: affixation, reduplication and compounding. This research therefore concludes that, Kiswahili adverbs can be classified according to their morphological structure. Syntactic study reveals that Kiswahili adverbs are mobile, they can occur initially at middle or at the end of a clause. The main syntactic position of an adverb is at the end of a clause but it can occur at the initial position by fronting through focalization and topicalization processes. Kiswahili adverb also has various semantic roles including place, time, process, frequency and degree. This study concludes that the semantic roles influence the morphological and syntactical structure of a Kiswahili adverb.

IKISIRI

Utafiti huu ulinuia kuchanganua **muundo na uamilifu wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili**. Kielezi ni neno linalotumiwa kutoa habari zaidi kuhusu kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Kategoria ya kielezi ni muhimu kwa kuwa hutumiwa katika mawasiliano hasa kueleza mahali, wakati, kiasi na namna kitendo kimetendeka. Kielezi pia ni muhimu kwa kuwa hufunzwa kama mojawapo ya kategoria za maneno ya Kiswahili katika mtaala wa elimu ya shule za msingi na shule za upili nchini Kenya. Hata hivyo, tafiti kuhusu kielezi cha Kiswahili zimedhihirisha kuwepo kwa changamoto za aina nne katika uchanganuzi. Kwanza, kimapokeo kielezi cha Kiswahili kilifasiliwa kuwa kisifa. Dhima ya kuwa kisifa si dhahiri na kutokana na hali hiyo, ni vigumu kutambua kielezi kwa kuwa vina uhusiano wa karibu sana na kategoria kama vile nomino, vivumishi na vihusishi. Pili ni kuwa, kielezi cha Kiswahili ni kategoria pana. Kuna maumbo mengi yanayofanya kazi ya vielezi yakiwemo viambishi, maneno na virai. Maumbo haya yanahitaji kubainishwa. Tatu, uainishaji wa kisemantiki wa kielezi cha Kiswahili una tatizo kwa kuwa kuna vielezi ambavyo haviwezi kuingizwa katika vijikategoria vinne vilivyopendekezwa awali. Mwisho ni kuwa sarufi ya Kiswahili haijatoa ufafanuzi wa kina kuhusu sintaksia ya kielezi hasa kuhusu uwezekano wa vielezi zaidi ya moja kutokea katika kishazi kimoja na kuhusu mazingira ambamo kielezi hutokea katika sentensi. Utafiti huu ulilenga kuchanganua uainishaji wa kielezi cha Kiswahili, kuchunguza umbo la kimofolojia na muundo wa kisintaksia wa kielezi cha Kiswahili, na kudhihirisha dhima za kisemantiki za kielezi cha Kiswahili. Vishazi huru ndivyo vilikuwa data lengwa. Data iliyotumiwa ilikusanywa kwa mbinu ya hojaji, kusikiliza na kurekodi mazungumzo katika lugha ya Kiswahili na kusoma matini teule. Baadaye data hiyo ilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya Sintaksia Finyizi. Uchunguzi wa kimofolojia ulibainisha kuwa Kiswahili kinatofautisha vielezi halisi na vielezi zalishwa. Vielezi halisi huwa na umbo sahili ilhali vielezi zalishwa huwa na umbo changamano na huundwa kupitia mchakato wa uambishaji, urudifu na uambatishaji. Utafiti unafikia hitimisho kuwa kielezi kinaweza kuainishwa kwa kuzingatia umbo la kimofolojia. Uchunguzi wa kisintaksia unadhihirisha kuwa kielezi cha Kiswahili kinaweza kutokea mwanzoni, ndani na mwishoni mwa kishazi. Sehemu msingi ya kielezi cha Kiswahili ni mwisho wa kishazi lakini kinaweza kutokea mwanzoni kupitia uhamisho mada na uhamisho fokasi. Kiswahili pia kinadhihirisha dhima mbalimbali za kisemantiki zikiwemo dhima ya mahali, wakati, utaratibu, kiasi na kiwango. Utafiti huu unahitimisha kuwa dhima za kisemantiki huathiri muundo wa kimofolojia na muundo wa kisintaksia wa kielezi cha Kiswahili.

VIFUPISHO

E	kielezi
ha	hamo
KB	kirai kibainishi
KE	kirai kielezi
KH	kirai kihusishi
KN	kirai nomino
KP	kirai kipatanishi
KSH	kirai kishamirishi
KT	kirai kitenzi
KV	kirai kivumishi
kt	keshatajwa
P	kipatanishi
SF	Sintaksia Finyizi
SZ	Sarufi Zalishi
Taz	tazama
tu	tupu

MAELEZO YA DHANA MUHIMU

- Dhima:** Uamilifu wa kisintaksia au kisémantiki kutokana na uhusiano baina ya kirai nomino au kirai bainishi na kiarifu katika muundo wa kishazi huru.
- Dhima maana:** Uamilifu wa kisémantiki wa kirai nomino au kirai kibainishi kutokana na uhusiano na kiarifu.
- Idadisho:** Hatua ya kuhusisha kila neno na kategoria yake ya kisarufi.
- Kanuni:** Sifa bia zinazotawala mifumo ya sarufi ya lugha zote za binadamu kwa mujibu wa Sarufi Zalishi.
- Kategoria:** Kundi la vijenzi vya kisarufi lenye kushiriki sifa bainifu.
- Kielezi:** Neno linalotoa habari zaidi kuhusu kitenzi, kivumishi na kielezi kingine.
- Kisabiki:** Neno linalotajwa awali ya anafora na linahitaji kurejelewa ili anafora ifasirike.
- Kishazi huru:** Jina lingine la sentensi sahili.
- Mofosintaksia:** Taaluma ya kisarufi inayozingatia uhusiano uliopo baina ya mofolojia na sintaksia.

- Muundo:** Mpangilio wa kategoria za kisarufi katika kuunda virai na vipashio vikubwa zaidi.
- Muungano:** Mfanyiko wa kuunganisha kategoria za kisintaksia ili kuunda vijenzi vikubwa zaidi.
- Sarufi Bia:** Ni mfumo wa kanuni za kisarufi ambazo lugha zote hushiriki.
- Sarufi Finyizi:** Mtazamo wa Sarufi Zalishi unaohitaji mikakati sahili ya nadharia na utafiti wa lugha.
- Sarufi Zalishi:** Mtazamo wa kisarufi ambao unasisitiza ujuzi wa kanuni ubongoni mwa msemaji wa lugha na unaomwezesha kuunda au kuzalisha na kufasiri sentensi.
- Uamilifu:** Kazi ifanywayo na kipashio katika muundo, umbo la neno au miundo ya sentensi.
- Umbo la Kimofolojia:** Idadi ya mofu zinazojumuika pamoja katika neno moja.

YALIYOMO

Mada.....	i
Ikirari.....	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Abstract.....	vi
Ikisiri.....	vii
Vifupisho	viii
Maelezo ya Dhana Muhimu.....	ix
Yaliyomo.....	xi
Orodha ya Vielelezo.....	xv
Orodha ya Majedwali.....	xvii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.0 Usuli wa Utafiti.....	1
1.1 Swala la Utafiti	5
1.2 Maswali ya Utafiti.....	7
1.3 Malengo ya Utafiti	7
1.4 Upeo na Mipaka.....	7
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	8
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	9
1.6.1 Maandishi Jumlifu Kuhusu Kielezi cha Kiswahili	10
1.6.2 Tafiti Bayana Kuhusu Kielezi.....	11
1.7 Misingi ya Nadharia.....	14
1.7.1 Hatua za Uchanganuzi wa Sentensi	16
1.7.1.1 Idadisho.....	16
1.7.1.2 Muungano	17
1.7.1.3 Uhamisho	21
1.7.2 Kanuni Bia katika Sintaksia Finyizi	23
1.8 Mbinu za Utafiti.....	25
1.8.1 Eneo la Utafiti	25

1.8.2	Sampuli na Usampulishaji	26
1.8.3	Mbinu za Ukusanyaji wa Data	27
1.8.3.1	Usomaji	27
1.8.3.2	Hojaji	27
1.8.3.3	Kusikiliza na Kurekodi	28
1.8.4	Uchanganuzi wa Data	28
1.8.5	Uwasilishaji wa Matokeo	29
	SURA YA PILI: KISHAZI CHA KISWAHILI	30
2.0	Utangulizi	30
2.1	Kategoria za Maneno ya Kiswahili	30
2.1.1	Kategoria Leksia	31
2.1.1.1	Kategoria ya Nomino	31
2.1.1.2	Kategoria ya Kitenzi	33
2.1.1.3	Kategoria ya Kielezi	34
2.1.1.4	Kategoria ya Kivumishi	34
2.1.1.5	Kategoria ya Kihusishi	35
2.1.2	Kategoria Sarifu za Maneno	36
2.1.2.1	Kategoria ya Kibainishi	37
2.1.2.2	Kategoria ya Kipatanishi	38
2.1.2.3	Kategoria ya Kishamirishi	39
2.2	Muundo Kirai	40
2.2.1	Kirai Leksia	40
2.2.1.1	Kirai Nomino	41
2.2.1.2	Kirai Kitenzi	42
2.2.1.3	Kirai Kielezi	45
2.2.1.4	Kirai Kivumishi	46
2.2.1.5	Kirai Kihusishi	48
2.2.2	Kirai Sarifu	50
2.2.2.1	Kirai Kibainishi	50
2.2.2.2	Kirai Kipatanishi	52
2.2.2.3	Kirai Kishamirishi	53

2.3	Mahusiano ya Virai katika Kishazi cha Kiswahili	55
2.4	Hitimisho	58
SURA YA TATU: MUUNDO WA KIELEZI KATIKA KISHAZI CHA		
	KISWAHILI	60
3.0	Utangulizi	60
3.1	Maumbo ya Kielezi cha Kiswahili Kutokana na Uundaji	60
3.1.1	Kielezi chenye Umbo Sahili	60
3.1.2	Kielezi chenye Umbo Changamani	61
3.1.2.1	Kielezi Kinachoundwa Kutoka kwa Nomino	62
3.1.2.2	Kielezi Kinachoundwa kutoka kwa Kivumishi	63
3.1.2.3	Vielezi Vinavyoundwa kwa Kurudia Leksimu	64
3.1.2.4	Kielezi Kiigizi.....	65
3.1.2.5	Kielezi Kinachoundwa kwa Uambatishaji wa Vielezi.....	66
3.2	Uchanganuzi Muktadha wa Kielezi katika Kishazi cha Kiswahili.....	69
3.2.1	Kielezi Kinachotokea Mwishoni mwa Kishazi.....	70
3.2.2	Uhamisho wa Kielezi katika Kishazi cha Kiswahili.....	73
3.2.2.1	Vielezi Vinavyotokea Ndani ya Kishazi	75
3.2.2.2	Kielezi Kinachotokea Mwanzoni mwa Kishazi.....	78
3.2.2.3	Uhamisho Usio Mkamilifu wa Kirai Kielezi.....	83
3.2.3	Mpangilio Msonge wa Vielezi katika Kishazi cha Kiswahili.....	87
3.3	Hitimisho	89
SURA YA NNE: UAMILIFU WA KIELEZI KATIKA KISHAZI CHA		
	KISWAHILI	90
4.0	Utangulizi	90
4.1	Dhima ya Mahali.....	90
4.1.1	Pahali Panapodhihirika	91
4.1.2	Pahali Pasipodhihirika	92
4.1.3	Mwelekeo	92
4.1.4	Hatima.....	92
4.1.5	Chanzo	93
4.1.6	Umbali	93

4.2	Dhima ya Utaratibu.....	94
4.2.1	Namna	94
4.2.2	Ala	94
4.3	Dhima ya Wakati.....	95
4.3.1	Vielezi vya Wakati Dhahiri	96
4.3.2	Vielezi vya Wakati Usiodhahiri	96
4.3.3	Vielezi Vinavyorejelea Muda.....	96
4.4	Dhima ya Kiasi	99
4.4.1	Vielezi vya Kuzidisha	99
4.4.2	Vielezi vya Kupunguza	99
4.5	Hitimisho	101
	SURA YA TANO: HITIMISHO.....	102
5.0	Utangulizi	102
5.1	Matokeo ya Utafiti	103
5.2	Mahitimisho	107
5.3	Mapendekezo ya Utafiti Zaidi	109
	MAREJELEO	111
	KIAMBATISHO A: Data ya Utafiti	115
	KIAMBATISHO B: Kibali cha Kufanya Utafiti Kutoka NACOSTI	120

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1.1: Idadisho	16
Kielelezo 1.2: Muungano hadi Kirai Kitenzi	18
Kielelezo 1.3: Muungano hadi Wakilishi Kiima.....	18
Kielelezo 1.4: Muungano hadi Wakilishi Shamirisho	19
Kielelezo 1.5: Muungano hadi Kirai Kielezi	20
Kielelezo 1.6: Hatima ya Muungano	21
Kielelezo 1.7: Uhamisho wa Kirai Nomino.....	22
Kielelezo 2.1: Kirai Nomino cha Umbo la Nomino Moja.....	41
Kielelezo 2.2: Kirai Nomino cha Umbo la Nomino na Kibainishi.....	42
Kielelezo 2.3: Kirai Nomino cha Umbo la Nomino na Kivumishi.....	42
Kielelezo 2.4: Kirai Kitenzi cha Umbo la Kitenzi Pekee	43
Kielelezo 2.5: Kirai Tenzi cha Umbo la Kitenzi na Nomino	43
Kielelezo 2.6: Kirai Tenzi cha Umbo la Kitenzi na Kielezi.....	44
Kielelezo 2.7: Kirai Kitenzi cha Umbo la Kitenzi na Kivumishi	44
Kielelezo 2.8: Kirai Kielezi cha Umbo la Kielezi Pekee.....	45
Kielelezo 2.9: Kirai Kielezi cha Umbo la Vielezi Viwili.....	46
Kielelezo 2.10: Kirai Kivumishi cha Umbo la Kivumishi Kimoja.....	47
Kielelezo 2.11: Kirai Kivumishi cha Umbo la Vivumishi Viwili	47
Kielelezo 2.12: Kirai Kivumishi cha Umbo la Kivumishi na Kielezi	48
Kielelezo 2.13: Kirai Kihusishi cha Umbo la Kihusishi na Nomino.....	49
Kielelezo 2.14: Kirai Kihusishi cha Umbo la Kihusishi na Kielezi	49
Kielelezo 2.15: Kirai Kibainishi cha Umbo la Kibainishi Pekee.....	50
Kielelezo 2.16: Kirai Bainishi cha Umbo la Vibainishi Viwili.....	51
Kielelezo 2.17: Kirai Bainishi cha Umbo la Kibainishi na Nomino.....	51
Kielelezo 2.18: Kirai Kipatanishi cha Umbo la Kipatanishi Tegemezi	52
Kielelezo 2.19: Kirai Kipatanishi cha Umbo la Kirai Kipatanishi Huru	53
Kielelezo 2.20: Muundo wa Kirai Kishamirishi Finyu.....	54
Kielelezo 2.21: Kishazi cha Umbo la Kirai Nomino na Kirai Kipatanishi Finyu	55

Kielelezo 2.22: Kirai Kipatanishi Panuzi chenye Kielezi Kinachofafanua Kitenzi	56
Kielelezo 2.23: Kirai Kipatanishi Panuzi chenye Kielezi Kinachofafanua Kielezi Kingine.....	57
Kielelezo 2.24: Kirai Kipatanishi Panuzi chenye Kielezi Kinachofafanua Kivumishi	58
Kielelezo 3.1: Kielezi cha Wakati Mwishoni mwa Kishazi.....	71
Kielelezo 3.2: Kielezi cha Namna Mwishoni mwa Kishazi	72
Kielelezo 3.3: Kielezi cha Mahali Mwishoni mwa Kishazi	72
Kielelezo 3.4: Kielezi cha Idadi Mwishoni mwa Kishazi.....	73
Kielelezo 3.5: Kielezi Kinachotokea Ndani ya Kishazi.....	76
Kielelezo 3.6: Wakati Kinachotokea Ndani ya Kishazi	77
Kielelezo 3.7: Uhamisho wa Kielezi Kinachodhihirisha Mada.....	79
Kielelezo 3.8: Uhamisho wa Kielezi Kinachowakilisha Fokasi	81
Kielelezo 3.9: Wingi wa Kielezi katika Kishazi kimoja	84
Kielelezo 3.10: Uhamisho wa Kielezi Kimoja Miongoni mwa Vielezi Vingi.....	85
Kielelezo 3.11: Uhamisho wa Kirai Kielezi	86
Kielelezo 4.1: Kishazi chenye Kielezi cha Dhima ya Pahali Panapodhihirika.....	91
Kielelezo 4.2: Kishazi chenye Kielezi cha Dhima ya Ala	95
Kielelezo 4.3: Kishazi chenye Kielezi cha Dhima ya Muda	97

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Ngeli za Nomino za Kiswahili.....	32
Jedwali 2.2: Kategoria Finyu za Kitenzi.....	33
Jedwali 2.3: Kategoria Finyu za Kielezi	34
Jedwali 2.4: Kategoria Finyu za Kivumishi.....	35
Jedwali 2.5: Kategoria Finyu za Kihusishi	36
Jedwali 2.6: Kategoria Finyu za Kibainishi	37
Jedwali 2.7: Kategoria Finyu za Kipatanishi	38
Jedwali 2.8: Kategoria Finyu za Kishamirishi	39
Jedwali 3.1: Kielezi chenye Umbo Sahili katika Kishazi cha Kiswahili	61
Jedwali 3.2: Kielezi Kinachotokana na Uambishaji Awali wa Nomino	62
Jedwali 3.3: Kielezi Kutokana na Uambishaji Tamati wa Nomino	63
Jedwali 3.4: Kielezi Kutokana na Uambishaji Awali wa Kivumishi	64
Jedwali 3.5: Kielezi Kirudufu katika Kishazi cha Kiswahili	65
Jedwali 3.6: Kielezi Kiigizi katika Kishazi cha Kiswahili	66
Jedwali 3.7: Kirai Kielezi Kinachoundwa kwa Uambatishaji	67

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Utafiti

Kielezi ni dhana inayorejelea mojawapo wa kategoria za kileksia. Kwa mujibu wa Haumann (2007), dhana ya kielezi ilitambuliwa mwanzo na mwanasarufi wa Alexandria kwa jina Dionysius Thrax aliyeandika kitabu cha sarufi ya kwanza ya Kiyunani katika enzi ya urasimi wa kale wa Wagiriki. Katika kitabu hicho, Thrax aliunda kielezi kwa kuunganisha maneno mawili ya Kigiriki *#epi#* ‘kuhusu’ na *#rhema#* ‘kitenzi’ na kutoa fasili kuwa kielezi ni sehemu ya usemi isiyoweza kunyambuliwa na inayotumiwa kutoa habari zaidi kuhusu kitenzi.

Katika karne ya 18, wanasarufi ambao walikuwa wameshawishika na mawazo ya Thrax waliendelea kupanua dhana ya kielezi kama inavyoelezwa na Michael (1970). Kielezi kilifafanuliwa zaidi kuwa hutoa habari si tu kuhusu kitenzi bali pia kuhusu vivumishi na vielezi vingine. Kutokana na mtazamo huo, mjadala uliibuka kuhusu iwapo kielezi hufafanua kielezi tu au pia vijenzi vingine katika sentensi.

Dhana ya kielezi ilipanuliwa zaidi kwa kuorodheshwa na kuainishwa katika karne ya 19. Aina tisa za vielezi vilitambuliwa: vielezi vya wakati, vielezi vya mahali, vielezi vya idadi, vielezi vya kiasi, vielezi vya kiwango, vielezi vya kuyakinisha, vielezi vya kukanusha, vielezi visivyo dhahiri, na vielezi vya kulinganisha. Vijikategoria hivi vilionekana kuwa vingi mno na hivyo wanasarufi wa kisasa wamejaribu kuvipunguza kwa kuoanisha vijikategoria vinavyokaribiana.

Uchunguzi wa kielezi ulipiga hatua zaidi katika karne ya 20, wanasarufi walipoendeleza isimu kwa kutumia sayansi jarabati (Kennedy 1920). Utafiti hasa kuhusu sifa bainifu za kielezi ulifanywa na kutokana na tafiti hizo, ilibainika kuwa kielezi kina sifa ya kuweza kuungana na kitenzi na hivyo kudhihirisha uhusiano wa kitenzi na kielezi. Baadhi ya tafiti hizo zilienda hatua moja mbele na kuangazia mabadiliko ya kisintaksia na kisemantiki yanayotokana na uhusiano wa kitenzi na kielezi.

Mwishoni mwa karne ya 20, kielezi kilifanyiwa utafiti zaidi na wanasarufi mbalimbali (Pinkster, 1972; Crystal, 1980; Huddleston, 1984; Cinque, 1999; Hladky, 2003; Ernst, 2004; na Haumann, 2007). Mbali na kueleza fasili ya kielezi, wanasarufi hawa wamechanganua kategoria, umbo, na dhima za vielezi kwa mitazamo ya taaluma ya mofolojia, sintaksia, na semantiki. Taaluma ya mofolojia inahusika na uundaji wa maneno. Baadhi ya wataalamu wamechunguza namna ambavyo kielezi kinaundwa katika lugha mbalimbali.

Uchanganuzi wa kisemantiki huangalia mifumo ya maana pamoja na mahusiano yake. Taaluma ya semantiki imehusika hasa katika uainishaji wa kielezi kwa kuzingatia maana zao. Uainishaji wa kisemantiki unatambua aina mbalimbali za vielezi, aina maarufu zaidi zikiwa vielezi vya wakati, vielezi vya mahali, vielezi vya namna na vielezi vya kiasi. Payne (1997) anaeleza kuwa kielezi kina thamani ya kuwasilisha dhima maana. Ingawa dhima maana kwa kawaida hurejelea uhusiano wa kirai nomino

na kiarifu, inabainika kuwa vielezi pia vina dhima anuwai. Utafiti huu ulichunguza dhima maana za kielezi kwa kuwa dhima maana ni dhana ya kisemantiki inayohusika katika taaluma ya sintaksia.

Uchanganuzi wa kisintaksia hurejelea kanuni za mwambatano wa kielezi na kategoria zingine za kisarufi katika sentensi. Vipengele muhimu vya kielezi ambavyo huchanganuliwa katika sintaksia ni muundo na uamilifu. Baadhi ya wanasarufi wa kisasa wamedhihirisha kuwa dhima za kisintaksia za kielezi ambazo kwa kawaida ni kuwa visifa vya vitenzi, vivumishi na vielezi vingine, huvipa vielezi sifa ya kuweza kutokea katika sehemu tofautitofauti katika kishazi. Isitoshe, vielezi zaidi ya kimoja vinaweza kutokea pamoja katika kishazi na vielezi hivyo huwa na mpangilio maalumu.

Katika uchanganuzi wa kisarufi, taaluma zilizojadiliwa zinaweza kuingiliana na hivyo wakati mwingine ni vigumu kuzitenga. Kwa mfano, ni vigumu kufanya uchanganuzi wa kimofolojia na kisintaksia bila kuhusisha semantiki. Mwingiliano husika unafaa kwa sababu maneno yoyote yanayoundwa yanapaswa kuwa na maana na sentensi pia zinafaa kufasirika. Vilevile taaluma ya mofolojia na sintaksia zina uhusiano wa karibu sana na hivyo tafiti nyingi zimefanywa kwa kufuma vipengele vya kimofolojia na vya kisintaksia katika mtazamo wa kimofosintaksia.

Mtazamo wa kimofosintaksia umejengwa kutokana na mseto wa taaluma mbili: mofolojia na sintaksia. Taaluma ya mofosintaksia kwa hivyo, inaangazia mwingiliano wa vipengele vya mofolojia na sintaksia. Dhana za mofosintaksia zimeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali kuhusiana na urejeshi, mnyambuliko wa vitenzi, uambishaji, uzalishaji wa maneno kutoka kategoria zingine, na upatanisho wa kisarufi (Alexiadou, 1997 na Buell, 2005). Uambishaji na uzalishaji wa maneno ni baadhi ya michakato ya kimofolojia ambayo imeangaziwa zaidi katika uchunguzi wa kielezi.

Baadhi ya vielezi huundwa kwa kuzalishwa kutoka kategoria zingine za maneno, na kwa hivyo huathiri muundo wa kishazi. Kwa kuwa michakato ya kimofolojia huathiri muundo wa kisintaksia (Anderson, 1992), ipo haja ya kufuma taaluma ya mofolojia na sintaksia katika uchanganuzi wa kielezi. Taaluma husika huchunguza namna vielezi zalika huathiri kategoria za kisarufi na mahusiano ya maneno yanayojumuika pamoja katika sentensi. Uchanganuzi wa kimofosintaksia kwa hivyo, utakuwa msingi mwafaka wa utafiti kuhusu muundo na uamilifu wa kielezi.

Kutokana na uchunguzi wa wanasarufi wa kale na wa kisasa, ni dhahiri kuwa kielezi ni kategoria muhimu katika kujenga muktadha lugha kama inavyowakilishwa na sentensi. Licha ya umuhimu ulioashiriwa, tafiti kuhusu kielezi zimedhihirisha kuwepo kwa changamoto katika uchanganuzi. Changamoto hizo zinatokana na mitazamo tofauti kuhusu vipengele vya kisarufi vya kielezi kama vile fasili, uainishaji, na uamilifu wa kielezi katika lugha. Mitazamo tofauti kuhusu dhana ya kielezi inaashiria kuwa kuna pengo katika uchanganuzi wa kielezi na hivyo ipo haja ya kukifanyia

utafiti zaidi.

1.1 Swala la Utafiti

Kielezi kimetambuliwa na waandishi mbalimbali wa Kiswahili kuwa mojawapo wa kategoria muhimu kisarufi na kimawasiliano (Kapinga, 1983; Mbaabu, 1992; Waihiga, 1999; Habwe na Karanja, 2004; Kihore, Massamba na Msanjila, 2003 na Njogu, Mwiwaki na Buliba, 2006). Kielezi kina jukumu la kuongeza habari zaidi ambazo hazingetolewa hasa na kitenzi na hivyo kufanya ujumbe kueleweka zaidi na kuboresha mawasiliano. Wanasarufi waliotajwa wamechanganua dhana ya kielezi kwa kurejelea vipengele kama vile fasili, umbo la kimofolojia, dhima, na uainishaji.

Hata hivyo, maandishi mbalimbali yamedhihirisha matatizo ya aina nne katika uchanganuzi wa kielezi cha Kiswahili. Tatizo kubwa linahusu hasa fasili, hoja kuwa kielezi cha Kiswahili kinatoa habari zaidi kuhusu kitenzi, kivumishi na kielezi kingine inaonekana kuwa pana sana. Dhima hiyo hairejelei vielezi vyote, baadhi ya vielezi vinatoa habari zaidi kuhusu kikundi fulani tu. Kwa mfano, kuna vielezi ambavyo hutoa habari zaidi kuhusu kitenzi tu lakini haviwezi kutoa habari zaidi kuhusu kivumishi. Kutokana na fasili hii pia ni vigumu kutofautisha kati ya vielezi na baadhi ya vivumishi, vihusishi na nomino. Hali hii inatatanisha katika kubainisha dhima za kielezi katika lugha ya Kiswahili.

Mbali na fasili, kuna maumbo mengi yanayofanya kazi ya kielezi yakiwemo mofimu, faridi peke na virai katika lugha ya Kiswahili. Uainishaji wa kielezi cha Kiswahili pia

unadhihirisha mtafaruku mkubwa. Mtafaruku huu unatokana na baadhi ya maandishi yanayodhihirisha uainishaji kwa kigezo cha kimofolojia, mengine yanadhihirisha uainishaji wa kisemantiki na mengine kisintaksia. Ingawa wanasarufi wengi wa Kiswahili wanaunga mkono uainishaji wa kisemantiki, inabainika kuwa uainishaji huo una udhaifu kwa kuwa kuna vielezi ambavyo haviwezi kuingizwa katika kategoria nne zilizopendekezwa.

Sintaksia ya kielezi cha Kiswahili imeshughulikiwa na baadhi ya waandishi kama vile Mohammed, (2001) na Massamba, Kihore na Hokororo, (1999). Kulingana na wataalamu hawa, kielezi hakidumu katika kishazi. Pia vielezi zaidi ya kimoja vinaweza kutokea katika sentensi. Hata hivyo, hakuna maelezo ya kina kuhusu msambao na mpangilio maalumu wa vielezi katika kishazi cha Kiswahili.

Matatizo yaliyoangaziwa yanaashiria kuwa vipengele vya kisarufi vya kielezi cha Kiswahili havijachunguzwa kwa kina. Kuna haja ya kuchunguza namna ambavyo kielezi cha Kiswahili kinaundwa, mazingira ambamo kielezi kinatokea katika kishazi cha Kiswahili pamoja na dhima za kisemantiki za kielezi cha Kiswahili. Kwa kurejelea nadharia ya Sintaksia Finyizi, utafiti wa kimofosintaksia, ulihitajika ili kujibu maswali kuhusu muundo na uamilifu wa kielezi cha Kiswahili kwa uangavu.

1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliazimia kujibu maswali manne:

1. Kielezi cha Kiswahili kina kategoria zipi?
2. Kielezi cha Kiswahili kinadhihirisha maumbo gani kutokana na uundaji?
3. Kielezi cha Kiswahili kina muundo dhima gani wa kisemantiki?
4. Sintaksia Finyizi ina utoshelevu gani katika kuchanganua kielezi cha Kiswahili?

1.3 Malengo ya Utafiti

Kulingana na maswali ya utafiti, malengo manne yananiwa kutimizwa:

1. Kubainisha kategoria za kielezi cha Kiswahili.
2. Kudhihirisha maumbo ya kielezi cha Kiswahili yanayotokana na uundaji.
3. Kubainisha muundo dhima wa kisemantiki unaodhihirishwa na kielezi cha Kiswahili.
4. Kutathmini Utoshelevu wa Sintaksia Finyizi katika kuchanganua kielezi cha Kiswahili.

1.4 Upeo na Mipaka

Kielezi ni dhana inayoweza kushughulikiwa katika taaluma mbalimbali za kiisimu: isimu jamii, isimu linganishi, isimu tafsiri, isimu matini, na isimu jumulifu (sarufi). Kimsingi, utafiti huu ulijumuika katika sarufi. Tangu za kisarufi zinazotambuliwa ni fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki, na pragmatiki. Uchanganuzi katika utafiti huu ulijikita katika sintaksia kwa kuzingatia kuwa kielezi huwakilishwa na kirai

kielezi katika kishazi. Taaluma ya mofolojia ilihusika katika kuchunguza namna ambavyo vielezi vinaundwa na jinsi ambavyo vielezi hivyo vinahusika katika muundo wa kishazi. Utanzu wa semantiki ulihusika katika kuchanganua dhima za kisemantiki za kielezi. Taaluma za fonolojia na pragmatiki hazikuhusishwa kwa sababu kimsingi utafiti huu utajikita katika taaluma ya sintaksia.

Vipengele vya kisarufi vya kielezi hujumuisha fasili, umbo, dhima, na kategoria. Utafiti huu ulichunguza vipengele hivyo vyote. Kielezi kama kijenzi katika kishazi cha Kiswahili, kilichanganuliwa kulingana na fasili na uainishaji. Muundo wa kielezi ulibainishwa kwa kigezo cha kimofolojia. Kisha vipengele vya kisintaksia vya kielezi cha Kiswahili pamoja na vipengele vya kisemantiki viliangaziwa. Katika kiwango cha kisintaksia, utafiti huu ulichunguza, mahusiano ya kielezi na kategoria zingine za kisarufi katika kishazi cha Kiswahili. Katika kiwango cha semantiki, dhima mbalimbali ambazo zinaweza kutimizwa na kielezi katika kishazi cha Kiswahili zilichunguzwa.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu ulichochea na sababu za kinadharia na za kitendakazi. Kinadharia, utafiti huu utachangia sarufi ya Kiswahili hasa katika utanzu wa sintaksia. Mtazamo wa kisintaksia utaongeza maarifa zaidi kuhusu vipengele vya kisarufi vya kielezi kama vile fasili, umbo, kategoria, na dhima. Utafiti huu pia una nafasi ya kutathimini utoshelevu wa nadharia ya Sintaksia Finyizi katika kuchanganua muundo na uamilifu wa kielezi cha Kiswahili.

Utafiti huu pia utakuwa na manufaa ya kutoa maelezo muhimu kuhusu ujifunzaji na ufunzaji wa kielezi cha Kiswahili. Kielezi ni mojawapo ya kategoria za maneno ambazo hufunzwa katika shule za msingi na za upili nchini Kenya. Utafiti huu utachangia katika kuboresha weledi na uwezo wa matumizi ya kielezi cha Kiswahili na hivyo kuimarisha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Aidha, utafiti huu unaweza kusaidia walimu wa lugha ya Kiswahili katika kuelekeza wanafunzi kuhusu utambuzi na matumizi ya kielezi katika kishazi cha Kiswahili.

Kazi hii itajumuika katika hazina ya tafiti zilizofanywa kuhusu sarufi ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuchangia katika utafiti wa baadaye kuhusu kielezi. Wataalamu wataweza kuendeleza taaluma za kiisimu kama vile mofolojia, sintaksia na semantiki ya kielezi. Wasomi wa lugha pia wataweza kufaidika kutokana na utafiti huu katika kufanya tafiti zaidi kwa kulinganisha muundo na uamilifu wa Kielezi cha Kiswahili na vielezi vya lugha zingine katika isimu linganishi.

Kwa jumla, utafiti huu utakuwa na umuhimu wa kinadharia na kitendakazi. Umuhimu husika unaashiria kuwa matokeo ya utafiti yatakuwa na manufaa mbalimbali. Ili kuelewa vyema kielezi kwa jumla, mwanga zaidi kuhusu sababu za kuchagua mada utatolewa katika yaliyoandikwa kuhusu mada.

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Taarifa ya kijumla tayari imeangaziwa kwa mukhtasari katika usuli wa utafiti. Sehemu hii itahakiki maandishi kuhusu dhana ya kielezi kwa undani zaidi. Maandishi haya yaligawanywa katika mawanda mawili: maandishi kuhusu kielezi cha Kiswahili

na tafiti bayana kuhusu kielezi.

1.6.1 Maandishi Jumlifu Kuhusu Kielezi cha Kiswahili

Dhana ya kielezi imeshughulikiwa na waandishi mbalimbali wa Kiswahili (Kapinga, 1983; Mbaabu, 1992; Waihiga, 1999; Habwe na Karanja, 2004; Kihore, Massamba na Msanjila, 2003; Njogu, Mwihaki na Buliba, 2006; Mwihaki, 2007). Sehemu hii itahakiki maandishi ya kielezi cha Kiswahili kwa kuangazia umbo, msambao, na uainishaji.

Maandishi yanayopatikana yanadhihirisha kuwa kielezi cha Kiswahili huundwa kutoka kategoria zingine za maneno. Habwe na Karanja, (2004) wanabainisha namna ambavyo nomino na vivumishi vinaweza kuambishwa ili kuunda vielezi. Kutokana na maelezo yao, inabainika kuwa maumbo mengi hufanya kazi ya kielezi katika kishazi. Maumbo hayo yanajumuisha viambishi awali na tamati, maneno kamili, na virai. Taarifa hii ilichangia utafiti huu katika kuchunguza umbo la kimofolojia la kielezi cha Kiswahili.

Maandishi kuhusu msambao wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili hayapatikani. Hata hivyo baadhi ya waandishi wametaja kwa ufupi kuwa kielezi kina sifa tofauti na kategoria zingine kwa kuwa kina uwezo wa kutokea katika mazingira tofauti tofauti katika kishazi bila kubadilisha maana ya kishazi husika (Mohammed, H. 2013). Maelezo haya yalifaa utafiti huu katika kuweka msingi wa kubainisha sababu za kielezi kuweza kutokea katika sehemu mbalimbali za kishazi.

Kipengele kingine cha kielezi ambacho kimeshughulikiwa na wanasarufi wa Kiswahili ni uainishaji. Vielezi vimeainishwa kisintaksia kutokana na matumizi ya kila kielezi katika sentensi. Kwa mujibu wa Kihore, Massamba, na Msanjila, (2003), tunapata aina mbili kuu za vielezi; vielezi halisi na vielezi viigizi. Vielezi halisi ni vile vielezi ambavyo vina uhusiano wa moja kwa moja na kitenzi, kivumishi, au kielezi kingine. Vielezi viigizi havina uhusiano wa moja kwa moja na tendo lenyewe bali ni mwigo wa tukio la tendo. Baadhi ya waandishi wameainisha kielezi kisemantiki. Habwe na Karanja, (2004) Mgullu, (1999), na Waihiga, (1999), wanataja aina saba za vielezi kulingana na maana zao: vielezi vya wakati, vielezi vya mahali, vielezi vya namna, vielezi vya kiasi, vielezi vya kusisitiza, vielezi vya maswali, na vielezi vya kuidadisha. Uainishwaji huu umeungwa mkono na wanasarufi wengi zaidi wa lugha ya Kiswahili.

Taarifa kuhusu kielezi cha Kiswahili inadhihirisha umuhimu wa dhana mbalimbali za kielezi pamoja na pengo katika uchanganuzi wa umbo, msambao, na uainishaji. Taarifa husika kwa hivyo, ilitoa mwangaza wa kuendelea kutekeleza utafiti huu. Ufafanuzi zaidi utatolewa katika tafiti bayana kuhusu kielezi.

1.6.2 Tafiti Bayana Kuhusu Kielezi

Kielezi kimefanyiwa tafiti na wataalamu katika lugha mbalimbali kama vile Kiingereza, Kiarabu, Kialbania, Kikantonisi na Kimandarin (Cinque, 1999; Yin, 2002; King'ori, 2005; Mohammed, H. 2013; na Pratiwi, 2014). Wataalamu hawa wamechanganua umbo, kategoria, na muundo wa kisintaksia wa kielezi. Baadhi ya tafiti zimelenga lugha moja na zingine zimelinganisha na kulinganua lugha tofauti.

Mofolojia, sintaksia, na semantiki ya kielezi cha Kikantonisi imechunguzwa kwa kulinganisha na kielezi cha Kiingereza (Yin, 2002). Utafiti huo ulinua kuchanganua vipengele anuwai vya kisarufi vya kielezi kama vile fasili, umbo na kategoria za vielezi. Data za utafiti huo zilijumuisha kongoo zilizotokana na mazungumzo halisi ambapo maneno 200,000 yalikusanywa yakiwemo masimulizi ya hadithi na sentensi zilizotolewa kwa vyombo vya habari.

Kielezi katika Kikantonisi kinaweza kutoa habari zaidi kuhusu nomino au kirai nomino, tofauti na kielezi cha Kiingereza ambacho hakitoi habari zaidi kuhusu nomino au kirai nomino. Pamoja na hayo, utambuzi wa kielezi cha Kikantonisi una utata kwa sababu kamusi zinaainisha baadhi ya nomino na vivumishi kama vielezi. Taarifa zaidi inasema kuwa, vielezi vya Kikantonisi haviwezi kutambuliwa kimofolojia kwa kuwa haviambishwi, na kwa hivyo hutambuliwa kwa kuzingatia matumizi ya kisintaksia. Utafiti huo ulichangia utafiti wetu katika kuchanganua, uainishaji, maumbo na dhima za kisemantiki za kielezi, pia katika mbinu za kukusanya data. Tofauti na utafiti huo, utafiti wetu ulishughulikia kielezi cha Kiswahili pekee.

Sintaksia ya kielezi cha Kiarabu na Kiingereza ilichanganuliwa kwa mtazamo wa nadharia ya Mfungo X (Mohammed, H. 2013). Utafiti huo ulidhamiria kulinganisha na kulinganua muundo wa kielezi kisintaksia katika lugha husika. Sentensi sita zilitumiwa katika uchanganuzi, tatu za Kiarabu na tatu za Kiingereza. Uchanganuzi ulidhihirisha kuwa kielezi cha Kiarabu sawia na cha Kiingereza kinadhihirisha

miundo tofauti katika sentensi. Tofauti na kielezi cha Kiarabu, kielezi cha Kiingereza hutokea kabla ya kitenzi ilhali kielezi cha Kiarabu hutokea kabla na baada ya kitenzi. Mahitimisho ya utafiti huo ni kuwa kielezi huweza kuwa na maana zaidi ya moja kutegemea mazingira katika sentensi. Utafiti huo ulichangia utafiti wetu kwa kujenga msingi wa uchanganuzi wa muundo wa kielezi cha Kiswahili katika kishazi. Tofauti na utafiti huo, utafiti wetu ulitumia nadharia ya Sintaksia Finyizi.

Sintaksia ya kielezi pia imechunguzwa na Cinque (1999) kwa mtazamo wa Sintaksia Finyizi. Cinque (keshatajwa) alidhamiria kubainisha msambao wa vielezi katika kishazi, katika lugha mbalimbali. Matokeo ya utafiti huo ni kuwa, kielezi hutokea katika sehemu mbalimbali za kishazi kwa kutegemea uamilifu wao. Mahitimisho ya utafiti huo ni kuwa, baadhi ya vielezi hutokea katika sehemu ya juu ya kishazi na vingine hutokea katika sehemu ya chini na kwa hivyo vielezi kwa jumla huwa na mpangilio wa kimsonge katika kishazi. Utafiti huo unachangia utafiti wetu katika kubainisha msambao wa kielezi cha Kiswahili. Tofauti na utafiti huo, utafiti huu unaangazia lugha moja tu wala si lugha mbalimbali.

Uhamisho wa vijenzi katika sentensi umeshughulikiwa na King'ori, (2005). Utafiti huo ulidhamiria kuchunguza uhamisho wa kichwa na kikanushi katika sentensi za Kiswahili kwa mtazamo wa Sintaksia Finyizi. Lengo la utafiti huo lilikuwa kubainisha sababu za kuhama kwa kichwa na kikanushi pamoja na kudhihirisha mahali ambapo vijenzi hivyo vinahamia. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa, uhamisho huongozwa na kanuni za Sintaksia Finyizi. Aidha utafiti huo unadhihirisha

kuwa kijenzi huhama hatua chache. Utafiti huo unachangia utafiti wetu katika kuchanganua uhamisho wa kielezi. Tofauti na utafiti huo, utafiti wetu utachunguza namna ambavyo kielezi kinaweza kuhama katika kishazi cha Kiswahili.

Umilisi wa kielezi ulichunguzwa kuhusiana na lugha ya Kiingereza (Pratiwi, 2014) Utafiti huo ulinua kutathmini uwezo wa wanafunzi wa gredi ya tano katika kutofautisha kielezi na kivumishi katika lugha ya Kiingereza. Lengo la utafiti lilikuwa kubainisha mbinu za kutambua kielezi ili kuboresha mawasiliano. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wanafunzi wengi wana utata katika kutofautisha kielezi na kivumishi. Hali hii ilitibitishwa na jinsi baadhi ya wanafunzi walivyoshindwa kutambua kielezi katika sentensi walizopewa. Mahitimisho ya utafiti huo ni kuwa ili kutofautisha kategoria hizi ni muhimu kuzingatia muktadha wa neno na dhima zake katika sentensi. Utafiti huo una mchango kwa utafiti wetu katika kubaini mbinu za utambuzi wa kielezi cha Kiswahili. Tofauti na utafiti huo, utafiti wetu ulichanganua vipengele anuwai vya kielezi cha Kiswahili wala si utambuzi pekee.

Tahakiki ya maandishi kwa jumla imefafanua mada mbalimbali kuhusu dhana ya kielezi. Mada zilizoshughulikiwa ni maana, umbo, kategoria, dhima na uhusiano wa kielezi na kategoria zingine za kisarufi katika kishazi. Upungufu unaojitokeza unahusisha fasili, umbo, uainishaji, dhima, na ukosefu wa maelezo kuhusu kanuni zinazotawala sintaksia ya kielezi. Utafiti wetu kwa hivyo una thamani ya kuchunguza muundo na uamilifu wa kielezi cha Kiswahili kwa misingi tofauti ya nadharia.

1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Sintaksia Finyizi ambayo ni mojawapo ya mitazamo ya Sarufi Zalishi (Radford, 1997). Kielelezo msingi cha Sarufi Zalishi (SZ) kiliendelezwa na Chomsky (1965) na kurekebisha mnamo mwongo wa themanini wa karne ya ishirini. Marekebisha ya mwongo wa themanini yanatambuliwa kwa jina la Utawala na Ufungami.

Nadharia ya Utawala na Ufungami ilijumuisha vijinadharia sita: Mfungo X, utawala, uhusika, dhima maana, ufungami, na ufundani. Vijinadharia hivi viliandamana na kanuni bia. Mbali na vijinadharia, Utawala na Ufungami ulitambua miundo miwili ya sentensi: muundo ndani na muundo nje. Mtazamo huo ulionekana kuwa changamano na wenye udhahania mwingi katika uchanganuzi wa sentensi. Kutokana na upungufu huo, Sarufi Zalishi ilisahilishwa kupitia mtazamo wa Sintaksia Finyizi.

Sintaksia Finyizi iliasisiwa kati ya mwaka wa 1993 na mwaka wa 1995 na mtaalamu Chomsky kwa madhumuni ya kurahisisha nadharia ya Utawala na Ufungami (Radford 1997). Nadharia ya Sintaksia Finyizi ilirahisisha uchanganuzi wa kisintaksia kwa mbinu mbili: kubomoa dhana ya muundo ndani wa sentensi na kubomoa vijinadharia kukabaki kanuni bia. Marekebisha ya uchanganuzi wa sentensi yaliambatana na mihimili miwili: hatua za uchanganuzi wa sentensi na mfumo wa kanuni.


1.7.1 Hatua za Uchanganuzi wa Sentensi

Sintaksia Finyizi (SF) inaendeleza imani ya kuwa sentensi sahili (kishazi huru) ni kitengo msingi zaidi cha muundo wa sarufi. Kishazi huru huwa na hadhi sawa na kirai kipatanishi (KP) chenye mchomozo mpana zaidi. Utangulizi wa misingi ya nadharia ulidokeza kuwa SF ilibomoa muundo ndani ikabakia muundo nje pekee, kwa kuzingatia hoja kuwa uundaji na ufasiri wa kishazi hauhitaji muundo ndani bali muundo nje unatosheleza. Muundo ndani ulifidiwa na hatua tatu za uchanganuzi wa kishazi: idadisho, muungano, na uhamisho.

1.7.1.1 Idadisho

Idadisho ni hatua ya kuhusisha kila neno na kategoria yake ya kisarufi. Kategoria ya neno ni kundi la maneno linaloshiriki sifa za kisarufi. Tangu majilio ya Ufungami na Utawala, Sarufi Zalishi inatambua kategoria nane za maneno: nomino (N), kitenzi (T), kivumishi (V), Kihusishi (H), kielezi (E), kibainishi (B), kishamirishi (SH), na kipatanishi (P) (Radford, 1997). Kishazi <Mtaalamu huyo ameandika vitabu vingi vizuri sana> kwa mfano, kinaundwa kwa kategoria sita.

Kielelezo 1.1: Idadisho



Hatua ya idadisho inategemea imani kuwa maneno yamehifadhiwa ubongoni mwa msemaji kulingana na kategoria za kisarufi. Uundaji na ufasiri wa kishazi, kwa hivyo, unategemea uteuzi wa kategoria za maneno. Madai haya yanaashiria kuwa jukumu la


kwanza la kuzingatia katika uchanganuzi wa kishazi ni kuainisha kategoria za maneno. Kategoria za kisarufi huzidi kuhusika katika hatua ya muungano.

1.7.1.2 Muungano

Muungano hurejelea mchakato wa kuunganisha kategoria za kisintaksia ili kuunda virai na vijenzi vikubwa zaidi (Radford, 1997). Kirai cha kawaida huundwa kwa muungano wa fungu la maneno mojawapo likiwa tawala. Neno tawala huwa ni kichwa cha kirai, lingine likiwa shamirisho. Sintaksia Finyizi, na kwa jumla Sarufi Zalishi, inabainisha virai vinane: kirai nomino (KN), kirai kibainishi (KB), kirai kitenzi (KT), kirai kivumishi (KV), kirai kielezi (KE), kirai kihusishi (KH), kirai kipatanishi finyu (P'), na kirai kishamirishi (KSH). Kirai hupewa jina kwa kurejelea kichwa chake.


Kishazi <*mtaalamu huyo ameandika vitabu vingi vizuri sana*> kimeunganisha virai vitano: KN₁, P', KT, KN₂, na KV. Muungano unasonga kijihatua kwa kijihatua hadi kishazi kamili kinapoundwa, ukianza katika kitenzi. Kitenzi kinaungana na vipatanishi katika kuunda kirai kipatanishi finyu (P'). Kirai kipatanishi finyu kinatawala vipatanishi (P) na (KT), inavyodhihirika katika Kielelezo 1.2.

Kielelezo 1.2: Muungano hadi Kirai Kitenzi




Kwa mujibu wa kanuni ya uarifu, kitenzi <andika> kinahitaji kiima. Kiima husika kinawakilishwa na KN <mtaalamu huyo>. Katika kutimiza kanuni ya kuhitaji kiima, kitenzi <andika> kinaungana na KN₁ <mtaalamu huyo> ili kuchomoza muungano zaidi.

Kielelezo 1.3: Muungano hadi Wakilishi Kiima




Pamoja na kuhitaji kiima, kitenzi elekezi <andika> kinahitaji shamirisho. Shamirisho ni jina la kisasa la yambwa msingi na imewakilishwa na KN₂ <vitabu vingi>, na inafuata kiima moja kwa moja. Inalazimu KN₂ kuungana na KN₁ kama inavyodhihirika katika Kielelezo 1.4.

Kielelezo 1.4: Muungano hadi Wakilishi Shamirisho




Shamirisho iliyowakilishwa na KN₂ <vitabu vingi> inaungana na kirai kivumishi (KV) <vizuri> ili kuunda kipatanishi finyu (P') <ameandika mtaalamu huyo vitabu vingi vizuri>. Kielezi <sana> kinahitaji kujumuishwa katika kirai kivumishi ili kukamilisha muungano katika kishazi.

Kielelezo 1.5 Muungano hadi Kirai Kielezi



Muungano hudhibiti mahusiano yenye mpangilio wa kihirakia. Mahusiano hayo yote yanatawaliwa na kirai kipatanishi panuzi (KP) na yanadhihirika kama ilivyo katika kielelezo 1.6. Kielelezo husika kinadhihirisha nafasi tupu (tu) katika pahala pa kawaida pa kiima.

Kielelezo 1.6 Hatima ya Muungano




Nanga ya muungano ni kitenzi, ambacho kwa kawaida hutuzwa hadhi ya kiarifu kutokana na uwezo wa kudhibiti dhima za kiima na shamirisho. Uwezo wa kudhibiti dhima unasababisha muungano kutimia wakati kiima kimo baada ya kiarifu na nafasi ya kawaida ya kiima ikiwa tupu. Nafasi tupu inajazwa kuhusiana na uhamisho.

1.8.1.3 Uhamisho

Uhamisho ni mchakato unaohusu usogezi wa kijenzi cha kisintaksia kutoka pahala pa awali hadi kituo kipya (Radford, 1997). Kijenzi kama vile kirai nomino (KN_1) katika kielelezo 1.7, huondoka mahali pa awali (hame) na kutua kwenye nafasi iliyokuwa tupu. Uhamisho unaanzia chini kuelekea juu ukiacha pitio linaloashiriwa kwa kistari (←-----) hafifu.

Kielezo 1.7 Uhamisho wa Kirai Nomino



Hatua ya uhamisho huongozwa na kanuni tatu: kanuni ya masafa mafupi, kanuni ya ulafi, na kanuni ya ukawilishaji (Radford, 1997). Kanuni ya masafa mafupi inakihitaji kijenzi kisafiri mwendo mfupi iwezekanavyo, ilhali kanuni ya ulafi husisitiza kuwa kijenzi kihame ili kukidhi mahitaji yake ya kiuamilifu katika kishazi. Nayo kanuni ya kukawilisha inaeleza kuwa kijenzi kingoje kuhama hadi ihitajike. Kanuni za uhamisho zinatangamana na kanuni zingine za Sintaksia Finyizi.

1.7.2 Kanuni Bia katika Sintaksia Finyizi

Kama ilivyodokezwa katika utangulizi wa sehemu hii, Sintaksia Finyizi ilibomoa vijinadharia sita vya mtazamo wa Utawala na Ufungami na kubakisha kanuni bia. Dhana ya kanuni inarejelea kikwazo cha kijumla ambacho hutawala muundo wa ufasiri wa kishazi. Kanuni maarufu zaidi ni saba lakini kanuni tano ndizo zilihusika katika utafiti huu: kanuni ya utegemezi muundo, kanuni ya utawala, kanuni ya uhusika, kanuni ya ufasiri kamili, na kanuni ya dhima maana.

Utegemezi muundo ni kanuni maarufu zaidi ya uundaji na ufasiri wa kishazi. Kanuni hii hutawala michakato kamili ya uundaji wa kishazi, inasema kuwa muundo wa kishazi hautegemei maneno yenyewe yaliyotumika katika kishazi bali kategoria za maneno. Utegemezi muundo ni muhimu katika utafiti wa muundo na uamilifu wa kategoria ya kielezi kwa sababu kielezi hutambuliwa kulingana na sifa za kisarufi.

Kanuni ya utawala inaeleza uhusiano baina ya vijenzi viwili sanjari kama vile kichwa cha kirai na shamirisho. Kwa kawaida, kichwa hutawala shamirisho. Uhusiano hudhihirishwa kupitia utawala ambapo kijenzi tawala hutangulia kijenzi tawaliwa katika muundo wa kisintaksia na hapatakiwi kuwa na kizingiti kinachotenganisha. Kanuni ya utawala ilihusika katika kubainisha uhusiano wa kielezi na kategoria zingine katika kishazi kamili.

Uhusika ni kanuni inayoeleza kuwa kiarifu kina uhusiano wa moja kwa moja na kirai nomino au kirai kibainishi kilichojumuika katika kishazi kimoja. Kanuni ya uhusika inatambulisha dhima mbili za kisintaksia ambazo ni kiima na shamirisho

ilivyodokezwa awali (Taz §1.6.1.2). Shamirisho pia huitwa yambwa msingi na inawezesha kielezi kujenga uhusiano na kitenzi.

Kanuni ya ufasiri kamili inasema kuwa kila kijenzi cha kisarufi lazima kifasirike kwa maana bayana ya kileksia au kisarufi. Kwa vile muundo wa kishazi haufai kuwa na vipashio visivyo na maana, kila kijenzi lazima kiwe na maana fulani iwe ya kisemantiki, kisintaksia, au kimofolojia. Pamoja na kuwa na umuhimu wa kisintaksia, kielezi huhusishwa na baadhi ya dhima za kisemantiki.

Kanuni ya dhima maana hueleza uhusiano wa kisemantiki wa kirai nomino (KN) au kirai kibainishi (KB) katika kishazi binafsi. Kwa kurejelea upangaji wa kiarifu, dhima maana mbalimbali zimetambulishwa, na hasa: kiini, kitendi, hisifu, pokezi, chombo, pahala, hatima na chanzo. Kanuni ya dhima maana ilihusika katika kubainisha dhima za kisemantiki za kielezi.

Misingi ya nadharia imeangazia mihimili miwili kuhusiana na Sintaksia Finyizi, ambayo ni hatua za uchanganuzi wa kishazi na kanuni zinazotawala muundo wa kishazi. Hatua za uchanganuzi wa kishazi zilizobainishwa ni idadisho, muungano, na uhamisho. Kila hatua inachangia weledi wa nafasi ya kielezi katika kishazi cha Kiswahili. Nazo kanuni za SF zilizobainishwa ni tano: kanuni ya utegemezi muundo, kanuni ya utawala, kanuni ya uhusika, kanuni ya dhima maana, na kanuni ya ufasiri kamili. Kanuni zote zilizobainishwa zilichangia katika kuongoza mbinu za utafiti.

1.8.0 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti zilizingatia mawanda mawili makuu: utafiti wa maktabani na utafiti wa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulihusisha usomaji wa vitabu, miswada, majarida na tasnifu kwa lengo la kupata taarifa zaidi kuhusu kielezi kwa jumla. Machapisho na makala yanayohusiana na mada ya utafiti huu yalisaidia katika kukuza misingi ya utafiti ili kudhibiti bora zaidi taarifa za kinadharia kuhusu muundo na uamilifu wa kielezi. Kitabu teule ambacho ni riwaya ya Kiswahili pia kilisomwa kwa lengo la kupata data lengwa ambayo ni vishazi huru vyenye vielezi. Baada ya usomaji wa maktabani, utafiti wa nyanjani ulitekelezwa kwa nia ya kuchunguza matatizo ya utambuzi, uainishaji wa kielezi na namna ambavyo kielezi kinatumiwa katika hali halisi kupitia mazungumzo. Utafiti nyanjani kwa hivyo ulisaidia katika kupata data ambayo haingepatikana kutoka usomaji maktabani. Kwa jumla utafiti huu ulihusisha hatua tatu: ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

1.8.1 Eneo la Utafiti

Data ya utafiti huu ambayo ni vishazi huru vyenye vielezi, ilikusanywa kutoka jiji la Mombasa. Eneo hili liliateuliwa kwa misingi kuwa ni mojawapo wa miji mikuu nchini na una watu kutoka janibu mbalimbali ambao wanazungumza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya kwanza ama kama lugha yao ya pili. Kiswahili kinachozungumzwa Mombasa pia hakijaathiriwa sana na lugha zingine. Chomsky na Halle (1968) wanaeleza kuwa wasemaji wa lugha huwa na ufahamu wa kanuni zinazoongoza matumizi ya lugha hiyo.

1.8.2 Sampuli na Usampulishaji

Utafiti huu ulitumia usampulishaji wa kimaksudi. Kombo na Tromp (2006) wanasema kuwa sampuli kusudi huwa mwafaka pale ambapo kundi fulani linaaminiwa kuwa na data inayoafiki malengo ya utafiti. Watafitiwa waliteuliwa kwa kutegemea umilisi wao wa lugha ya Kiswahili. Mtafiti aliteua kimaksudi watafitiwa ambao ni walimu wa Kiswahili kutoka kwa sampuli kubwa ya walimu. Walimu walioteuliwa ni wa kiwango cha shule ya upili. Kigezo cha tajriba ya watafitiwa kutumia na kufundisha Kiswahili kilituongoza. Walimu walioshiriki walitakiwa kuwa wamefunza somo la Kiswahili kwa miaka kumi au zaidi.

Katika kusampulisha walimu, ufundishaji wa kipengele cha mtaala wa shule za upili cha muundo wa sentensi ya Kiswahili kilitumiwa. Kipengele hiki hufundishwa katika kidato cha pili na cha tatu. Isitoshe, kielezi hufundishwa kwa kina katika kidato cha pili na cha tatu. Hivyo basi walimu wa kidato cha pili na cha tatu waliteuliwa. Watafitiwa sita walishiriki katika utafiti huu. Idadi hii ilizua data toshelevu kwa kazi hii. Milroy (1967) anapendekeza matumizi ya sampuli ndogo katika utafiti wa kiisimu kwa sababu sampuli kubwa huzua data yenye urudifu mwingi.

Data iliyohitajika ilikusanywa pia kutoka kwa matini teule ambayo ni riwaya ya *Mkamandume* (Mohammed, S.A. 2013). Kitabu hiki kiliteuliwa kimaksudi kwa msingi kuwa kimesheheni vishazi vingi vilivyo na vielezi. Kitabu hiki pia kina vishazi huru vingi ikilinganishwa na vitabu vingine vya fasihi ambavyo vimetumia hasa sentensi ambatani na changamani. Kitabu kilichoteuliwa kwa hivyo, kilifaa katika

utafiti huu.

1.8.3 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Ubora wa kazi yoyote ya utafiti hutegemea ubora wa data iliyokusanywa ili kuchanganuliwa (Kombo na Tromp, 2006). Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia mbinu tatu bayana: usomaji, hojaji, na kusikiliza na kurekodi.

1.8.3.1 Usomaji

Data ilikusanywa baada ya kusoma kwa makini kitabu kilichoteuliwa ambacho ni *Mkamandume* (2013). Vishazi huru tofautitofauti vilitambuliwa na kuorodheshwa katika majedwali yaliyoundwa kwa kusudi hilo. Mbinu ya usomaji ilidhamiriwa kuwa mwafaka kwa kuwa kitabu kilichoteuliwa kina vishazi huru sanifu vyenye vielezi vya Kiswahili ambavyo vina sifa zilizochunguzwa katika utafiti huu.

1.8.3.2 Hojaji

Mtafiti pia alitumia hojaji kukusanya data aliyohitaji. Hojaji ni orodha ya maswali ambayo huwasilishwa kwa watafitiwa ili wajibu (Mugenda na Mugenda, 1999). Hojaji iliyotumiwa ilikuwa na sehemu mbili: maelezo ya kibinafsi na maswali kuhusu dhana ya kielezi cha Kiswahili. Watafitiwa ambao ni walimu walitakiwa kueleza changamoto za kutambua kielezi cha Kiswahili na kisha kuunda vishazi kwa kutumia vielezi vilivyoorodheshwa katika hojaji. Vishazi hivyo vilitumiwa kuchanganua muundo na uamilifu wa kielezi. Hojaji iliyotumiwa ilitarajiwa kuzua data ya kutegemewa katika utafiti huu kwa kuwa mtafitiwa aliongozwa na maswali yaliyolenga malengo ya utafiti.

1.8.3.3 Kusikiliza na Kurekodi

Mbali na hojaji, mtafiti alitumia mbinu ya kusikiliza na kurekodi kukusanya data. Mbinu hii ilitumiwa katika kukusanya data kwa kurekodi na kuhifadhi mazungumzo katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia kinasa sauti. Mazungumzo yaliyokusudiwa kusikilizwa yalikusanywa kwenye vikao vya wasafiri, mikahawa, barabarani na sokoni jijini Mombasa. Sehemu hizi ziliteuliwa kwa sababu kutokana na jaribio la utafiti, Kiswahili kinatumika pakubwa kama chombo cha mawasiliano. Baadaye mtafiti alichuja na kunakili data muhimu ambayo ni vishazi vyenye vielezi ili viweze kutumiwa katika uchanganuzi. Mbinu ya kusikiliza na kurekodi ilitarajiwa kuzua data ya kutegemewa kwa kuwa mtafiti alijihusisha katika mazungumzo na hivyo kuwezesha kupata data ambayo ilihitajika na ambayo haingepatikana kwa kutumia hojaji na usomaji.

Jumla ya vishazi mia moja na kumi na nne vilitumiwa katika utafiti huu. Idadi hii ya vishazi ni kiwakilishi cha vishazi vyenye sifa zilizochanganuliwa na hivyo ilitarajiwa kufanikisha uchanganuzi wa muundo na uamilifu wa kielezi kwa kurejelea malengo ya utafiti.

1.8.4 Uchanganuzi wa Data

Vishazi vilivyokusanywa vilipangwa na kuainishwa katika makundi mbalimbali kulingana na sifa za kisarufi za kielezi kama vile umbo, kategoria na dhima. Kwa kutumikiza nadharia ya Sintaksia Finyizi, vielezi vyenye maumbo sawa viliwekwa pamoja na kuorodheshwa. Maumbo haya yalichanganuliwa kwa kigezo cha kimofolojia. Kisha vielezi viliainishwa katika kategoria mbalimbali kwa vigezo vya kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Uamilifu wa kielezi katika kishazi pia

ulibainishwa kwa madhumuni ya kutambua na kuweka pamoja vielezi vinavyoweza kutokea katika sehemu fulani katika kishazi. Hatimaye dhima za kisemantiki za kielezi zilidhihirishwa kwa kuzingatia kanuni ya dhima maana. Kwa jumla uchanganuzi wa data ya nyanjani ulilenga kujibu maswali ya utafiti.

1.8.5 Uwasilishaji wa Matokeo

Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo husika yaliimarishwa kwa matumizi ya majedwali na michoro ya kisintaksia. Taarifa ililenga kuangazia mofosintaksia na dhima za kisemantiki za kielezi. Vishazi vilivyokusanywa vilipangwa katika majedwali huku kategoria za vielezi vikibainishwa, michoro ya kisintaksia ilitumiwa kuchanganua muundo wa kielezi katika muktadha wa kishazi. Muundo wa kishazi cha Kiswahili umebainishwa katika sura ya pili.

SURA YA PILI

KISHAZI CHA KISWAHILI

2.0 Utangulizi

Sura ya kwanza ilidhihirisha kuwa muundo wa kishazi unategemea mahusiano ya kategoria za kisarufi, ambazo ni kategoria za maneno au virai (Taz. §1.6.1). Kategoria za maneno huungana kuunda virai na kisha kategoria za virai zikaungana kuunda vishazi. Licha ya kuwa utafiti huu unalenga kielezi katika kishazi cha Kiswahili, kategoria zingine za maneno zitaangaziwa kwa kuwa kielezi kinahitaji kuhusiana na kategoria zingine za maneno ili kutimiza uamilifu wake katika kishazi. Sura hii kwa hivyo, itaangazia maelezo ya kijumla kuhusu vipengele vitatu vya muundo wa kishazi cha Kiswahili: kategoria za maneno ya Kiswahili, muundo kirai katika kishazi cha Kiswahili, na mahusiano ya virai katika kuunda kishazi cha Kiswahili ili kubainisha mambo ya kimsingi kabla ya kufanya uchanganuzi.

2.1. Kategoria za Maneno ya Kiswahili

Kategoria ni dhana inayotumiwa kueleza kundi la maneno lenye sifa za kisarufi zinazofanana (Radford, 1997). Kulingana na kanuni ya tegemezi muundo, uamilifu wa maneno katika virai na vishazi unategemea kategoria zake ila si maneno yenyewe. Mfumo wa maneno ya Kiswahili unabainisha kategoria nane za maneno: nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi, kihusishi, kibainishi, kishamirishi, na kipatanishi. Kategoria hizi nane za maneno hugawika katika vikundi viwili: kategoria leksia na kategoria sarifu.

2.1.1 Kategoria Leksia

Kategoria leksia hurejelea maneno ambayo hubeba maana dhahiri za kimsingi bila kutegemea kipashio kingine. Kategoria leksia hujumuisha aina zote za maneno yenye maana leksia. Kategoria tano za maneno leksia zinazotambuliwa ni: nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi, na kihusishi.

2.1.1.1 Kategoria ya Nomino

Nomino ni neno linalotumiwa kutaja jina la mtu, kitu, mahali, hali, tabia, tukio, mchakato, au utaratibu. Kategoria finyu za nomino huainishwa kwa kuzingatia ngeli za nomino. Uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili umefanywa kwa kuzingatia vigezo viwili ambavyo ni: kigezo cha kimofolojia, na kigezo cha kisintaksia. Uainishaji wa nomino kimofolojia unazingatia taratibu za viambishi vya umoja na wingi wa nomino ambavyo aghalabu hupatikana katika mianza ya nomino husika. Kisintaksia, uainishaji wa ngeli hutawaliwa na kanuni ya ufungami hasa upatanisho wa kisarufi.

Utafiti huu hautaangazia vigezo vyote vya uainishaji wa ngeli. Uainishaji wa kisintaksia wa ngeli za nomino utaangaziwa kwa kuwa unadhihirisha kuwa lugha hufungamanisha maneno yaliyo katika tungo ili kuleta upatanisho wa kisarufi kati yao. Upatanisho huu huweza kuwa kati ya maneno tofauti au katika kishazi (Mdee 1986). Mfungamano huu hujitokeza katika maneno yanayohusiana. Uainishaji wa kisintaksia kwa hivyo ndio utafaa katika utafiti wa muundo na uamilifu wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili. Kulingana na uainishaji wa Vitale (1982), mahusiano ya utaratibu wa kisintaksia katika uainishaji wa ngeli yamedhirishwa katika Jedwali 2.1.

Jedwali 2.1: Ngeli za Nomino za Kiswahili

Mpangilio Kihesabati	wa	Ngeli ya Kisintaksia	Matumizi katika Kishazi
1		A	Mtoto <i>aliumia</i> vibaya.
2		WA	Watoto <i>waliumia</i> vibaya.
3		U	Mlango <i>ulifungwa</i> ndi!
4		I	Milango <i>ilifungwa</i> ndi!
5		LI	Shamba <i>limelimwa</i> vizuri.
6		YA	Mashamba <i>yamelimwa</i> vizuri.
7		KI	Chakula <i>kimeiva</i> kabisa.
8		VI	Vyakula <i>vimeiva</i> kabisa.
9		I	Nyumba <i>itabomolewa</i> kesho.
10		ZI	Nyumba <i>zitablemolewa</i> kesho.
11		U	Ukuta <i>umepakwa</i> rangi vizuri.
14		U	Ufisadi <i>umekita</i> mizizi nchini kabisa.
15		KU	Kusoma <i>kunanufaisha</i> mno.
16		PA	Pahali hapa <i>patasafishwa</i> jioni.
17		KU	Mahali kwote <i>kumejengwa</i> haraka.
18		MU	Mahali mle <i>mnapendeza</i> kwelikweli.

Jedwali hili linadhihirisha kuwa viambishi vinavyotumika kuleta upatanisho wa kisarufi katika muundo wa kishazi ndivyo vinavyotumika kutambulisha ngeli katika mpangilio wa kisintaksia wa ngeli za nomino za Kiswahili. Viambishi vinavyotambulisha ngeli za nomino hujikita katika umbo la kitenzi. Umuhimu wa ufafanuzi wa kategoria ya nomino ni kuwa nomino huwezesha kielezi kujenga uhusiano na kitenzi katika muundo wa kishazi.

2.1.1.2 Katgoria ya Kitenzi

Kitenzi ni katgoria inayorejelea neno ambalo huashiria kitendo na linaweza kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kielezi, kihusishi, au nomino. Kitenzi huweza kukubali viambishi vya mnyambuliko, nafsi, ngeli, yambwa, na njeo. Vitenzi hugawika katika katgoria finyu tatu: vitenzi elekezi, vitenzi sielekezi na vitenzi vishirikishi kama inavyobainishwa katika Jedwali 2.2.

Jedwali 2.2: Katgoria Finyu za Kitenzi

Katgoria finyu	Sifa bainishi	Mifano	Matumizi katika kishazi
kitenzi elekezi	[+KN]	kamata	Askari yule shujaa aliwakamata wezi jana.
kitenzi sielekezi	[-KN]	nyesha	Mvua nyingi ilinyesha juzi asubuhi.
kitenzi kishirikishi	[+N/KV]	ni	Huyu ni mkulima shupavu zaidi.

Kitenzi elekezi ni kitenzi ambacho kinaweza kudhibiti dhima ya yambwa katika muundo wa kishazi huru. Kitenzi sielekezi ni kitenzi kisichoweza kudhibiti dhima ya yambwa katika muundo wa kishazi huru. Kitenzi kishirikishi huwa na dhima ya kushirikisha nomino na nomino nyingine, au kirai kivumishi. Katgoria ya kitenzi ina uhusiano wa moja kwa moja na kielezi.

2.1.1.3 Kategoria ya Kielezi

Kama ilivyodokezwa katika usuli wa utafiti, kielezi ni neno linalotoa habari zaidi kuhusu kitenzi, kivumishi au kielezi kingine (Taz. §1.6.2). Kielezi hujibu swali *Vipi? Lini? Wapi?* au *Mara ngapi?*. Kategoria finyu za kielezi zinazotambuliwa ni saba lakini kategoria maarufu zaidi ni nne: kielezi cha mahali, kielezi cha wakati, kielezi cha namna, na kielezi cha kiwango. Jedwali 2.3 linadhihirisha kategoria finyu za vielezi.

Jedwali 2.3: Kategoria Finyu za Kielezi

Kategoria Finyu	Mifano ya Maneno	Matumizi katika Kishazi
kielezi cha mahali	mbali	Watoto wameenda <i>mbali</i> .
kielezi cha wakati	sasa	Tutaondoka <i>sasa</i> .
kielezi cha namna	polepole	Mwalimu anazungumza <i>polepole</i> .
kielezi cha kiwango	sana	Mwizi ameumia <i>sana</i>

Kutokana na jedwali la kategoria finyu za vielezi, inabainika kuwa uainishaji wa vielezi hufanywa kwa kuzingatia uamilifu wake katika sentensi. Uamilifu uliopo unabainisha uhusiano uliopo baina ya kielezi na maneno mengine kama vile kitenzi, kihusishi, na kivumishi.

2.1.1.4 Kategoria ya Kivumishi

Kivumishi ni kategoria ya maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu nomino. Kivumishi kwa hivyo, kina uhusiano wa moja kwa moja na nomino. Sifa ya nomino

inayodhihirishwa hufungamanishwa na nomino husika. Jedwali 2.4 linadhihirisha kategoria finyu za kivumishi.

Jedwali 2.4: Kategoria Finyu za Kivumishi

Kategoria finyu	Mifano ya maneno	Matumizi katika kishazi
kivumishi sifa	shujaa	Kijana <i>shujaa</i> alimtoa mtoto shimoni.
kivumishi tabia	mzembe	Mwanafunzi <i>mzembe</i> ataadhibiwa.
kivumishi umbo	mrefu	Mti <i>mrefu</i> ulikatwa jana.

Jedwali la kategoria finyu za kivumishi linabainisha kuwa nomino inaweza kuvumishwa kwa kutaja tabia au sifa yake. Ni muhimu kutambua kuwa mtazamo wa Sintaksia Finyizi umepunguza idadi ya kategoria finyu za kivumishi. Maneno yote yaliyokuwa yakitambuliwa kama vivumishi vya sifa katika Sarufi Mapokeo ndiyo pekee huainishwa kama vivumishi katika Sarufi Zalishi. Kategoria ya kihusishi pia inadhihirisha mabadiliko katika uainishaji wa kategoria za maneno.

2.1.1.5 Kategoria ya Kihusishi

Kihusishi ni neno linalofasiri uhusiano wa vitenzi au nomino na vijenzi vingine vya kishazi. Vihusishi hujidhihirisha kwa kategoria finyu mbili: kihusishi sahili na kihusishi kielezi. Jedwali 2.5 linabainisha kategoria finyu za kihusishi.

Jedwali 2.5: Kategoria Finyu za Kihusishi

Kategoria Finyu	Mifano ya maneno	Matumizi katika kishazi
kihusishi sahili	ya	Ndege yuko juu ya mti.
kihusishi elezi	sokoni	Wanabiashara wameelekea <i>sokoni</i> .

Vihusishi sahili vinatokana na maneno sahili kwa kuwa maneno husika yanaundwa kwa silabi moja. Vihusishi elezi vinaundwa kwa maneno ambayo yalijulikana kama vielezi vya mahali na vielezi vya wakati katika Sarufi Mapokeo. Kihusishi kina uhusiano mkubwa na vielezi vya mahali, tofauti ni kuwa kielezi cha mahali kinadhihirisha mahali kitendo kimetendeka ilhali kihusishi kielezi kinatumiwa kuelezea uhusiano wa mahali na kitu kinachorejelewa.

Kategoria zilizojadiliwa katika sehemu hii zinashiriki sifa moja ya kimsingi: kategoria husika zinawakilisha maana dhahiri ya kileksia inayoweza maneno husika kuingizwa katika kamusi kama vidahizo. Sehemu inayofuata itaangazia kategoria sarifu za maneno.

2.1.2. Kategoria Sarifu za Maneno

Kategoria sarifu hurejelea maneno ambayo hayana maana dhahiri ya kisemantiki lakini huwakilisha taarifa za utendakazi wa kisarufi. Kategoria husika kimsingi, hubeba taarifa inayodhihirisha uamilifu wa kisarufi wa aina fulani za vijenzi vya kishazi. Maneno haya hayawezi kuzalisha maneno mengine jinsi ambavyo maneno kama vivumishi vinazalisha nomino au vielezi (Poole, 2002). Kunazo aina tatu za kategoria sarifu: kibainishi, kipatanishi na kishamirishi.

2.1.2.1 Kategoria ya Kibainishi

Kibainishi hurejelea neno linalohusiana na nomino kwa kuashiria sifa ambazo hazijafungamana na nomino ingawa huhusiana na nomino husika kwa namna fulani (Longobardi, 1994). Sifa zenyewe zinaweza kuwa idadi ya kitajwa, uwakilishaji wa kitajwa kwa namna ya kipronomino, umilikishi wa kitajwa, urejeleshi wa kitajwa, au uashiraji wa kitajwa. Kategoria ya kibainishi hudhihirisha kategoria finyu zifuatazo: kiashiria, kimilikishi, kiratibishi, pronomino, kiswalishi, kiidadishi, kijumlishi. Jedwali 2.6 linadhihirisha kategoria finyu za kibainishi.

Jedwali 2.6: Kategoria Finyu za Kibainishi

Kategoria Finyu	Mfano wa Neno	Matumizi katika Kishazi
kiashiria	hiki	Kiti <i>hiki</i> kimevunjika vipande vipande.
kimilikishi	lake	Jino <i>lake</i> limengolewa sasa hivi.
kiratibishi	kwanza	<i>Kwanza</i> ni kuondoka msituni.
pronomino	wewe	<i>Wewe</i> mwimbaji umependeza kabisa.
kiswalishi	yupi	Mwanafunzi <i>yupi</i> ameumia mara kadhaa?
kiidadishi	vingi	Vikombe <i>vingi</i> vitanunuliwa mwaka ujao.
kijumlishi	yoyote	Leta sahani <i>yoyote</i> hapa jikoni.

Maneno yote yaliyokuwa yakiainishwa kama vivumishi viashiria, vivumishi vimilikishi, vivumishi viswalishi, vivumishi viidadishi, vivumishi vya pekee, na pronomino katika Sarufi Mapokeo ndiyo yaliainishwa kama vibainishi katika Sarufi Zalishi. Kibainishi kiliainishwa upya kwa kuzingatia hoja kuwa kibainishi hakina sifa inayofungamana na nomino kama ilivyo kategoria ya kivumishi. Kibainishi na

kivumishi pia hutofautiana kwa kuwa kuna uwezekano wa kufululiza vivumishi viwili au zaidi kuvumisha nomino ilhali vibainishi viwili haviwezi kufululizana (Radford, 2004). Kategoria ya kibainishi hushiriki katika upatanisho wa kisarufi na kategoria ya kipatanishi.

2.1.2.2 Kategoria ya Kipatanishi

Kipatanishi ni kiambishi ambacho aghalabu hufungama awali ya mzizi wa kitenzi ili kuwakilisha vijenzi vya kisarufi kama nafsi au ngeli ya kiima, njeo, hali, na yambwa (Radford, 1997). Vipatanishi ambavyo huwakilisha sifa husika mara nyingi hudhihirika kama viambishi katika umbo la kitenzi. Sifa husika huweza pia kuwakilishwa na kitenzi kisaidizi hivyo basi kukifanya kipatanishi. Kategoria ya kipatanishi huainishwa katika kategoria mbili finyu: kipatanishi tegemezi na kipatanishi huru. Jedwali 2.7 linabainisha kategoria finyu za kipatanishi.

Jedwali 2.7: Kategoria Finyu za Kipatanishi

Kategoria finyu	Mifano katika Kishazi	Matumizi katika Kishazi
tegemezi	<i>ni- li- ki- soma</i>	<i>Nilikisoma</i> kitabu hicho zamani.
huru	<i>ngali</i>	Mpishi <i>angali</i> jikoni.

Kipatanishi tegemezi hudhihirika kupitia kwa viambishi awali ambavyo hutekeleza dhima ya upatanisho katika umbo la kitenzi. Upatanisho wa aina hii hudhihirika katika lugha ambishi-bainishi. Kipatanishi huru hudhihirika kupitia kwa kitenzi kisaidizi kwa kuwa ndicho hutekeleza dhima ya upatanisho wa kisarufi katika muundo wa kishazi. Mbali na dhima ya upatanisho wa kisarufi, kishazi pia

hudhihirisha dhima ya uunganisho ambayo hutekelezwa na kategoria ya kishamirishi.

2.1.2.3 Kategoria ya Kishamirishi

Kishamirishi ni kategoria inayoungana na kishazi kingine ili kukikamilisha kwa kutoa taarifa zenye uhusiano wa vishazi viwili (Radford, 1997). Kishamirishi kinaweza kubainika kama kiambishi au neno kamili. Kiswahili kinatambua aina mbili za vishamirishi: kishamirishi rejeshi na kishamirishi unganifu. Jedwali 2.8 linadhihirisha kategoria finyu za kishamirishi.

Jedwali 2.8: Kategoria Finyu za Kishamirishi

Kategoria Finyu	Mfano wa neno	Matumizi katika kishazi
kishamirishi rejeshi	-amba	Nguo <i>ambayo</i> itashonwa vizuri...
kishamirishi unganifu	ingawa	... <i>ingawa</i> amepita sana.

Kutokana na jedwali hili, inabainika kuwa maneno ambayo yaliitwa viunganishi katika sarufi mapokeo ndiyo yameainishwa upya kama kategoria ya kishamirishi. Kishamirishi unganifu kinatumiwa kutanguliza kishazi ambatani ilhali kishamirishi rejeshi kinatumiwa kutanguliza kishazi tegemezi.

Sehemu hii imejikita katika kubainisha kategoria sarifu za maneno ya Kiswahili. Kategoria tatu sarifu zilizojadiliwa ni kibainishi, kipatanishi na kishamirishi. Kategoria finyu za kila mojawapo wa kategoria pana tatu zilizotambulishwa zimedhihirishwa katika majedwali.

Uchanganuzi wa kategoria za maneno umebainisha kuwa kategoria za maneno ya Kiswahili hugawika katika vikundi viwili: kategoria leksia na kategoria sarifu. Kategoria zote mbili ni muhimu katika uchanganuzi wa kishazi kwa mujibu wa kanuni ya utegemezi muundo. Sehemu inayofuata itaangazia nafasi ya kategoria za maneno ya Kiswahili katika kuunda virai vya Kiswahili.

2.2 Muundo Kirai

Kirai hurejelea fungu la maneno yaliyoungana katika kishazi. Uundaji wa virai huongozwa na mchakato wa muungano unaoleta pamoja maneno mawili au zaidi yanayotenda kazi kwa pamoja katika kishazi (Radford, 1997). Muundo wa kirai huzingatia uhusiano uliopo kati ya neno kuu na maneno mengine. Neno kuu linaitwa kichwa cha kirai na maneno mengine yanatambuliwa kama shamirisho (Taz. §1.7.1.2). Sarufi Mapokeo ilibainisha kirai kuwa maneno mawili au zaidi hata hivyo kulingana na sintaksia ya kisasa hasa Sintaksia Finyizi, neno moja linaweza kuwa kirai iwapo neno hilo ni kichwa cha kirai husika. na iwapo neno hilo limetokea katika mazingira ambamo fungu la maneno laweza pia kutokea. Hivyo basi maumbo yatakayoangaziwa katika sehemu hii yatahusisha kirai cha umbo la neno moja na kirai cha umbo la maneno zaidi ya mawili. Kiswahili kinadhihirisha aina nane za virai (Radford, keshatajwa) Virai hivi vimegawanywa katika vikundi viwili ambavyo ni kikundi cha kileksia na kikundi cha kisarifu.

2.2.1 Kirai Leksia

Kirai leksia hurejelea aina zote za virai ambavyo hutokana na kategoria za maneno ambayo kiasilia yana maana ya kileksia (Radford, keshatajwa). Kirai leksia huwa na


kichwa cha neno la kileksia na vinajumuishwa kategoria tano: kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kivumishi, kirai kihusishi, na kirai kielezi.

2.2.1.1 Kirai Nomino

Kirai nomino ni kirai ambacho muundo wake umetawaliwa na nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu ya maneno. Maumbo ya kirai nomino yanayobainishwa katika Kiswahili ni: nomino moja pekee, nomino na kibainishi, nomino na kivumishi, nomino na kirai kishamirishi, nomino na kirai kivumishi na nomino na kirai kibainishi.

Kirai nomino (KN) cha nomino moja linawakilishwa katika Sheria: $KN \longrightarrow N$. Sheria hii inasema kuwa umbo la kirai nomino linajumuisha umbo la nomino moja pekee. Umbo hili linadhihirika katika kishazi <Askari shujaa aliwakamata wezi wawili jana> ambapo KN kinawakilishwa na nomino #askari#. Umbo husika linadhihirishwa katika Kielelezo 2.1.


Kielelezo 2.1: Kirai Nomino cha Umbo la Nomino Moja



Kirai nomino huweza pia kujumuisha nomino (N) na kibainishi (B) na kuwakilishwa na sheria: $KN \longrightarrow N + B$. Kulingana na sheria hii, umbo la kirai nomino linatawaliwa na nomino na kufuatwa na kibainishi. Katika kishazi <askari yule shujaa aliwakamata wezi wawili jana>, kirai nomino kinawakilishwa kwa kirai <askari yule> kama


inavyodhihirika katika kielelezo kifuatacho:

Kielelezo 2.2: Kirai Nomino cha Umbo la Nomino na Kibainishi



Umbo la nomino (N) na kivumishi (V) linawakilishwa kwa sheria: $KN \rightarrow N + V$. Kulingana na sheria hii, umbo la kirai nomino linatawaliwa na nomino na kufuatwa na kivumishi. Umbo hili linadhihirika katika kishazi *<askari shujaa aliwakamata wezi wawili jana>* ambapo KN kinawakilishwa na kirai *<askari shujaa>* kama inavyodhihirika katika kielelezo 2.3.

Kielelezo 2.3: Kirai Nomino cha Umbo la Nomino na Kivumishi



Sehemu hii imebainisha baadhi ya maumbo ya kirai nomino. Maumbo husika yanadhihirisha kuwa kirai nomino kinaweza kubeba nomino moja, nomino na kibainishi, na nomino na kivumishi. Kirai nomino huweza kujumuishwa katika muundo wa kirai tenzi.


2.2.1.2 Kirai Kitenzi

Kirai tenzi (KT) ni kirai ambacho neno tawala ni kitenzi. Kitenzi huandamana na

kategoria zingine za maneno katika kishazi na hivyo kudhihirisha maumbo mbalimbali. Maumbo husika ni kama vile kitenzi pekee, kitenzi na nomino, kitenzi na kielezi, kitenzi na kivumishi.


Umbo la kitenzi pekee linawakilishwa kwa sheria: $KT \longrightarrow T$. Kulingana na sheria hii, umbo la kirai kitenzi linajumuisha kitenzi kimoja pekee. Katika kishazi *<wakulima wale wamelima>*, kirai kitenzi *<lima>* kinadhihirisha umbo husika. Kirai tenzi cha umbo la kitenzi kimoja kinawakilishwa katika kielelezo 2.4.

Kielelezo 2.4: Kirai Kitenzi cha Umbo la Kitenzi Pekee




Kirai kitenzi kinaweza pia kuwa na umbo la kitenzi na nomino. Sheria: $KT \longrightarrow T + N$ inatumiwa kuwakilisha umbo husika. Kulingana na sheria hii, neno tawala katika kirai kitenzi ni kitenzi likifuatwa na nomino. Kishazi *<wakulima wale wamelima shamba>* kinajumuisha kirai kitenzi *<lima shamba>*. Kielelezo 2.5 kinawakilisha umbo la kirai husika.

Kielelezo 2.5: Kirai Tenzi cha Umbo la Kitenzi na Nomino




Sheria $KT \rightarrow T + E$ inawakilisha umbo la kirai kitenzi ambalo linajumuisha kitenzi na kielezi. Kulingana na sheria hii, neno tawala katika umbo husika ni kitenzi likifuatwa na kielezi. Kishazi *<wakulima wale wamelima vizuri>* kinadhihirisha kirai kitenzi *<lima vizuri>*. Kielelezi 2.6 kinabainisha umbo husika.

Kielelezo 2.6: Kirai Tenzi cha Umbo la Kitenzi na Kielezi



Kirai kitenzi huweza kuwa na umbo la kitenzi na kivumishi. Umbo husika linawakilishwa na sheria: $KT \rightarrow T + V$. Kulingana na sheria hii, kirai kitenzi kimejumuisha kitenzi kama neno tawala na kufuatwa na kivumishi. Kishazi *<wakulima wale ni shupavu>* kinadhihirisha kirai kitenzi. Kielelezo 2.7 kinabainisha umbo husika.

Kielelezo 2.7: Kirai Kitenzi cha Umbo la Kitenzi na Kivumishi



Muundo wa kirai kitenzi umebainishwa katika sehemu hii. Vielelezo vilivyorejelewa vinadhihirisha kuwa kirai kitenzi huweza kuundwa kwa kitenzi pekee, kitenzi na nomino, kitenzi na kielezi, na kitenzi na kivumishi. Kirai kitenzi kina uhusiano wa karibu na kirai kielezi.

2.2.1.3 Kirai Kielezi

Kirai kielezi hurejelea kirai kilicho na muundo neno moja au maneno mawili au zaidi yanayofanya kazi kwa pamoja kama kielezi. Umbo la kirai kielezi hutawaliwa na kielezi likifuatwa na maneno mengine. Maumbo yanayobainishwa katika Kiswahili ni: kielezi kimoja pekee, na vielezi viwili.


Umbo la kirai kielezi pekee linawakilishwa kwa sheria $KE \longrightarrow E$. Sheria hii inasema kuwa umbo la kirai kielezi linajumuisha kielezi kimoja pekee. Kishazi <vitabu vimehifadhiwa vizuri> kinadhihirisha umbo la kielezi pekee. Umbo husika kinawakilishwa katika Kielelezo 2.8.

Kielelezo 2.8: Kirai Kielezi cha Umbo la Kielezi Pekee

$$\begin{array}{c} KE \\ | \\ E \\ | \\ \text{vizuri} \end{array}$$

Kirai kielezi pia kinaweza kujumuisha umbo la vielezi viwili. Umbo husika linawakilishwa kwa sheria $KE \longrightarrow E + E$. Kulingana na sheria hii, kirai kielezi kinaundwa kwa maneno mawili ambayo yote yanahitajika kufanya kazi pamoja kama kielezi. Kishazi <vitabu vimehifadhiwa vizuri sana> kinadhihirisha kirai kielezi <vizuri sana>. Umbo la kirai kielezi cha vielezi viwili linawakilishwa katika kielelezo 2.9.

Kielelezo 2.9: Kirai Kielezi cha Umbo la Vielezi Viwili




Kulingana na maumbo yaliyorejelewa, inabainika kuwa kirai kielezi hakielekei kuwa na mahusiano ya lazima baina ya neno kuu na neno au fungu la maneno linaloandamana nalo kama ilivyo katika virai vingine. Badala yake, kirai kielezi kinaundwa kwa maneno mawili na ambayo yote yanahitajika kuwa vielezi. Aidha kielezi hakiwezi kusimama pekee ili kuleta maana. Kirai kielezi kinaweza kujumuishwa katika muundo wa kirai kivumishi hasa ikiwa kinatoa habari zaidi kuhusu kivumishi.

2.2.1.4 Kirai Kivumishi

Kirai kivumishi ni kirai kilicho na kivumishi kama neno tawala. Kwa kawaida maumbo ya kirai kivumishi hujumuisha kivumishi na neno au fungu la maneno linaloandamana nalo. Maumbo ya kirai kivumishi yanayobainishwa katika Kiswahili ni: kivumishi kimoja, vivumishi viwili, na kivumishi na kielezi.


Umbo la kivumishi kimoja linawakilishwa kwa sheria $KV \rightarrow V$. Kulingana na sheria hii, kirai vumishi kinatawaliwa na kivumishi. Kishazi *<mti mrefu umekatwa>* kinajumuisha kirai vumishi *<mrefu>*. Umbo husika linawakilishwa na Kielelezo 2.10.

Kielelezo 2.10: Kirai Kivumishi cha Umbo la Kivumishi Kimoja




Umbo la vivumishi viwili linawakilishwa kwa sheria $KV \longrightarrow V + V$. Kulingana na sheria hii, kirai kivumishi kinatawaliwa na kivumishi na kufuatwa na kivumishi kingine. Kishazi <mwizi mfupi mnene amekamatwa> kinajumuisha kirai kivumishi <mfupi mnene>. Umbo husika linawakilishwa na Kielelezo 2.11.

Kielelezo 2.11: Kirai Kivumishi cha Umbo la Vivumishi Viwili



Kirai kivumishi kinaweza pia kujumuisha umbo la kivumishi na kielezi. Umbo husika linawakilishwa kwa sheria: $KV \longrightarrow V + E$. Sheria hii inasema kuwa neno tawala katika umbo hili la kirai kivumishi ni kivumishi na kufuatwa na kielezi. Kishazi <mti mrefu zaidi umekatwa > kinadhihirisha umbo la kirai kivumishi <mrefu zaidi>. Kirai kivumishi cha umbo la kivumishi na kielezi kinawakilishwa katika kielelezo kifuatacho.

Kielelezo 2.12: Kirai Kivumishi cha Umbo la Kivumishi na Kielezi




Maumbo mawili ya kirai kivumishi yamebainishwa katika sehemu hii, umbo la kivumishi pekee na umbo la kivumishi na kielezi. Sawa na kirai elezi, inadhihirika kuwa kirai kivumishi kinatawala kategoria chache sana za maneno. Kirai kingine kinachotawala kategoria chache za maneno ni kirai kihusishi.

2.2.1.5 Kirai Kihusishi

Kirai kihusishi ni kirai kilicho na kihusishi kama neno tawala. Maumbo ya kirai kihusishi hujumuisha kihusishi na neno linaloandamana nalo. Maumbo ya kirai kihusishi yanayobainishwa katika Kiswahili ni: kihusishi na nomino, na kihusishi na kielezi.


Kihusishi na nomino ni umbo la kirai kihusishi linalowakilishwa kwa sheria $KH \longrightarrow H + N$. Kulingana na sheria hii, umbo la kirai kihusishi linajumuisha kihusishi kinachofuatwa na nomino. Kishazi <kichwa cha kuku hakistahimili kilemba> kinadhihirisha kirai husishi <cha kuku>. Umbo husika linawakilishwa katika Kielelezo 2.13.

Kielelezo 2.13: Kirai Kihusishi cha Umbo la Kihusishi na Nomino



Umbo la kihusishi na kielezi linawakilishwa kwa sheria $KH \rightarrow H + E$. Sheria hii inasema kuwa umbo la kirai kihusishi linajumuisha kihusishi kinachofuatwa na kielezi. Kishazi <*wakulima wamelima tangu asubuhi*> kinadhihirisha kirai kihusishi <*tangu asubuhi*>. Kielelezo 2.14 kinawakilisha umbo husika.

Kielelezo 2.14: Kirai Kihusishi cha Umbo la Kihusishi na Kielezi



Maumbo mawili ya kirai kihusishi yamebainishwa katika sehemu hii. Maumbo husika yanadhihirisha kuwa kirai kihusishi kinajumuisha kihusishi na nomino kama vile <*cha kuku*> na kihusishi na kielezi kama vile <*tangu asubuhi*>. Maumbo hayo yamewakilishwa katika vielelezo.

Muundo wa kirai leksia umechanganuliwa katika sehemu hii. Kategoria tano ambazo zimebainishwa ni: kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kielezi, kirai kivumishi, na kirai kihusishi. Maumbo mbalimbali ya virai leksia yamebainishwa kwa matumizi ya sheria na vielelezo matawi. Virai leksia hushirikiana na virai sarifu.

2.2.2 Kirai Sarifu


Kirai sarifu kinarejelea kundi la virai ambavyo vina muundo unaotawaliwa na uhusiano baina ya kategoria sarifu za maneno na maneno mengine (Taz . §2.1.2). Virai sarifu kwa hivyo huwa na vichwa vinavyoundwa kwa kategoria sarifu za maneno. Kwa kuzingatia kategoria sarifu za maneno ya Kiswahili, virai sarifu vifuatavyo vinabainishwa: kirai kibainishi, kirai kipatanishi, na kirai kishamirishi.

2.2.2.1 Kirai Kibainishi

Kirai kibainishi ni kirai kilicho na kibainishi kama neno tawala. Kibainishi huungana na kategoria zingine za maneno ili kuunda maumbo mbalimbali ya kirai kibainishi. Baadhi ya maumbo yanayodhihirika katika Kiswahili ni: kibainishi pekee, vibainishi viwili, na kibainishi na nomino.


Umbo la kibainishi pekee linawakilishwa na sheria: $KB \longrightarrow B$. Kulingana na sheria hii, umbo la kirai kibainishi linajumuisha kibainishi kimoja pekee. Kishazi *<hao walionyesha juhudi kubwa sana>* kinadhihirisha kirai kibainishi *<hao>*. Kielelezo 2.15 linawakilisha umbo husika.

Kielelezo 2.15: Kirai Kibainishi cha Umbo la Kibainishi Pekee




Kirai kibainishi kinaweza kuwa na umbo la vibainishi viwili. Umbo husika linawakilishwa na sheria: $KB \longrightarrow B + B$. Sheria hii inasema kuwa kirai kibainishi kinajumuisha kibainishi kinachofuatwa na kibainishi kingine. Kishazi <hao wote walionyesha juhudi kubwa sana> kinadhihirisha kirai bainishi <hao wote>. Kirai bainishi cha umbo la vibainishi viwili kinawakilishwa katika kielelezo 2.16.

Kielelezo 2.16: Kirai Bainishi cha Umbo la Vibainishi Viwili



Umbo la kibainishi na nomino linawakilishwa na sheria: $KB \longrightarrow B + N$. Kulingana na sheria hii, umbo la kirai kibainishi linajumuisha kibainishi kinachofuatwa na nomino. Umbo husika linawakilishwa kwa kirai <huo mkutano> katika kishazi <washirika hao walionyesha juhudi kubwa katika huo mkutano>. Kirai kibainishi cha umbo la kibainishi na nomino kinawakilishwa kwa Kielelezo 2.17.

Kielelezo 2.17: Kirai Bainishi cha Umbo la Kibainishi na Nomino



Sehemu hii imebainisha muundo wa kirai kibainishi kwa kuonyesha maumbo matatu. Kutokana na uchanganuzi wa maumbo husika, inabainika kuwa kibainishi kinaweza kuungana na kategoria mbalimbali za maneno. Baadhi ya maumbo ya kirai kibainishi


hudhihirika ndani ya muundo wa kirai patanishi kama inavyoelezwa katika sehemu ifuatayo.

2.2.2.2 Kirai Kipatanishi

Kirai kipatanishi (KP) hurejelea kirai kinachotawaliwa na kipatanishi. Kirai kipatanishi hudhihirisha mahusiano baina ya kipatanishi na kategoria ya kitenzi katika muundo wa kishazi. Kwa kuzingatia kategoria finyu za kipatanishi, maumbo mawili ambayo ni kirai kipatanishi tegemezi na kirai kipatanishi huru yanabainishwa katika Kiswahili.

Umbo la kirai kipatanishi tegemezi linajumuisha kipatanishi tegemezi kama kichwa cha kirai. Umbo husika linawakilishwa kwa sheria $KP \rightarrow P + T$. Sheria hii inasema kuwa umbo la kirai kipatanishi linajumuisha kipatanishi tegemezi na kitenzi. Kishazi *<wezi walilivizia duka hili jana>* kinadhihirisha kirai kipatanishi tegemezi *<walili->* katika kirai kipatanishi *<walilivizia>*. Kielelezo 2.18 kinawakilisha umbo la kirai kipatanishi tegemezi.


Kielelezo 2.18: Kirai Kipatanishi cha Umbo la Kipatanishi Tegemezi



Umbo la kirai kipatanishi huru linajumuisha kipatanishi huru kama kichwa cha kirai. Umbo husika linawakilishwa kwa sheria $KP \rightarrow P + KP$. Kulingana na sheria hii kirai

kipatanishi kinaundwa kwa kipatanishi huru na kirai kipatanishi kinachobeba kipatanishi tegemezi na kitenzi. Kishazi <wezi wamekuwa wakilivizia duka hili tangu mwaka jana> kinadhihirisha kirai kipatanishi huru <wamekuwa wakilivizia>. Umbo la kirai kipatanishi huru linawakilishwa katika Kielelezo 2.19.

Kielelezo 2.19: Kirai Kipatanishi cha Umbo la Kirai Kipatanishi Huru




Maumbo mawili ya kirai kipatanishi yamebainishwa katika sehemu hii. Maumbo husika ni kirai kipatanishi tegemezi ambacho kimewakilishwa na <wakili> na kirai kipatanishi huru ambacho kimewakilishwa na <wamekuwa>. Kirai kipatanishi kinaweza kujumuisha kirai kishamirishi.

2.2.2.3 Kirai Kishamirishi

Kirai kishamirishi hurejelea kirai ambacho kategoria tawala ni kishamirishi. Muundo wa kirai kishamirishi hudhihirisha mahusiano ya kishamirishi na maneno mengine katika kishazi. Maumbo ya kirai kishamirishi yanayobainishwa katika Kiswahili ni: umbo finyu na umbo panuzi.

Kirai kishamirishi chenye umbo finyu hujumuisha kishamirishi na kirai kipatanishi. Umbo husika linawakilishwa kwa sheria: $KSH \longrightarrow SH + KP$. Kulingana na sheria hii, umbo la kirai kishamirishi linajumuisha kishamirishi kinachofuatwa na kitenzi. Kishazi <nguo zote zilisafishwa na zikaanikwa> kinadhihirisha kirai kishamirishi finyu <na zikaanikwa>. Kielelezo 2.20 kinawakilisha umbo husika.

Kielelezo 2.20: Muundo wa Kirai Kishamirishi Finyu




Kirai sarifu kimeangaziwa katika sehemu hii. Kategoria tatu ambazo zimebainishwa ni: kirai kibainishi, kirai kipatanishi, na kirai kishamirishi kwa kurejelea vielelezo vilivyotumiwa, virai sarifu vimedhihirisha sifa ya kuweza kuungana na kategoria mbalimbali za maneno.

Kwa kijumla, sehemu ya uchanganuzi wa muundo wa kirai imebainisha jinsi kategoria za maneno huhusiana katika muundo wa kirai. Inadhihirika kuwa virai leksia hutangamana na virai sarifu ili kuzalisha tungo ndefu zaidi. Ufafanuzi wa muundo kirai ni muhimu katika kubainisha muundo wa kishazi.

2.3.1 Mahusiano ya Virai katika Kishazi cha Kiswahili

Sura ya kwanza ilibainisha kuwa kishazi huru kina hadhi sawa na sentensi sahihi ambayo inaeleweka kama kirai patanishi katika Sintaksia Finyizi (Taz §1.7.1). Kishazi kamili cha Kiswahili kinashirikisha kijenzi kimoja cha lazima ambacho ni kirai kitenzi (KT) au kirai kipatanishi (KP). Kirai kipatanishi kinaungana na virai vingine ili kuzua maumbo tofauti ya kishazi huru. Kishazi kama vile <walifanya>, kinadhihirisha umbo la kirai kipatanishi finyu. Kishazi husika kinaweza kupanuliwa zaidi kwa kufanyiwa uchomozi. Uchomozi wa kishazi cha umbo la kirai kipatanishi finyu kinaongezewa virai vingine kama kirai nomino, kirai kibainishi, kirai kielezi au kirai kihusishi. Kishazi <vibarua walifanya kazi> kina umbo panuzi kwa sababu kipatanishi <wali> kinafuatwa na kirai kitenzi <fanya kazi> ambacho kinashirikisha kirai nomino <vibarua>. Muundo wa kishazi husika kinawakilishwa katika Kielelezo 2.21.


Kielelezo 2.21: Kishazi cha Umbo la Kirai Nomino na Kirai Kipatanishi Finyu



Katika kudhihirisha muundo na uamilifu wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili, kishazi <vibarua walifanya kazi> kinaweza kupanuliwa zaidi kwa kuongeza virai


vielezi mbalimbali ili kudhihirisha muktadha wa kielezi husika katika kishazi. Kishazi <*vibarua walifanya kazi vizuri*>, kinajumuisha kielezi <*vizuri*> na kinaweza kuwakilishwa ifutavyo.

Kielelezo 2.22: Kirai Kipatanishi Panuzi chenye Kielezi Kinachofafanua Kitenzi




Kielelezo hiki kinadhihirisha kuwa kielezi kimejumuishwa katika kirai tenzi ambacho kimeungana na kirai nomino ili kuunda kishazi kamili. Kielezi kilichohusika kinafafanua namna ambavyo kitendo kilitendeka. Kishazi <*vibarua walifanya kazi vizuri*>. Kinaweza kuchomozwa zaidi kwa kuongeza kielezi kingine kwa mfano <*vibarua walifanya kazi vizuri sana*>. Kishazi husika kinawakilishwa ifuatavyo:

Kielelezo 2.23: Kirai Kipatanishi Panuzi chenye Kielezi Kinachofafanua Kielezi Kingine



Kielelezo hiki kinadhihirisha kuwa kielezi <*sana*> kinafafanua kielezi <*vizuri*> na hivyo kuongeza maana ya taarifa inayotolewa na kishazi msingi <*vibarua walifanya kazi*>. Kishazi hiki kinaweza kuchomozwa pia ili kubainisha namna ambavyo kielezi kinahusiana na kirai vumishi katika uundaji wa kishazi kamili. Kishazi <*vibarua walifanya kazi nzuri sana*>. Kinajumuisha kivumishi <*nzuri*> ambacho kinafafanuliwa zaidi na kielezi <*sana*>. Kishazi chenyewe kinawakilishwa ifuatavyo:

Kielelezo 2.24: Kirai Kipatanishi Panuzi chenye Kielezi Kinachofafanua Kivumishi



Kielelezo hiki kinadhihirisha kuwa kielezi kinaweza kujumuishwa katika kirai vumishi na kuunganishwa virai vingine ili kuunda kishazi kamili. Kielezi <sana> kinatoa habari zaidi kuhusu kivumishi <nzuri> kwa kuleza kiwango cha uzuri wa kitendo kilichotendwa. Kutokana na uchambuzi wa kishazi kamili, inabainika kuwa virai mbalimbali vinaungana ili kuunda kirai patanishi ambacho ni panuzi zaidi.

2.4 Hitimisho

Sura ya pili imechunguza muundo wa kishazi cha Kiswahili kwa kuchanganua kategoria za maneno, na muundo kirai. Aina mbili za kategoria za maneno zilizotambulishwa ni: kategoria leksia na kategoria sarifu. Imebainika pia kuwa kategoria za maneno ndizo huungana ili kuunda virai. Kwa kuzingatia kategoria za maneno, aina mbili za virai zilibainishwa: kirai leksia na kirai sarifu. Maumbo mbalimbali ya virai husika yalidhihirishwa na kuwakilishwa katika vielelezo. Hatimaye mtafiti alibainisha jinsi maumbo husika yanadhihirika katika muundo wa

kishazi cha Kiswahili. Uchanganuzi wa mahusiano ya virai katika kuunda kishazi unadhihirisha kuwa kirai kielezi kinahusiana na virai vingine na kwa hivyo ni mojawapo wa vijenzi muhimu katika uundaji wa kishazi. Taarifa iliyoangaziwa katika sura hii itafaa katika kuchanganua muundo wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili.

SURA YA TATU

MUUNDO WA KIELEZI KATIKA KISHAZI CHA KISWAHILI

3.0 Utangulizi

Dhana ya muundo ilifafanuliwa awali katika sura ya kwanza kama mpangilio wa kategoria za kisarufi katika kuunda virai, na vipashio vikubwa zaidi (Taz §1.0). Sehemu hii inanuia kuchunguza maumbo ya kielezi kutokana na uundaji. Muundo wa kisintakisia pia utaangaziwa kwa lengo la kubainisha mazingira ambamo kielezi kinapatikana katika kishazi cha Kiswahili, kudhihirisha namna ambavyo kielezi kinahama katika kishazi cha Kiswahili, pamoja na kuchunguza namna ambavyo vielezi vinapangika kimsonge katika kishazi cha Kiswahili.

3.1 Maumbo ya Kielezi cha Kiswahili Kutokana na Uundaji

Data ya utafiti huu, inadhihirisha maumbo mawili ya kielezi kutokana na namna ambavyo vinaundwa. Maumbo husika ni umbo sahili na umbo changamani. Vielezi vyenye umbo sahili kulingana na utafiti huu, ni vile ambavyo vinaundwa kwa mofimu huru. Vielezi vyenye umbo changamani ni vile ambavyo vinaundwa kwa uambishaji au uambatishaji wa kategoria zingine za maneno.

3.1.1 Kielezi chenye Umbo Sahili

Katika utafiti huu, kielezi chenye umbo sahili hakichukui viambishi vyovyote na kwa hivyo huwa leksimu. Vielezi vyenye umbo sahili huwa havihusiani na kategoria zingine za maneno na kwa hivyo ni halisi. Kazi yao ni kuwa vielezi katika kishazi. Mifano ya vielezi vyenye umbo sahili ni kama: *ajabu, kabisa, mbali, mno, ovyo, sana,*

tu, na *zaidi*. Matumizi ya vielezi hivi katika kishazi yanadhihirishwa katika Jedwali 3.1.

Jedwali 3.1: Kielezi chenye Umbo Sahili katika Kishazi cha Kiswahili

Kielezi	Matumizi katika Kishazi
ajabu	Liyongo alikuwa mtu mnene <i>ajabu</i> .
kabisa	Mkulima alinunua gari jeupe jipya <i>kabisa</i> .
mno	Gharama ya maisha mjini Mombasa ni ghali <i>mno</i> .
ovyo	Juma amezoea kutumia gari <i>ovyo</i> .
sana	Hawa wote walionyesha juhudi kubwa <i>sana</i> katika huo mkutano.
tu	Wanatumia <i>tu</i> zile pesa.
zaidi	Huyu ni mkulima shupavu <i>zaidi</i> .
mbali	Watoto wameenda <i>mbali</i>

Jedwali hili linadhihirisha kuwa vielezi vinaweza kuundwa kwa mofimu huru. Vielezi vilivyorejelewa kama vile *sana*, *zaidi*, *ovyo*, na *mbali* havina viambishi na hivyo basi vimechukuliwa katika utafiti huu kuwa vielezi sahili. Vielezi husika ni vichache mno.

3.1.2 Kielezi chenye Umbo Changamani

Kielezi cha Kiswahili kinaweza kuwa na umbo changamani. Umbo changamani linatokana na uambishaji au uambatishaji wa kategoria zingine za maneno. Viambishi awali au tamati huchopekwa kwa nomino au kivumishi ili kuunda vielezi. Vielezi pia huweza kuundwa kwa kuambatisha maneno kwa kuongeza faridi peke kwa nomino. Aidha, leksimu huweza kurudiwa ili kuunda vielezi. Baadhi ya vielezi kama vile vya kionomatopea, huweza kuundwa kutokana na uigaji wa sauti. Inabainika pia kuwa kirai elezi kinaweza kufanya kazi ya vielezi katika kishazi. Inadhihirika kuwa vielezi

vyenye umbo changamano huzalishwa kutoka kategoria zingine.

3.1.2.1 Kielezi Kinachoundwa Kutoka kwa Nomino

Vielezi huundwa kwa kuambatanisha viambishi /ki/, /ni/, au /u/ kwenye nomino. Kiambishi /ki/ kinachopekwa kwa nomino kama vile: *fisi, kondoo, nyama, jeshi*, na *mwanaume* ili kuunda vielezi: *kifisi, kikondoo, kinyama, kijeshi*, na *kiume* mtawalia. Jedwali 3.2 linadhihirisha nomino zinazochukua kiambishi /ki/ ili kuunda vielezi.

Jedwali 3.2: Kielezi Kinachotokana na Uambishaji Awali wa Nomino

Kielezi	Uambishaji awali		Matumizi katika Kishazi
	Kiambishi	Nomimo	
<i>kifisi</i>	ki	Fisi	Wanasisia wanapora mali <i>kifisi</i> .
<i>kikondoo</i>	ki	Kondoo	Alikufa <i>kikondoo</i> .
<i>kinyama</i>	ki	Nyama	Askari walimchapa mfungwa <i>kinyama</i> .
<i>kijeshi</i>	ki	Jeshi	Wanafunzi hawa wanatembea <i>kijeshi</i> .
<i>kiume</i>	ki	mwanaume	Maimuna anafanya kazi <i>kiume</i> .

Jedwali 3.2 linadhihirisha kuwa nomino inaweza kuchopekwa kiambishi /ki/ ambacho kinafananisha kitendo na kinachorejelewa ili kuunda vielezi vya namna mfanano. Kiambishi husika kina maana ya *kama* na huchopekwa mwanzoni mwa nomino ili kuonyesha kufanana kwa hali mbili tofauti. Kiambishi awali /u/ huweza pia kuchopekwa kwa nomino ili kuunda vielezi. Nomino *pande* huongezwa kiambishi /u/ ili kuunda kielezi *upande*. Kielezi husika kinadhihirisha mahali ambapo kitendo kimetendeka. Hata hivyo vielezi vinavyoundwa kwa kuchopeka kiambishi /u/ kwenye nomino ni vichache mno.

Nomino za kawaida kama vile *soko*, *korokoro*, na *nyumba*, huweza kubadilika kuwa vielezi kwa kuchopeka kiambishi tamati /ni/ cha mahali mwishoni mwa nomino hizo ili kuunda maneno *sokoni*, *korokoroni*, na *nyumbani*. Jedwali 3.3 linadhihirisha matumizi ya vielezi husika katika kishazi.

Jedwali 3.3: Kielezi Kutokana na Uambishaji Tamati wa Nomino

Kielezi	Uambishaji Tamati		Matumizi katika Kishazi
	Nomino	Kiambishi	
sokoni	soko	ni	Wanabiashara wameondoka <i>sokoni</i> .
nyumbani	nyumba	ni	Mtoto ameachwa <i>nyumbani</i> .
korokoroni	Korokoro	ni	Mfungwa alitoroka <i>korokoroni</i> .

Nomino *soko*, *nyumba*, na *korokoro* zinarejelea jina la kitu lakini kiambishi /ni/ kinapochopekwa kwenye nomino husika, nomino hizo hubadilika kuwa vielezi *sokoni*, *nyumbani* na *korokoroni* ambavyo vinanerejelea mahali dhahiri ambapo kitendo kilitendeka.

3.1.2.2 Kielezi Kinachoundwa kutoka kwa Kivumishi

Vielezi changamano pia huweza kuzalishwa kutoka kwa vivumishi. Kiambishi awali /ki/ au /vi/ huchopekwa kwenye kivumishi ili kuleta maana ya vielezi. Vivumishi kama vile *-baya*, *-dogo*, na *-zuri* vinaweza kuongezwa kiambishi /ki/ au /vi/ ili kuunda vielezi *-vibaya*, *-kidogo*, na *-vizuri* mtawalia. Jedwali 3.4 linadhihirisha uundaji na matumizi ya vielezi husika katika kishazi.

Jedwali 3.4: Kielezi Kutokana na Uambishaji Awali wa Kivumishi

Kielezi	Uambishaji awali		Matumizi katika Kishazi
	Kiambishi	Kivumishi	
vibaya	vi	-baya	Mtoto ameanguka <i>vibaya</i> .
kidogo	ki	-dogo	Musa ameumia <i>kidogo</i> .
vingine	vi	-ngine	Tulijaribu <i>vingine</i> .
vizuri	vi	-zuri	Shamba letu limelimwa <i>vizuri</i> .

Velezi vilivyorejelewa *vibaya* na *vizuri* katika vishazi <*mtoto ameanguka vibaya*>, na <*shamba letu limelimwa vizuri*> vinaeleza namna ambavyo kitendo kilitendeka. Kielezi *vingine* katika kishazi <*tulijaribu vingine*> kinaonyesha njia mbadala ya kutenda kitendo kilichorejelewa na kielezi <*kidogo*> katika kishazi <*Musa ameumia kidogo*> kinaeleza kiasi cha kutendeka kwa kitendo.

3.1.2.3 Vielezi Vinavyoundwa kwa Kurudia Leksimu

Vielezi vya Kiswahili vinaweza kuundwa kwa kurudia leksimu mara mbili kwa mfano maneno *haraka* na *ovyo* yanaweza kurudiwa ili kuunda kielezi changamano kama vile *harakaharaka* na *ovyoovyo*. Kielezi zalika kama *kimchezo*, kinaweza pia kurudiwa ili kuunda kielezi *kimchezomchezo*. Jedwali 3.5 linadhihirisha matumizi ya kielezi husika katika kishazi

Jedwali 3.5: Kielezi Kirudufu katika Kishazi cha Kiswahili

Kielezi	Urudufu	Matumizi katika Kishazi
harakaharaka	haraka + haraka	<i>Harakaharaka</i> vipanga vikatumbukia shimoni.
hivihivi	hivi + hivi	Wanafunzi wengi hufanya kazi <i>hivihivi</i> .
hobelahobela	hobela + hobela	Oliech alibebwa <i>hobelahobela</i> .
kimchezo	kimchezo+ mchezo	Hamadi alifanya kazi <i>kimchezomchezo</i>
kisirisiri	kisiri + siri	<i>Kisirisiri</i> babu akauza shamba.
kwelikweli	kweli + kweli	Mahali humu mnapendeza <i>kwelikweli</i>
nyumanyuma	nyuma + nyuma	Mkamandume alirudi <i>nyumanyuma</i> kwa uoga.
ovyooovyoo	ovyoo + ovyoo	Wanasiasa huzungumza <i>ovyooovyoo</i>

Jedwali 3.5 linadhihirisha kuwa vielezi virudufu hasa hueleza namna kitendo kimetendeka. Kwa mfano kielezi <harakaharaka> katika kishazi <harakaharaka vipanga vilitumbukia shimoni> kinaeleza jinsi au namna ambavyo vipanga viliingizwa kwenye shimo.

3.1.2.4 Kielezi Kiigizi

Viigizi huweza kufanya kazi ya vielezi katika kishazi. Viigizi hutokana na kulinganishwa kwa sauti inayotolewa na nomino au kitenzi kinachotajwa. Aina hii ya maneno hujulikana kama tanakali za sauti au vifanano vya sauti kwa kuwa hutokana na kuiga sauti. Viigizi *bwe! Ndi! Zu!* na *Tuli!* Vinaweza kutumika kama vielezi. Jedwali 3.6 linadhihirisha matumizi ya vielezi husika katika kishazi.

Jedwali 3.6: Kielezi Kiigizi katika Kishazi cha Kiswahili

Kiigizi	Matumizi katika Kishazi
bwe!	Mbwa alibweka <i>bwe!</i>
ndi!	Mlango ulifungwa <i>ndi!</i>
zu!	Moshi ulizuka <i>zu!</i>
tuli!	Wachezaji walitulia <i>tuli!</i>

Viigizi vinaweza pia kurejelewa kama vielezi vya kionomatopia. Kisintaksia viigizi vina uamilifu sawa na vielezi kwa kuwa vinatokea baada ya kitenzi na vinaweza kufanya kazi ya kielezi kwa kutoa habari zaidi kuhusu namna ambavyo kitendo kimetendeka. Viigizi hutumika pia kama viunganishi elezi au viashiria matini katika mawasiliano. Hivyo basi kuna muumano wa uamilifu wa viigizi na vielezi katika kishazi.

3.1.2.5 Kielezi Kinachoundwa kwa Uambatishaji wa Vielezi

Kirai kielezi huweza kutumika kama vielezi. Kirai elezi ni kikundi cha maneno ambacho kichwa chake ni kielezi kwa mfano. *<ameondoka sasa hivi>*, *sasa hivi* ni maneno mawili ambayo yanafanya kazi ya kielezi. Mifano mengine ni kama vile *mapema jana jioni, mara tatu leo asubuhi, vibaya sana na mbali kabisa*. Jedwali 3.7 linadhihirisha uambatishaji wa vielezi na matumizi ya vielezi hivyo katika kishazi.

Jedwali 3.7: Kirai Kielezi Kinachoundwa kwa Uambatishaji

Uambatishaji	Matumizi katika Kishazi
mapema + jana + asubuhi	Walisoma gazeti <i>mapema jana asubuhi</i> .
vibaya + sana	Mtoto ameumia <i>vibaya sana</i>
mbali + kabisa	Ndege ameruka <i>mbali kabisa</i> .

Jedwali 3.7 linadhihirisha kuwa vielezi viwili au zaidi vinaweza kuambatishwa pamoja ili kufanya kazi ya vielezi. Kielezi cha pili aghalabu husisitiza ujumbe uliotolewa na kielezi cha kwanza. Kirai kielezi *vibaya sana* katika kishazi <*Mtoto ameumia vibaya sana*> kinaeleza kiasi cha jinsi ambavyo mtoto alianguka. Vilevile vielezi vinaweza kuwa na majukumu mbalimbali vinapotumika pamoja katika kishazi.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa katika sehemu hii, inadhihirika kuwa kielezi kina maumbo mawili kwa kutegemea namna ambavyo kinaundwa. Kielezi huweza kuwa na umbo sahili au huweza kuwa na umbo changamani. Utafiti huu unabainisha kuwa vielezi vyenye umbo sahili ni vichache mno na vinajumuisha vielezi kama vile: *sana*, *kabisa ovyo*, na *tu*, miongoni mwa vingine. Vielezi husika vimeundwa kwa mofimu huru na kazi yao hasa ni kuwa vielezi katika kishazi. Kielezi cha Kiswahili pia kinaundwa kutoka kategoria zingine kama vile kategoria ya nomino na kivumishi. Vielezi husika huwa na umbo changamani. Nomino huchopekwa kiambishi /ki/, /ni/ na /u/ ili kuunda vielezi vya namna na vya mahali. Vielezi pia huundwa kwa kuchopeka kiambishi /ki/ au /vi/ kwenye kivumishi ili kuunda vielezi vya namna. Utafiti huu vilevile unabainisha kuwa kielezi huweza kuundwa kwa kurudia kielezi

hasa cha namna kama vile *ovyoyo* ili kuunda kielezi *ovyooovyoyo*. Kielezi husika kinaleta msisitizo wa ujumbe katika kishazi. Aidha viigizi hupata uamilifu wa kielezi vinapotumika kufafanua kitenzi katika kishazi.

Katika uambishaji na uambatishaji wa maneno ili kuunda kielezi, hatua za idadisho na muungano zinahusika. Si kategoria zote ambazo zinaweza kuambishwa ili kuunda vielezi. Hivyo basi, kupitia mchakato wa idadisho, baadhi ya kategoria zinateuliwa ili ziweze kushiriki katika uundaji wa kielezi. Kwa mujibu wa utafiti huu, kategoria zinazoteuliwa ili kuambishwa ni nomino na kivumishi. Aidha si kategoria zote ambazo zinaweza kuambatishwa ili kuunda kirai kielezi. Kupitia mchakato wa muungano, kihusishi kanaungana na nomino ili kuunda kirai ambacho kinafanya kazi ya kielezi katika kishazi. Vilevile, vielezi viwili au zaidi vinaungana ili kuunda kirai kielezi. Inadhihirika pia kuwa vielezi vinavyoangana ili kuunda umbo la kirai kielezi hasa ni vile vinavyorejelea wakati.

Tafiti za awali kuhusu kielezi cha Kiswahili zimechunguza mofolojia ya kielezi kwa kuangazia namna ambavyo kielezi kinaweza kuundwa kutoka kategoria zingine za maneno (Habwe na Karanja, 2004, Mgullu, 1999). Utafiti huu unaendeleza mitazamo ya wataalamu hao kwa kudhihirisha kuwa kielezi kina maumbo mawili ya kimofolojia: umbo sahili na umbo changamani. Utafiti wa Yin (2002) kuhusu mofolojia ya kielezi katika Kikantonisi ulibainisha kuwa kielezi cha kikantonisi hakiwezi kutambuliwa au kuainishwa kimofolojia kwa kuwa vielezi katika lugha husika haviambishwi. Data ya utafiti huu inabainisha kuwa kategoria zingine za maneno katika lugha ya Kiswahili zinaweza kuambishwa ili kuunda vielezi na kwa

hivyo, kielezi kinaweza kutambuliwa na kuainishwa kimofolojia.

Uzalishaji wa vielezi, unadhihirisha kuwa kielezi kina uhusiano mkubwa na kategoria zingine za maneno. Uhusiano huo unawiana na mhimili wa kanuni ya uhusika katika Sintaksia Finyizi ambao unaeleza kuwa kiarifu kina uhusiano na kielezi na pia maneno mengine yanayojumuika pamoja katika kishazi. Kielezi kinaarifu zaidi kuhusu kitendo katika kishazi (Taz §1.7.2). Kanuni za uundaji wa maneno hukubaliana na kanuni za kisintaksia. Hii ni kwa sababu maneno yanayoundwa lazima yaathiri muundo wa kisintaksia. Hivyo basi vielezi vinavyoundwa huathiri muundo wa kishazi kama inavyoangaziwa katika sehemu inayofuata.

3.2 Uchanganuzi Muktadha wa Kielezi katika Kishazi cha Kiswahili

Katika kuchanganua muktadha wa kielezi, muundo wa kisintaksia wa kielezi utaangaziwa. Muktadha katika utafiti huu, unarejelea mazingira ambamo kielezi kinaweza kupatikana katika kishazi. Usuli wa utafiti ulidokeza kuwa sintaksia hushughulikia uchanganuzi, mpangilio, na uhusiano wa vipashio katika kishazi (Taz. § 1.0). Sehemu hii itaangazia msambao wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili kwa kuchunguza iwapo kielezi kinaweza kusonga hadi mbele kushoto mwa kishazi kupitia mchakato wa uhamisho fokasi na uhamisho mada. Mpangilio wa vielezi zaidi ya moja pia utaangaziwa ili kubainisha iwapo vielezi vya Kiswahili vinapangika kimsonge kama vile Cinque (1999) anavyoeleza.

Kielezi cha Kiswahili kinadhihirika kuwa na upekee kikilinganishwa na kategoria zingine. Hii ni kwa sababu kina uwezo zaidi wa kutokea katika sehemu tofautitofauti

za kishazi. Jackendoff (1972) anatoa ufafanuzi wa muktadha wa kielezi kwa jumla na ana msimamo kuwa vielezi hugawika katika vikundi viwili kisintaksia: vielezi vya kishazi na vielezi vya vitenzi. Vielezi vya vishazi vinatokea mwanzoni mwa kishazi na hudhibitiwa na kirai kipatanishi navyo vielezi vya vitenzi hutokea baada ya kitenzi au mwishoni mwa kishazi na hudhibitiwa na kirai kitenzi. Aidha, Jackendoff (keshatajwa) anasema kuwa kunavyo vielezi ambavyo haviingii kwenye vikundi viwili vilivyotajwa. Vielezi husika hutokea kati ya kiima na kitenzi halisi na hudhibitiwa na kitenzi au kirai kipatanishi. Potsdam (1998) anamuunga mkono Jackendoff (1972) kuhusu ugawaji wa vielezi katika vikundi viwili lakini anatofautiana naye kuhusu kinachodhibiti vielezi kwa kujadili kuwa, vikundi viwili vilivyotajwa vinadhhibitiwa na vichwa vinavyobeba vielezi hivyo na lazima vitokee karibu na vichwa hivyo. Kichwa katika muktadha huu, kinarejelea lile neno ambalo linafafanuliwa na kielezi. Kwa kawaida, kielezi kinatokea karibu na neno ambalo kinafafanua. Utafiti huu unakubaliana na maelezo Potsdam (1998) kuwa vielezi vya Kiswahili vinadhhibitiwa na vichwa vinavyobeba vielezi hivyo na hivyo kusababisha kielezi kutokea katika sehemu tofautitofauti za kishazi kama inavyojadiliwa katika sehemu ifuatayo.


3.2.1 Kielezi Kinachotokea Mwishoni mwa Kishazi

Vielezi vinavyotokea mwishoni mwa kishazi ni vile ambavyo vinafuata kitenzi katika kishazi. Hii ni sehemu msingi zaidi ya vielezi vya Kiswahili kwa kuwa aina zote za vielezi zina uwezo wa kutokea mwishoni kutegemea uamilifu wa kielezi husika katika kishazi. Mifano ifuatayo inabainisha vishazi vilivyo na vielezi vinavyotokea mwishoni mwa kishazi.

- 1 a) Wanafunzi walichelewa *juzi*.
- b) Askari walinyatia *polepole*.
- c) Mnazi umepandwa *nje*.
- d) Mwalimu ametusaidia *mara kadhaa*.


Kishazi <*wanafunzi walichelewa juzi*> kinajumuisha kielezi cha wakati <*juzi*>. Kielezi husika kinatokea mwishoni mwa kishazi baada ya kitenzi <*walichelewa*> na kinaeleza wakati kitendo kilitendeka. Kielelezo 3.1 kinawakilisha kishazi husika.

Kielelezo 3.1: Kielezi cha Wakati Mwishoni mwa Kishazi




Kielezi cha namna <*polepole*> kimetokea mwishoni katika kishazi <*askari walinyatia polepole*>. Kielezi husika kinafafanua kitenzi <*walinyatia*>. Kielelezo 3.2 kinawakilisha kishazi husika.

Kielelezo 3.2: Kielezi cha Namna Mwishoni mwa Kishazi




Kwa kawaida, vielezi vya mahali hutoka mwishoni mwa kishazi. Hii ni kwa sababu data ya utafiti inadhihirisha kuwa baadhi yavyo lazima viwepo katika kishazi ili kishazi kiwe kamilifu kimaana. Kielezi <nje> katika kishazi <mnazi umepandwa nje> kinatanguliwa na kitenzi <umepandwa> na kinaeleza mahali kitendo kinatendeka. Kishazi husika kinawakilishwa katika Kielelezo 3.3.

Kielelezo 3.3: Kielezi cha Mahali Mwishoni mwa Kishazi



Vielezi vya idadi pia hutokea mwishoni mwa kishazi. Kielezi <maru kadhaa> katika kishazi <mwaimu ametusaidia maru kadhaa> kinatokea baada ya kitenzi <ametusaidia> Kielezi husika kinatupa habari kuhusu kiasi cha kutendeka kwa kitendo, Kishazi hiki kinawakilishwa ifuatavyo:

Kielelezo 3.4: Kielezi cha Idadi Mwishoni mwa Kishazi



Sehemu hii inadhihirisha kuwa aina zote za vielezi vya Kiswahili vina uwezo wa kutokea mwishoni mwa kishazi bila vizingiti vyovyote. Vielezi husika vinatokea baada ya kitenzi kwa kuwa vimedhibitiwa na kirai kitenzi ambacho kimebeba vielezi hivyo. Hata hivyo, vielezi vinaweza kutokea katika sehemu nyingine ya kishazi kupitia mchakato wa uhamisho kama inavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo.

3.2.2 Uhamisho wa Kielezi katika Kishazi cha Kiswahili

Taarifa kuhusu msingi wa nadharia ilidokeza kuwa uhamisho ni hatua ya uundaji wa kishazi unaohusu usogezi wa kijenzi cha kisintaksia kutoka pahala pake pa awali hadi kituo kipyaa (Taz. §1.7.1.3). Kulingana na kanuni ya ulafi, kijenzi kinaweza kuhama kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji yake ya kimofolojia au sarufi kwa jumla.

Kwa mujibu wa Chomsky (1968), kunazo aina mbili za uhamisho ambazo ni uhamisho wa kijenzi na uhamisho wa hoja. Utafiti huu umeshughulikia uhamisho wa kielezi kama kijenzi katika kishazi cha Kiswahili.

Uhamisho ambao umeangaziwa na tafiti nyingine hasa unahusu kirai nomino. Hata hivyo inabainika kuwa kirai kielezi pia kinaweza kuhama kutoka upande wa kulia wa kishazi hadi sehemu ya mbele kushoto. Poletto na Pollock (2004) wanadhihirisha jinsi kielezi cha Kiitaliano kinaweza kuhama hadi mzingo wa kushoto wa kishazi. Bassong (2010) anaeleza kuhusu uhamisho fokasi na uhamisho mada wa kielezi na anasema kuwa uhamisho fokasi hurejelea kusonga kwa kijenzi hadi mwanzo wa kishazi ili kuleta msisitizo na kuleta habari mpya kwa anayepokea habari.

Uhamisho mada vilevile hurejelea kusonga kwa kijenzi hadi mwanzo wa kishazi ingawa sasa kijenzi hicho kinabeba ujumbe ambao tayari unafahamika. Cinque (1999) anasema kwamba uhamisho wa vielezi kwa jumla unaweza kutokana na kuhama kwa kitenzi. Hata hivyo, haelezi kwa udhahiri sababu za kuhama kwa kielezi na pahali ambapo kielezi kinahamia. Ernst (2004) anasisitiza kuwa vielezi hutokea katika sehemu tofautitofauti za kishazi kutegemea dhima zao za kisemantiki ingawa pia haelezi ni kwa nini maana ya vielezi hutofautiana kulingana na mazingira ambamo kielezi kinapatikana katika kishazi.

Sehemu hii itaangazia uhamishaji mbele wa kielezi cha Kiswahili. Uhamishaji mbele unarejelea kusonga kwa kijenzi kutoka sehemu ya kulia ya kishazi hadi mzingo wa kushoto wa kishazi. Michakato hii ya usongeshaji inasababishwa na uhamisho fokasi

na uhamisho mada wa kielezi. Data ya utafiti huu imedhihirisha kuwa kielezi cha Kiswahili kinapohama huwa kinatua ndani ya kishazi kisha kinahama tena hadi mwanzo wa kishazi. Hivyo basi sehemu hii itadhihirisha sababu za kuhama kwa kielezi na pahali ambapo kielezi kinahamia.

3.2.2.1 Vielezi Vinavyotokea Ndani ya Kishazi


Vielezi vinaweza kutokea ndani ya kishazi. Nafasi ya ndani ya kishazi inarejelea nafasi hasa kati ya kiima na kitenzi. Kielezi kinaweza kufuata nomino, kivumishi, au kihusishi kinachotokea kabla ya kitenzi. Kielezi kinapotokea ndani huweza kuwa sehemu hiyo ni pahali pake pa kawaida au huweza kuwa kimehama kutoka mwisho wa kishazi. Mifano ifuatayo inabainisha vielezi vinavyotokea ndani ya kishazi:

2a) Wanafunzi werevu *sana* wametuzwa.

b) Mti mrefu *zaidi* umekatwa.

Vishazi 2a na b vinajumuisha vielezi vya namna ambavyo ni *sana* na *zaidi*. Vielezi husika vimetokea kabla ya kitenzi. Inabainika kuwa vielezi vilivyorejelewa ni halisi na vinaeleza zaidi kuhusu vivumishi *werevu* na *mrefu* mtawalia. Kielezi kinachotokea ndani ya kishazi kinawakilishwa katika kielelezo kifuatacho:

Kielelezo 3.5: Kielezi Kinachotokea Ndani ya Kishazi



Kielelezo hiki kinadhihirisha kuwa kielezi *sana* kinapatikana ndani ya kishazi katika pahali pake pa kawaida kwa sababu kinatoa habari zaidi kuhusu kivumishi ambacho kimeambatana nacho. Hata hivyo kielezi husika kinapoeleza zaidi kuhusu vitenzi au vielezi vingine, basi kitatokea mwishoni mwa kishazi kwa mfano,


3a) Mtoto amelia *sana*.

b) Mtoto ameanguka vibaya *sana*.

Kielezi *sana* katika kishazi 3a kinaeleza zaidi kuhusu kitenzi. Iwapo kielezi husika kitatokea kwingine, kwa mfano *sana mtoto amelia* au *mtoto sana amelia*, kishazi hakitakuwa sanifu. Katika kishazi 3b, kielezi kinaeleza zaidi kuhusu kielezi kingine, iwapo kitatokea katika sehemu nyingine kishazi hakitakuwa sanifu. Hii ina maana kuwa vielezi vinavyotokea ndani ya kishazi hasa ni vile vinavyoeleza zaidi kuhusu kivumishi kinachotoa habari zaidi kuhusu nomino. Katika mchakato wa uhamisho, vielezi vinaweza kutua ndani ya kishazi kisha viendeleo kuhama hadi sehemu ya mwanzo wa kishazi kama mfano 4 unavyodhihirisha.


4a) Wanafunzi walichelewa *juzi*.

4b) Wanafunzi *juzi* walichelewa _____



Kielezi <*juzi*> katika kishazi <*wanafunzi walichelewa juzi*> kimetokea mwishoni mwa kishazi. Hata hivyo, kinaonekana kuhama hadi ndani katika kishazi *wanafunzi juzi walichelewa* ambapo kimetokea kati ya kiima <*wanafunzi*> na kitenzi <*walichelewa*>. Kielezi hiki hakionekani kuwa katika sehemu yake maalumu kwa kuwa kimetua tu pale lakini kinaendelea kuhama hadi mwanzoni mwa kishazi. Kwa sababu hiyo hakionekani kuwa sahihi. Kielelezo 3.6 kinawakilisha kishazi chenyewe:

Kielelezo 3.6: Wakati Kinachotokea Ndani ya Kishazi



Kielelezo 3.6 kinadhihirisha namna ambavyo kielezi kinaweza kuhama mbele lakini kabla ya kutua katika sehemu ya mwanzo wa kishazi, kinatua ndani kisha kinasonga hadi kitangulie kiima ili kutimiza kanuni ya masafa mafupi katika Sintaksia Finyizi. Kanuni hii inahitaji kijenzi kisonge hatua chache iwezekanavyo na kwa hivyo kielezi kinaendelea kuhama hadi mzingo wa kushoto wa kishazi.

Vishazi vilivyorejelewa katika sehemu hii vinadhihirisha kwamba baadhi ya vielezi vya Kiswahili vina uwezo wa kutokea ndani ya kishazi bila ugumu wowote. Vielezi vya wakati na namna ndivyo vinaonekana kuwa huru zaidi. Vielezi vya idadi na mahali vinaonekana kusababisha vishazi visivyo sanifu vinapotokea ndani ya kishazi kinyume na lugha zingine kama vile Kiingereza ambapo vielezi vya idadi hutokea ndani ya kishazi bila ugumu wowote. Vielezi vinavyotokea ndani ya kishazi vinabainika kutua tu kisha vinahama mwanzoni mwa kishazi kama inavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo.

3.2.2.2 Kielezi Kinachotokea Mwanzoni mwa Kishazi

Kielezi kinaweza kutokea mwanzoni kwa kutangulia kiima na vipashio vingine vyote katika kishazi kupitia uhamisho fokasi na uhamisho mada. Hata hivyo, si vielezi vyote ambavyo vinaweza kuhama kama mada (M) au fokasi (F). kuna vielezi ambavyo vinahama tu kama mada wala si fokasi. Haya yatadhihirishwa katika sehemu hii. Mfano wa kishazi kilicho na kielezi mwanzoni ni kama vile:

5a) Wanafunzi walichelewa juzi.


b) Wanafunzi *juzi* walichelewa.

c) *Juzi* wanafunzi walichelewa

Kielezi kilichotajwa ni cha wakati. Kielezi husika kimefanywa kuwa mada kisha kikasonga hatua kwa hatua kutoka mwisho wa kishazi hadi mwanzo. Kielezi <*juzi*> katika kishazi <*juzi wanafunzi walichelewa*>, kwa mfano, kinatangulia kiima. Ingawa kielezi husika hakijakaribiana na kitenzi <*walichelewa*>, uhusiano wa kategoria hizi

mbili unadhihirika kwa kuwa kielezi kinatoa habari zaidi kuhusu kitenzi kwa kueleza kitendo kilitendeka lini. Kielelezo 3.7 kinawakilishwa uhamisho mada.

Kielelezo 3.7: Uhamisho wa Kielezi Kinachodhihirisha Mada




Sehemu msingi ya kielezi <juzi> huwa mwishoni mwa kishazi lakini kimehama hadi mwanzoni na kufanywa kuwa mada ili kuleta msisitizo. Kwa hivyo katika kishazi <wanafunzi walichelewa juzi>, mada ni mtendaji (wanafunzi). Kielezi juzi kinapohama mwanzoni, ina maana kuwa habari inayotolewa hasa inahusu wakati. Huu ni uhamisho mada kwa kuwa habari inayotolewa na kielezi juzi si mpya bali tayari inafahamika vilevile maana ya kishazi haibadiliki. Nadharia ya Sintaksia Finyizi inasema kuwa kijenzi hakihami ovyo, lazima kuwepo sababu ambayo inakifanya kihame kutoka sehemu ya kawaida hadi sehemu nyingine. Sababu ya

kuhama kwa kielezi *juzi* katika kishazi kilichorejelewa ni kutimiza uamilifu wa kisarufi kwa kukifanya kuwa muhimu kuliko vijenzi vingine. Hata hivyo, kielezi kinapohama katika kishazi kilichorejelewa, maana ya kishazi hicho haibadiliki. Sintaksia Finyizi pia inasema kuwa kijenzi kinapohama huacha hame mahali kilipotoka. Aidha, kijenzi kinachohama huanza sehemu ya chini hadi sehemu ya juu na uhamisho hupitia masafa mafupi. Kielelezo 3.7 kinadhihirisha mahali ambapo kielezi kimetoka na kuacha hame, kielezi husika kinahama kutoka chini upande wa kulia hadi juu upande wa kushoto. Kielelezo pia kinaonyesha kuwa kielezi kimepitia masafa mafupi kwa kutua ndani ya kishazi kisha kikahama tena hadi mwanzoni mwa kishazi.

Kielezi *juzi* pia kinaweza kufanywa kuwa fokasi kisha kikasonga hadi mwanzo ili kuleta habari mpya katika kishazi. Kishazi 2a kitabadilika kuwa <*Ni juzi wanafunzi walichelewa*>. Kirai fokasi (KF) katika Kielelezo 3.8, kinadhihirisha uhamisho fokasi.

Kielelezo 3.8: Uhamisho wa Kielezi Kinachowakilisha Fokasi



Kielelezo hiki kinadhihirisha neno ambalo limelengwa katika kishazi. Neno hilo ni *juzi* kielezi hiki kinatokea mwanzoni kama habari mpya ambayo haikuwa ikifahamika awali. Katika uhamisho mada, neno ambalo linahamishwa huwa limebeba maana ambayo tayari inafahamika.

Sehemu hii imebainisha kuwa baadhi ya vielezi vinaweza kutokea mwanzoni. Vielezi vya wakati na namna ndivyo vinadhihirika kuwa huru zaidi kuliko vielezi vingine. Data ya utafiti inaonyesha kuwa ni nadra kwa vielezi vya idadi na vya mahali kutokea mwanzoni kama mada. Vielezi husika hutokea mwanzoni hasa katika mazungumzo yasiyo rasmi. Aidha, vielezi vya uhakika kama vile *kimsingi, kwa kweli* vinaweza kuhama kama mada lakini haviwezi kuhamishwa kama fokasi. Kishazi: <*kimsingi, shule zote zitafungwa*> kwa mfano, kimebeba kielezi *kimsingi* ambacho kimehamishwa kama mada. Kishazi husika hakiwezi kuwa <*ni kimsingi shule zote*

zitafungwa. Hii ina maana kuwa kielezi husika hakiwezi kuhama mbele kama fokasi. Hivyo basi baadhi ya vielezi vinaweza kuhamishwa mbele au kwenye mzingo wa kushoto wa kishazi kama mada na kama fokasi. Vielezi vya wakati kama vile *leo, jana, kesho, na juzi* ndivyo vina uhuru zaidi wa kuhama kama mada na fokasi. Vielezi vingine hubakia katika sehemu yao ya kawaida ambayo ni mwishoni mwa kishazi ili kutimiza uamilifu wa kuwa chagizo.

Kayne (1994), Alexiadou (1997, na Cinque (1999) wanaeleza kuwa kielezi katika lugha mbalimbali kinaweza kuwa chagizo au kitangulizi. Kielezi huwa chagizo iwapo kimetokea mwishoni mwa kishazi hasa baada ya kitenzi. Vielezi husika vinaweza kuhama hadi sehemu ya mwanzo wa kishazi na kutokea kama kitangulizi. Utafiti huu unakubaliana na maelezo ya Kayne, Alexiadou na Cinque (weshatajwa) kuwa kielezi huwa chagizo na husonga kutoka mwisho wa kishazi hadi mwanzoni mwa kishazi. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na wataalamu hao kwa kudhihirisha kuwa kielezi kinapohama kinatokea mwanzoni kama mada au fokasi ili kusisitiza ujumbe unaotolewa na kielezi wala si kama kitangulizi.

Utafiti wa Cinque (1999) kuhusu msambao wa vielezi katika lugha mbalimbali, unadhihirisha kuwa vielezi hutokea katika sehemu maalumu. Utafiti huu unakubaliana na Cinque (keshatajwa) kwa kuonyesha kuwa baadhi ya vielezi vya Kiswahili hutokea katika sehemu maalumu tu. Vielezi vinavyotoa habari zaidi kuhusu vivumishi na vielezi vingine haviwezi kusogezwa hadi sehemu nyingine. Katika kishazi *<mtaalamu yule ameandika vitabu vingi vizuri zaidi>*, kielezi *zaidi* hakiwezi kuhama na kutangulia kiima. Iwapo kitahamishwa kitasababisha kishazi kisicho sanifu kama vile **<zaidi mtaalamu yule aliandika vitabu vizuri>*. Hii ina maana kuwa, vielezi


vinavyohama hasa ni vile ambavyo vimedhibitiwa na kichwa ambacho ni kirai kitenzi. Kwa kawaida kielezi kinatokea karibu na kichwa ambacho kimebeba kielezi hicho na kwa hivyo kinapobebwa na kirai kitenzi, kitatokea karibu na kitenzi, kinapobebwa na kirai vumishi, kitatokea karibu na kivumishi, na kinapobebwa na kielezi kingine basi kitatokea karibu na kielezi.

Aidha, kunavyo vielezi ambavyo kawaida hutokea mwanzoni mwa kishazi. Kwa mfano vielezi kama vile *siku hizi, kawaida* hutokea mwanzoni hasa vinapotumika kama viashiria matini ili kuunganisha mazungumzo ya awali na ya sasa kwa kusudi la kudumisha mawasiliano. Sababu nyingine ya kuhama kwa vielezi ni kuwa, vielezi zaidi ya kimoja vinapotokea mwishoni mwa kishazi kama kirai kielezi, vielezi hivyo vinaweza kupunguzwa na kuhamishwa mwanzoni ili kuondoa ufululizaji wa vielezi vingi katika sehemu moja. Uhamishaji wa aina hii umerejelewa katika utafiti huu kama uhamisho usio mkamilifu.

3.2.2.3 Uhamisho Usio Mkamilifu wa Kirai Kielezi


Kama ilivyoelezwa awali, sehemu ya kirai kielezi inaweza kuhamishwa na kuacha sehemu nyingine mwishoni mwa kishazi. Kishazi <*Rais aliwasili mjini mapema sana leo*> kimebeba kirai kielezi chenye vielezi vinne. Kishazi hiki kinaweza kupitia mchakato wa uhamisho na kubadilika kuwa <*Leo mapema sana, rais aliwasili mjini*> au < *Leo, rais aliwasili mjini mapema sana*>. Sehemu hii itaangazia uhamisho wa sehemu ya kirai elezi. Kielelezo 3.9 kinawakilisha kishazi <*rais aliwasili mjini mapema sana leo*>

Kielelezo 3.9: Wingi wa Kielezi katika Kishazi Kimoja



Kirai kielezi kilichorejelewa kinaweza kupunguzwa kwa kuhamisha kielezi *leo* ambacho ni sehemu ya kirai <*mjini mapema sana leo*> hadi mwanzoni mwa kishazi ili kuunda kishazi <*leo rais aliwasili mjini mapema sana*>. Kielelezo 3.10 kinadhihirisha kishazi husika.


Kielelezo 3.10: Uhamisho wa Kielezi Kimoja Miongoni mwa Vielezi Vingi



Kielelezo 3.10 kinadhihirisha uhamisho usio mkamilifu. Kielezi kimoja ambacho ni *leo*, kimesonga na kutangulia maneno mengine katika kishazi ili kusisitiza wakati wa kutendeka kwa kitendo. Vielezi vingine katika kishazi kilichorejelewa havihami kwa kuwa hakuna sababu ya kuhama kwa vielezi hivyo na kwa hivyo vinabaki kwenye kirai tenzi. Kielezi cha wakati *leo* kinaonekana kuwa na uhuru wa kutokea sehemu mbalimbali. Aidha kielezi cha namna kama *sana* hakina uhuru wa kutokea katika sehemu mbalimbali. Hii ni kwa sababu tayari kinaleta msisitizo katika sehemu yake ya kawaida. Iwapo tutahamisha vielezi *sana* hadi mwanzoni, kwa mfano <*sana leo rais aliwasili mjini mapema*> kishazi kitasikika kutokuwa sahihi. Hii ina maana kuwa kuna vielezi ambavyo vina ukuruba zaidi vikiwekwa pamoja kuliko vingine. Kielezi *sana* hakikubali kuhama ila iwapo kitaambatishwa na vielezi vingine. Kwa mfano kishazi <*rais aliwasili mjini mapema sana leo*> kimebeba kirai elezi <*mjini mapema*

sana leo>. Sehemu ya kirai husika inayoweza kuhamishwa ni <*mapema sana leo*>. Kielelezo 3.11 inadhihirisha namna sehemu hiyo inahamishwa.

Kielelezo 3.11: Uhamisho wa Kirai Kielezi



Katika kishazi kilichorejelewa, vielezi vitatu vinahama na kuacha kielezi kimoja mwishoni. Hii ina maana kuwa kielezi kama vile *sana* ambacho huwa hakihami kinaweza kuhama iwapo kitaambatana na vielezi vingine. Aidha kielezi *leo* kinaonekana kuwa na ukuruba zaidi na vielezi vingine. Kielelezo 3.11 kinadhihirisha uhamisho usio mkamilifu wa kirai kielezi.

Sehemu hii imeangazia uhamisho usio mkamilifu wa kirai kielezi. Inabainika kuwa sehemu ya kirai kielezi kinaweza kuhamishwa ili kupunguza ufululizaji wa vielezi

katika kishazi kimoja. Utafiti huu pia umebainisha kuwa vielezi vya aina mbalimbali huwa na mpangilio maalumu vinapotokea pamoja katika kishazi. Sehemu ifuatayo itaangazia mpangilio msonge wa vielezi katika kishazi.

3.2.3 Mpangilio Msonge wa Vielezi katika Kishazi cha Kiswahili

Data ya utafiti inaonyesha kwamba vielezi vingi vya aina mbalimbali vinaweza kutokea pamoja katika kishazi cha Kiswahili. Kama ilivyokwishajadiliwa, kunavyo vielezi ambavyo huwa katika sehemu maalumu tu na kunavyo vielezi ambavyo huweza kusonga hadi sehemu nyingine ya kishazi. Kulingana na Cinque (1999), vielezi havitokei ovyo katika kishazi bali huwa na mpangilio wa kimsonge: vielezi vilivyo katika sehemu ya juu ya msonge na vile vilivyo katika sehemu ya chini ya msonge.

Data ya utafiti huu inaonyesha kuwa vielezi vya Kiswahili pia hupangika kimsonge katika kishazi. Kishazi *<msanii alibebwa hobelahobela mara mbili jana jioni ukumbini>* kinaonyesha kuwa kielezi cha namna *hobelahobela* kimetangulia vielezi vingine, kikifuatwa na kielezi cha idadi *marambili* kisha kielezi cha wakati *jana jioni* na mwisho ni kielezi cha mahali *ukumbini*. Mfano mwingine unaojitokeza katika data ya utafiti ni: *<wachezaji wanacheza vizuri sana uwanjani>*. Sawa na kishazi kilichotangulia, kishazi hiki kinabainisha kuwa kielezi cha namna *vizuri* kinatangulia kielezi cha kiasi *sana* na kielezi cha mahali *uwanjani* kinatokea mwishoni baada ya kielezi cha kiasi. Hata hivyo kutokana na uhamisho kama ilivyojadiliwa awali, kielezi cha mahali kinaweza pia kutokea kabla ya kielezi cha wakati kama inavyodhihirishwa katika vishazi *<msanii alibebwa hobelahobela marambili ukumbini jana jioni>*.

Vilevile, kielezi cha mahali kinaweza kutangulia kielezi cha namna kwa mfano <*wachezaji wanacheza uwanjani vizuri sana*>.

Vielezi vya namna vinadhihirika kutokea katika sehemu ya juu ya msonge kwa sababu vinakaribiana na kitenzi katika kishazi cha Kiswahili. Vielezi vya mahali, vya kiasi na vya wakati vinadhihirika kutokea katika sehemu ya chini. Hata hivyo, vielezi vya wakati vinaweza kutokea kabla na baada ya vielezi vingine bila tatizo. Kishazi <*wakulima wameenda shambani mapema sana*> kimesheheni vielezi vitatu: kielezi cha mahali *shambani*, kielezi cha wakati *mapema*, kielezi cha kiwango *sana*. Kielezi cha mahali kinadhihirika kuwa katika sehemu ya juu ya msonge kuliko kielezi cha wakati na kielezi cha kiwango *sana* ambacho kinafafanua kielezi cha wakati *mapema*. Hii ina maana kuwa vielezi vinavyofafanua vielezi vingine huwa katika sehemu ya chini ya kishazi.

Data ya utafiti pia inaonyesha kuwa vielezi viwili vya mahali vinapofuatana kwa mfano <*watalii watazuru mji wa Mombasa nchini Kenya*>, kielezi kinachorejelea eneo dogo hutangulia kielezi kinachorejelea eneo kubwa. Aidha, vielezi vya wakati vinapofuatana kwa mfano <*tutafanya mtihani saa moja asubuhi*>, wakati kamili hutangulia wakati usiodhahiri. Kama ilivyojadiliwa na Cinque (1999), utafiti huu unabainisha kuwa vielezi vya Kiswahili vinadhihirisha mipangilio ya kimsonge ifuatayo:

- i. Vielezi vya namna > vielezi vya kiasi> vielezi vya wakati> vielezi vya mahali
- ii. Vielezi vya wakati> vielezi vya namna> vielezi vya kiasi> vielezi vya mahali

Vielezi vya namna huwa sehemu ya juu ya msonge vikifuatwa na vielezi vya kiasi kisha vielezi vya wakati na mwisho ni vielezi vya mahali ambavyo hutokea katika sehemu ya chini ya msonge. Vielezi vya wakati pia huweza kutangulia vielezi vingine vyote katika kishazi.

3.3 Hitimisho

Sura hii imeangazia maumbo ya kielezi kutokana na uundaji. Inabainika kuwa vielezi vinagawika katika vikundi viwili: vielezi sahili na vielezi changamano. Vielezi sahili ndivyo vielezi msingi na vimeundwa kwa mofimu huru. Vielezi husika ni vichache mno. Vielezi changamano vinajumuisha hasa vielezi vinavyozalishwa kutoka kategoria zingine za maneno. Vielezi hivi vinaundwa kwa kuchopeka viambishi au faridi peke kwa kategoria zingine za maneno. Sura hii pia imemulika muundo wa kisintaksia wa kielezi na inabainika kuwa baadhi ya vielezi vina uwezo wa kutokea sehemu yoyote ya kishazi ilhali kuna vielezi ambavyo hutokea katika sehemu fulani tu. Katika uchanganuzi muktadha wa kielezi, inadhihirika kuwa kielezi hutokea mwishoni mwa kishazi lakini kinaweza kuhama hatua kwa hatua hadi mwanzoni mwa kishazi. Imebainika pia kuwa vielezi vya Kiswahili vinapangika kimsonge katika kishazi vinapotokea pamoja. Uchanganuzi muktadha wa kielezi cha Kiswahili umedhihirisha kuwa mazingira ambamo kielezi kinatokea huweza kutegemea maana ya kielezi husika. Hivyo basi sura inayofuata itachanganua uamilifu wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili.

SURAYANNE

UAMILIFU WA KIELEZI KATIKA KISHAZI CHA KISWAHILI

4.0 Utangulizi

Uamilifu unarejelea kazi ifanywayo na kipashio katika muundo, umbo la neno au miundo ya sentensi. Katika kuchanganua uamilifu wa kielezi, dhima za kisemantiki zitaangaziwa. Dhima za kisemantiki hurejelea mahusiano ya kimaana yanayodhihirika baina ya kitenzi na vipashio kama kielezi na nomino ambavyo vinatawaliwa na kitenzi kinachohusika. Haegeman (1994), Radford (1997) na Yule (2011) wanatambua mahusiano yafuatayo yanayodhihirishwa na maneno kwa jumla: mtendi, maudhui, hisifu, mfaidi, mahali, hatima, chanzo, na ala. Quirk na wenzake (1985) wanasema kwamba kielezi kwa jumla kinadhihirisha dhima zifuatazo: dhima ya mahali, utaratibu, wakati, na kiasi. Kwa kuongozwa na kanuni ya dhima maana katika Sintaksia Finyizi, utafiti huu unanuia kubainisha dhima za kielezi zilizopo katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya dhima hizi zilikuwa zimeangaziwa katika uchanganuzi muktadha na uundaji wa kielezi kwa kuwa maana za vielezi ndizo zimetumika hasa kuweka vielezi hivyo katika vikundi mbalimbali. Sehemu ifuatayo itashughulikia dhima zinazodhihirishwa na kielezi cha Kiswahili.

4.1 Dhima ya Mahali


Kwa mujibu wa Fasano (2014), mahali hurejelea sehemu ambayo kitendo kimetendeka na kwa kawaida hujibu swali ‘wapi’. Katika lugha ya Kiswahili, maneno kamili au viambishi huweza kutumiwa ili kudhihirisha mahali kitendo kimetendeka. Kulingana na data ya utafiti, dhima ya mahali inajumuisha pahali panapodhihirika,

pahali pasipodhihirika, mwelekeo, hatima, chanzo, na umbali.

4.1.1 Pahali Panapodhihirika

Mahali panapodhihirika ni dhima inayobainishwa na kielezi cha Kiswahili. Dhima husika hurejelewa kwa kutumia maneno kamili, kwa mfano, neno #*Kampala*# katika kishazi <*babake anaishi Kampala*> linarejelea mahali maalumu. Kielelezo kifuatacho kinawakilisha dhima husika katika kishazi.

Kielelezo 4.1: Kishazi chenye Kielezi cha Dhima ya Pahali Panapodhihirika



Kielelezo 4.1 kimebeba kielezi *Kampala* kinachodhirisha dhima ya mahali. Kielezi husika kinajibu swali <*babake anaishi wapi*> na kinatambulisha pahali panaporejelewa katika kishazi. Kielezi husika ni muhimu katika kishazi kwa kuwa iwapo kitaondolewa kishazi hakitakuwa kamilifu kimaana. Hivyo basi kinaongeza habari katika kishazi.

4.1.2 Pahali Pasipodhihirika

Mahali pasipodhihirika hurejelea mahali ambapo si mahsus. Data ya utafiti inadhahirisha kuwa maneno kama vile *juu, chini, mbele, nyuma, kando*, na *katikati* huweza kutumika ili kurejelea mahali ingawa mahali penyewe hapatambuliwi hasa ni wapi. Kishazi <*Juma ameketi nyuma*> kwa mfano, kinajibu swali ni wapi kitendo kimetendeka. Kielezi *nyuma* kinatoa habari kuhusu mahali kitendo kimetendeka ingawa mahali hapo hapadhahiriki hasa. Vilevile kinarejelea eneo pana.

4.1.3 Mwelekeo

Dhima ya mahali pia inajumuisha mwelekeo. Data ya utafiti inabainisha kuwa dhima ya mwelekeo inajumuisha matumizi ya vielezi vinavyoambatana na vitenzi kama vile kuelekea, kuteremka, na kupanda ili kudhihirisha upande kitendo kinatendeka. Kishazi <*mbuzi wamepanda mlima*> kinadhahirisha mwelekeo wa kutendeka kwa kitendo. Neno *mlima* ni nomino inayorejelea pahali panapodhihirika lakini kwa kuwa nomino yenyewe inaeleza zaidi kuhusu kitenzi *panda* basi kitafanya kazi ya kielezi. Kishazi <*magaidi wameelekea mashariki*> pia kinaonyesha mwelekeo sawa na kishazi <*wanariadha wameteremka chini*>. Katika vishazi vilivyorejelewa, Kitenzi ndicho kinasaidia katika kutofautisha kati ya mahali panapodhihirika na mwelekeo.

4.1.4 Hatima

Dhima ya mahali vilevile inajumuisha hatima. Dhima hii inakaribiana mno na dhima ya mwelekeo. Hatima ina maana kuwa kitendo kilianza mahali fulani na kwa hivyo kimefikia mwisho. Kielezi #*sokoni*# katika kishazi <*wanabiashara wameenda sokoni*> kinaonyesha hatima ya kitendo *enda*. Kishazi husika kinajumuisha neno

sokoni ambalo kimsingi ni nomino lakini kinapoambishwa kinafanya kazi ya kielezi. Kielezi husika kinaonyesha mahali ambapo wanabiashara wameenda. Dhima ya hatima hasa hudhihirishwa na kitenzi kinachotumika pamoja na kielezi. Kwa mfano, kitenzi *kwenda* kinapoambatana na kielezi hudhihirisha dhima ya hatima.

4.1.5 Chanzo

Dhima ya chanzo pia inabainishwa katika kielezi cha Kiswahili. Kishazi <*wanafunzi wanatoka shuleni*> kinaeleza mahali ambapo wanafunzi walikuwepo kabla ya kuanza safari ya kwenda. Kielezi *shuleni* kinadhihirisha dhima ya chanzo. Sawia na dhima ya hatima, dhima ya chanzo inategemea hasa kitendo ambacho kimeambatana na kielezi. Kitenzi toka hudhihirisha dhima ya chanzo kinapotumika pamoja na kielezi katika kishazi.

4.1.6 Umbali

Umbali ni dhima nyingine inayodhihirishwa na kielezi cha Kiswahili. Dhima husika huonyesha *karibu* au *mbali* na pahali ambapo kitendo kimetendeka kama inavyodhihirishwa na vishazi <*wanaishi karibu na mto Tana*> na <*wanafunzi wanasafiri mbali*>. Dhima husika hurejelea kipimo kutoka mahali panaporejelewa na mahali kitendo kimetendeka au mahali alipo mzungumzaji hadi pahali anapoelekea.

Sehemu hii imeangazia dhima za mahali zinazodhihirishwa na kielezi cha Kiswahili. Dhima hizi, kwa jumla zinajibu swali *wapi* na hivyo hutupa habari kuhusu mahali ambapo kitendo kimetendeka. Dhima nyingine ya kisemantiki inayodhihirishwa na kielezi cha Kiswahili ni dhima ya utaratibu.

4.2 Dhima ya Utaratibu

Dhima ya utaratibu hueleza jinsi kitendo kimefanyika (Leech & Svartvik, 2002). Hujibu swali *vipi* katika kishazi. Kulingana na data ya utafiti, dhima ya utaratibu huweza kugawika katika vikundi vitatu ambavyo ni namna, njia na ala na vinafafanuliwa zaidi katika sehemu ifuatayo.


4.2.1 Namna

Dhima ya namna hurejelea jinsi ambavyo kitendo kimetendeka. Kwa mfano, katika kishazi <*Mwajuma huzungumza vizuri*>, kielezi #*vizuri*# kinajibu swali *vipi* na kinatoa habari zaidi kuhusu jinsi ambavyo kitendo kimetendeka. Dhima ya namna inaweza kudhihirishwa pia kwa matumizi ya maneno yanayoiga sauti au mlio wa kitu kwa mfano *bwe!* katika kishazi <*mbwa alibweka bwe*>, pamoja na maneno yanayofananisha kitendo na mtendaji kama vile <*wanasiasa wanapora mali kifisi*> neno *kifisi* kinaeleza namna kitendo kilitendeka.

4.2.2 Ala

Dhima ya *ala* inarejelea kifaa ambacho kimetumika katika kutekeleza kitendo. Kishazi <*mgonjwa amedungwa sindano*> kinaonyesha chombo ambacho kimetumika kutenda kitendo. Kielelezo 4.2 kinawakilisha dhima iliyorejelewa.

Kielelezo 4.2: Kishazi chenye Kielezi cha Dhima ya Ala



Neno *sindano* ni nomino lakini katika Kielelezo 4.2, linafanya kazi kama kielezi kwa kuwa kinaeleza chombo kilichotumika kutekeleza kitendo. Kirai husishi kinaweza pia kutumika kama kielezi kinachobainisha dhima ya ala. Katika kishazi <*tulisafiri kwa ndege*> Neno #*ndege*# ni nomino lakini linapoambatanishwa na *kwa* litafanya kazi ya kielezi kwa kueleza kifaa kilichotumika kutenda kitendo cha kisarufi na linajibu swali *vipi*.

4.3 Dhima ya Wakati

Dhima ya wakati hurejelea vielezi vinavyoeleza wakati ambao kitendo kilitendeka, kinatendeka au kitatendeka (Fasano, 2014). Hujibu swali *lini* katika kishazi. Data ya utafiti inadhihirisha vikundi vitatu vya vielezi vya wakati: vielezi vya wakati dhahiri, vielezi vya wakati usiodhahiri, na vielezi vinavyorejelea kipindi au muda fulani.

4.3.1 Vielezi vya Wakati Dhahiri

Vielezi vya wakati dhahiri katika lugha ya Kiswahili ni vingi na hujumuisha majira ya siku kama vile *asubuhi*, *jioni*, na *adhuhuri*. Katika kishazi <*Mkutano utaanza asubuhi*> kielezi *asubuhi* kinaeleza wakati wa kufanyika kwa kitendo. Neno *asubuhi* kwa kawaida, huwa nomino lakini linapojibu swali ni lini kitendo kilitendeka, basi kinakuwa kielezi. Vielezi vya wakati pia vinajumuisha majina yanayotaja siku kwa mfano, *kesho*, *leo*, *jana*, *Jumatatu*, na *Jumanne* pamoja na miezi kwa mfano *Januari* na *Februari*. Hata hivyo, nomino husika zinarejelewa tu kama vielezi iwapo vinatoa habari zaidi kuhusu kitenzi.


4.3.2 Vielezi vya Wakati Usiodhahiri

Vielezi vya wakati usio dhahiri vinajumuisha maneno kama vile *zamani*, *punde*, na *baadaye*. Kielezi *zamani* katika kishazi <*zahanati hii ilijengwa zamani*> kinatueleza wakati wa kutendeka kwa kitendo ingawa wakati maalumu haujadhihirishwa. Kielezi husika kinajibu swali *lini* ingawa hakibainishi ni wakati upi hasa ambapo kitendo kilitendeka. Data ya utafiti inaonyesha kuwa vielezi vinavyorejelea wakati usio dhahiri ni vichache mno katika lugha ya Kiswahili.

4.3.3 Vielezi Vinavyorejelea Muda

Data ya utafiti huu inadhihirisha kuwa vielezi vinavyorejelea muda kwa kawaida huwa fungu la maneno ambalo hutanguliwa na neno *kwa*. Kielezi *kwa miezi miwili* katika kishazi <*mtihani utafanywa kwa miezi miwili*> kinatupa habari kuhusu kipindi cha kutendeka kwa kitendo. Kielelezo 4.3 kinadhihirisha dhima ya muda.

Kielelezo 4.3: Kishazi chenye Kielezi cha Dhima ya Muda



Kirai husishi *kwa miezi miwili* katika Kielelezo 4.3 kinafanya kazi ya kielezi ili kudhihirisha dhima ya muda wa kutendeka kwa kitendo. Mifano zaidi ya vielezi vinavyodhihirisha dhima ya muda ni kama vile: *kwa muda mrefu*, *kwa siku tatu* miongoni mwa vingine.

Data ya utafiti pia inadhihirisha kuwa vielezi vya wakati hugawika zaidi katika vikundi vitatu; vielezi vya wakati uliopita, vielezi vya wakati uliopo, na vielezi vya wakati ujao. Vielezi vya wakati uliopita ni kama vile: *jana*, *juzi*, na *zamani*. Vielezi hivi hutumika pamoja na kiambishi /li/ ambacho huambatishwa kwenye kitenzi katika kishazi. Kishazi <*mahafala walifuzu jana*> kwa mfano, kinajumuisha kielezi *jana*. Kielezi husika kinashirikiana na kiambishi /li/ katika kitenzi *walifuzu* ili kudhihirisha wakati uliopita.

Kulingana na data ya utafiti huu, vielezi *sasa* na *leo* ndivyo vinatumika kurejelea wakati uliopo. Vielezi hivi hushirikiana na kiambishi /na/ ili kudhihirisha kinachotendeka katika wakati uliopo. Katika kishazi, <muuguzi anamhudumia mgonjwa sasa>. Kielezi *sasa* pamoja na kiambishi /na/ katika kitenzi *anamhudumia* vinadhahirisha wakati uliopo. Vielezi vinavyorejelea wakati ujao ni kama vile; *kesho*, *mtondo*, na *mtondogoo*. Vielezi hivi hutumika pamoja na kiambishi /ta/ ambacho kinaambatishwa kwenye kitenzi ili kuashiria wakati ujao. Kishazi <barabara itakarabatiwa kesho> kinajumuisha kielezi *kesho* ambacho kinashirikiana na kiambishi /ta/ katika kitenzi *itakarabatiwa* ili kudhihirisha wakati ujao. Inabainika pia kuwa baadhi ya vielezi huweza kurejelea nyakati zozote. Viambishi /li/, /na/ na /ta/ katika vitenzi ndivyo husaidia kutofautisha vielezi hivyo. Kwa mfano katika vishazi <mkutano utanza asubuhi> na <mkutano ulianza asubuhi> viambishi /ta/ na /li/ ndivyo vinasaidia katika kutofautisha wakati wa kutendeka kwa kitendo.

Sehemu hii imemulika vielezi vyenye dhima ya wakati na inadhihirika kuwa vielezi vya wakati hugawika katika vikundi vitatu: vielezi vya wakati dhahiri, wakati usiodhahiri na vielezi vya muda. Majina kama *asubuhi*, *kesho*, *Januari*, virai husishi pamoja na viambishi pia huweza kufanya kazi ya vielezi ili kutimiza dhima ya wakati. Aidha vielezi vinaweza kurejelea wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao.

4.4 Dhima ya Kiasi

Dhima za kisemantiki za kiasi hurejelea kuwepo kwa sifa fulani ambayo huweza kukadiriwa kwa viwango (Carter na wengine, 2011.) Ukadiriaji huu huweza kuzidisha au kupunguza sifa ya kitenzi, kivumishi au kielezi kinachohusika katika kishazi. Kulingana na data ya utafiti, vielezi vya kiasi hugawika katika vikundi viwili. Vielezi vya kuzidisha na vya kupunguza.

4.4.1 Vielezi vya Kuzidisha

Vielezi vya kuzidisha hurejelea kiwango cha juu cha kitendo kilichotendeka. Kwa mfano, kielezi *sana* katika kishazi <*Mtoto ameumia vibaya sana*> kinadhihirisha kiwango cha kitendo ambacho kimefanyika. Kielezi *sana* kinazidisha kiwango cha kutendeka kwa kitendo ambacho ni kuumia.

Kielezi cha kiasi huweza pia kuzidisha kiwango cha sifa ya nomino. Kwa mfano katika kishazi <*mti huo ni mrefu kabisa*>, kielezi *kabisa* kinazidisha kiwango cha urefu wa mti. Aidha, vielezi vya kiasi vinaweza kutoa msisitizo vinapotumiwa na vielezi vingine. Kwa mfano, kielezi *zaidi* katika kishazi <*askari anatembea haraka zaidi*> kinazidisha kiwango cha kutembea kwa askari.

4.4.2 Vielezi vya Kupunguza

Vielezi vya kupunguza hurejelea kiwango cha chini cha kutendeka kwa kitendo fulani. Kwa mfano, kielezi *kidogo* katika kishazi <*mtoto ameumia kidogo*> kinaeleza kiwango cha kuumia kwa mtoto. Kishazi kilichorejelewa kinatoa habari kuwa kitendo kimetendeka kwa kiwango cha chini. Hii ina maana kuwa mtoto aliumia lakini si

sana. Kulingana na utafiti huu, kielezi kimoja pekee ndicho kinadhihirisha dhima ya kiasi cha kupunguza. Dhima ya kiasi huweza pia kujumuisha vielezi vinavyojibu swali mara ngapi. Vielezi hivyo aghalabu huambatishwa na neno *mara* kwa mfano *mara tatu*, na *mara kadhaa*. Kishazi <*wanariadha hufanya mazoezi mara tatu kwa juma*> kinajumuisha kielezi *mara tatu* ambacho kinaeleza kiasi cha kutendeka kwa kitendo.

Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa Roux (2007) ambaye ameshughulikia uchanganuzi wa kisarufi wa kielezi katika lugha ya Kitswana. Roux (keshatajwa) anadhihirisha dhima mbalimbali za kielezi na anahitimisha kuwa dhima za kisemantiki za kielezi ndizo zinatumiwa katika kuainisha vielezi. Utafiti huu vilevile, unabainisha kuwa sifa bainifu za kielezi cha Kiswahili zinategemea hasa maana ya vielezi hivyo na kwa hivyo kuwezesha vielezi kugawanywa na kuainishwa katika vikundi vinne vikuu. Kutokana na dhima zilizoangaziwa, ambazo ni: dhima ya mahali, dhima ya utaratibu, dhima ya wakati, na dhima ya kiasi, tunapata vielezi vya mahali, vielezi vya namna, vielezi vya wakati na vielezi vya kiasi mtawalia.

Maelezo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa, kuna mwingiliano kati ya sintaksia na semantiki ya kielezi cha Kiswahili. Hii ni kwa sababu unapofahamu maana ya kielezi basi utakuwa na wepesi wa kufahamu kazi ya kielezi hicho katika kishazi. Kwa mfano, kielezi *sana* tayari inatupa habari kuhusu dhima ya kuzidisha na tunafahamu kuwa kinachozidishwa kinaweza kuwa kitenzi, kivumishi au kielezi. Hivyo basi kielezi *sana* kitatokea baada ya kitenzi, kivumishi au kielezi. Kwa mfano, katika kishazi <*mtoto ameumia sana*>, kielezi *sana* kinaeleza zaidi kuhusu kitenzi na kwa

hivyo kutokea baada ya kitenzi. Katika kishazi <*mti mrefu sana umekatwa*>, kielezi *sana* kinaeleza zaidi kuhusu kivumishi *mrefu* na kwa hivyo kutokea baada ya kivumishi husika. Katika kishazi <*shamba limelimwa vizuri sana*>, kielezi *sana* kinaeleza zaidi kuhusu kielezi vizuri. Kwa hivyo, maana ya kielezi inasaidia kufahamu uamilifu wa kielezi hicho katika kishazi. Kutokana na mwingiliano wa semantiki na sintaksia ya kielezi, utafiti huu una mtazamo kuwa, vielezi vinaweza kuainishwa kwa kuzingatia uamilifu wao katika kishazi ili kupata vielezi vya mwanzo, vielezi vya ndani na vielezi vya mwisho wa kishazi.

4.5 Hitimisho

Sura hii imeangazia dhima mbalimbali za kisemantiki ambazo vielezi husika vimedhihirisha. Dhima zilizobainishwa ni: dhima ya mahali, dhima ya utaratibu, dhima ya wakati, na dhima ya kiasi. Taarifa iliyoangaziwa inaonyesha kuwa dhima za kisemantiki za kielezi zimechangia katika uchanganuzi muktadha wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili. Hii ni kwa sababu uainishaji wa vielezi kwa kuzingatia maana zao umesaidia katika kueleza mazingira ambamo vielezi hivyo vinapatikana katika kishazi pamoja na kubainisha vielezi ambavyo vinaweza kuhama na vile ambavyo hudumu katika kishazi kama ilivyoelezwa katika sura ya tatu. Vishazi vilivyorejelewa katika utafiti vinadhihirisha kuwa vielezi vina majukumu muhimu katika kishazi cha Kiswahili.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza muundo na uamilifu wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili. Lengo kuu lilikuwa kuchanganua data ya vishazi huru vya Kiswahili kwa madhumuni ya kudhihirisha aina za vielezi vya Kiswahili, kubainisha maumbo ya kielezi cha Kiswahili kutokana na uundaji, kuchunguza dhima za kisemantiki zinazodhihirishwa na kielezi katika kishazi cha Kiswahili na kutathmini utoshelevu wa Sintaksia Finyizi katika kuchanganua kielezi katika kishazi cha Kiswahili.

Sura ya kwanza imeshughulikia utangulizi ambapo tumejadili mwelekeo wa utafiti wetu. Sura hiyo imejadili mambo ya kimsingi kuhusiana na utafiti. Haya ni pamoja na ufafanuzi wa istilahi muhimu, usuli wa mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada, upeo na mipaka ya utafiti, na mbinu za utafiti. Utafiti huu umeshughulikia swala la utafiti kupitia uchanganuzi ulioongozwa na nadharia ya Sintaksia Finyizi. Nadharia husika inajumuisha mihimili miwili ambayo ni hatua za uchanganuzi wa kishazi na kanuni zinazotawala muundo wa kishazi.

Sura ya pili iliingazia kishazi cha Kiswahili kwa kuchunguza namna ambavyo maneno yanahusishwa na kategoria mbalimbali kisha yanaungana kuunda kirai na hatimaye kishazi. Sura hii ilinua kujenga msingi wa uchanganuzi wa data kwa kuwa kielezi ni mojawapo wa kategoria za maneno. Sura ya tatu imeshughulikia umbo la kimofolojia pamoja na muundo wa kisintaksia wa kielezi. Sura hii ilidhamiria

kubainisha namna ambavyo kielezi kinaweza kutambuliwa katika kishazi cha Kiswahili na kudhihirisha msambao wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili. Sura ya nne imeshughulikia dhima za kisemantiki za kielezi cha Kiswahili.

5.1 Matokeo ya Utafiti

Katika sura ya pili, matokeo ya uchanganuzi wa kishazi huru cha Kiswahili yaliwasilishwa. Ilibainika kuwa muundo wa kishazi unategemea kategoria za maneno na virai. Ilidhihirishwa pia kuwa kategoria za maneno ya Kiswahili zinagawika katika vikundi viwili: kategoria leksia na kategoria sarifu. Ilielezwa kuwa kategoria leksia inajumuisha nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi, na kihusishi. Kategoria sarifu zinajumuisha kategoria za kibainishi, kipatanishi, na kishamirishi.

Uchanganuzi muundo wa kishazi cha Kiswahili, ulibainisha kuwa kupitia kanuni tegemezi muundo, maneno na virai vinavyojumuika pamoja katika muundo wa kishazi huwa na uhusiano tegemezi. Kanuni ya uhusika ilidhihirisha kuwa kielezi kina uhusiano na kategoria zingine za maneno na hivyo kinaweza kubebwa na virai mbalimbali kama vile kirai kitenzi, kirai kivumishi, na kirai kihusishi. Kanuni ya uhusika pia ilisaidia katika kutambua sifa za kisarufi za kielezi. Mbali na kanuni ya uhusika, ilidhihirishwa pia kuwa kanuni ya dhima maana ni muhimu katika kubainisha dhima za kisemantiki za kielezi. Idadi ya dhima ambazo kielezi kinadhihirisha katika kishazi cha Kiswahili ilibainishwa katika sura ya nne.

Katika kuchanganua maumbo ya kielezi, inabainika kuwa kielezi cha Kiswahili kinaweza kuwa na umbo sahili au umbo changamani. Maumbo haya yanatokana na namna vielezi vinaundwa. Vielezi vyenye umbo sahili ndivyo vielezi msingi na vielezi changamani huzalishwa kutoka kategoria zingine za maneno. Vielezi msingi ni vichache mno katika lugha ya Kiswahili na vinajumuisha maneno kama vile *sana*, *kabisa*, *ovyo*, *zaidi*, na *mno*. Vielezi vinavyozalishwa kutoka kategoria zingine vinajumuisha nomino ambazo zinaongezwa viambishi awali /ki/, au /u/ na kiambishi tamati /ni/. Vivumishi pia vinaweza kuongezwa kiambishi /ki/ au /vi/ ili kuunda vielezi. Aidha, kuna maneno ambayo ingawa kimsingi si vielezi, huweza kufanya kazi kama vielezi. Kwa mfano vihusishi hufanya kazi ya vielezi vinapojibu swali *wapi*, vielezi hivyo huitwa vihusishi elezi. Vilevile viigizi vinaweza kufanya kazi ya vielezi vinapojibu swali *vipi*. Nomino pia huweza kuwa vielezi vya mahali hasa vinapotumika kujibu swali *wapi*. Aidha vielezi huweza kuchukua umbo la urudufu ambapo leksimu hurudiwa mara mbili. Ilibainishwa kuwa ingawa vielezi huzalishwa, vielezi vyenyewe haviwezi kunyambuliwa na havina uwezo wa kubadilisha kategoria ya maneno ambayo yanaambatana navyo.

Inabainika pia kuwa, kielezi ni kategoria yenye upekee kwa kuwa kina sifa ya kuweza kutokea katika sehemu mbalimbali ya kishazi. Vielezi huweza kutokea mwanzoni mwa kishazi, ndani ya kishazi na mwishoni mwa kishazi. Sehemu msingi zaidi ya vielezi ni mwishoni mwa kishazi. Data ya utafiti ilidhihirisha kuwa vielezi vinavyotokea ndani ya kishazi ni vichache mno. Hata hivyo baadhi ya vielezi hutokea tu katika sehemu maalumu. Ilidhihirika pia kuwa nafasi inayochukuliwa na kielezi katika kishazi hutegemea hasa maumbo na dhima za kisemantiki za vielezi husika

kwa mfano vielezi vya wakati huweza kutokea mwanzoni mwa kishazi kinapokuwa na jukumu la kuleta msisitizo ilhali vielezi vya mahali hutokea mwishoni hasa vinapotumika na kitenzi elekezi. Uchanganuzi pia ulibainisha kuwa vielezi zaidi ya kimoja vinaweza kutokea pamoja katika kishazi. Vielezi vya aina mbalimbali vinapotokea pamoja, hupangika kimsonge. Kwa mfano kielezi cha namna hutangulia kikifuatwa na kielezi cha mahali kisha kielezi cha kiasi na mwisho kielezi cha wakati.

Uchanganuzi wa dhima za kisemantiki za vielezi katika kishazi cha Kiswahili unabainisha kuwa kielezi kinadhihirisha dhima anuwai za kisemantiki ambazo ni: dhima ya mahali ambayo inajumuisha chanzo, hatima, mwelekeo na umbali, dhima ya utaratibu ambayo inajumuisha njia, namna na ala, dhima ya wakati ambayo inajumuisha wakati dhahiri, wakati usiodhahiri, na kipindi cha kutendeka kwa kitendo, dhima ya kiasi ambayo inajumuisha vielezi vya kuzidisha na vielezi vya kupunguza. Ilibainika kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya umbo la kielezi na dhima za kielezi husika. Kwa mfano, vihusishi vinavyofanya kazi ya vielezi hasa huwa na dhima ya mahali na wakati. Vilevile nomino zinazofanya kazi ya vielezi huwa na dhima ya mahali na wakati na vielezi vinavyozalishwa kutoka kwa vivumishi huwa na dhima ya namna.

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Sintaksia Finyizi. Uchanganuzi wa muundo wa kishazi cha Kiswahili ulidhihirisha kuwa virai vinavyojumuika pamoja katika muundo wa kishazi huwa na uhusiano tegemezi kama inavyoelekeza kanuni ya tegemezi muundo. Kanuni husika imesaidia katika kuidadisha maneno katika kategoria mbalimbali ambayo ndio hatua ya kwanza ya uundaji wa kishazi. Hatua ya

muungano imehusika katika kuunda virai na vipashio vikubwa zaidi. Hatua ya tatu ambayo ni uhamisho, imedhihirisha kuwa kielezi kinaweza kuhama kutoka upande wa kulia wa kishazi hadi mzingo wa kushoto wa kishazi. Mchakato huu wa uhamisho unahusisha kanuni ya ulafi ambayo hueleza kuwa kijenzi husonga tu ili kutosheleza mahitaji ya kisarufi. Hili linabainishwa kielezi kinaposonga ili kitimize uamilifu wa kuwa fokasi au mada katika kishazi. Uhamisho huhusisha pia kanuni ya masafa mafupi ambayo hueleza kuwa kijenzi kinapaswa kusonga hatua chache tu. Hili linabainika kielezi kinaposonga kutoka mwisho wa kishazi kisha kinatua ndani na hatimaye kusonga tena hadi mwanzoni mwa kishazi. Ilibainishwa pia kuwa uhusiano baina ya kielezi na maneno mengine katika kishazi unaweza kuelezwa kwa mujibu wa kanuni ya uhusika. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa dhana ya dhima maana ni muhimu katika ufafanuzi wa dhima za kisemantiki za kielezi cha Kiswahili.

Sehemu hii imewasilisha matokeo ya uchanganuzi wa muundo na uamilifu wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili. Imeelezwa kuwa kielezi kina uhusiano wa karibu na kategoria zingine za maneno. Aidha kielezi kinaweza kujumuishwa katika kirai kitenzi, kirai kivumishi na kirai kihusishi. Ilibainishwa pia kuwa kielezi kinaweza kuwa msingi au kinaweza kuzalishwa kutoka kategoria zingine za maneno. Matokeo ya utafiti pia yalibainisha kuwa kielezi kinadhihirisha dhima anuwai za kisemantiki ambazo ni dhima ya mahali, dhima ya wakati, dhima ya utaratibu, na dhima ya kiasi. Matokeo ya utafiti ambayo yamewasilishwa yamemwelekeza mtafiti kutoa mahitimisho kadhaa kuhusu muundo na uamilifu wa kielezi katika kishazi cha Kiswahili.

5.2 Mahitimisho

Kutokana na matokeo yaliyotambuliwa na utafiti huu, inaweza kuhitimishwa kuwa malengo ya utafiti yalitimizwa. Uchanganuzi wa muundo wa kishazi cha Kiswahili unadhihirisha kuwa kategoria ya kielezi kina uhusiano na kategoria zingine za maneno kupitia kwa uundaji na vilevile kupitia kwa uamilifu. Vielezi vinaundwa kutoka kategoria zingine za maneno kwa njia ya uambishaji. Aidha, maneno mengine yanaweza kufanya kazi ya vielezi katika kishazi.

Matokeo ya uchanganuzi wa maumbo ya kielezi yanabainisha kuwa vielezi vinagawika katika vikundi viwili vikuu: vielezi msingi na vielezi zalika. Vielezi msingi vinajumuisha hasa vielezi sahili ambavyo vimeundwa kwa mofimu huru ilhali vielezi zalika vinajumuisha vielezi vyenye muundo changamani ambavyo vimezalishwa kutoka kategoria zingine na kwa hivyo vina viambishi awali au tamati vinavyovigeuza kuwa vielezi. Vielezi changamano vilevile, vinaweza kuwa kategoria zingine zinazofanya kazi ya vielezi. Kijumla, inabainika kuwa ingawa vielezi huzalishwa, vielezi vyenyewe haviwezi kunyambuliwa na havina uwezo wa kubadilisha kategoria ya maneno mengine.

Aidha, uchanganuzi muktadha wa kielezi cha Kiswahili umebainisha kuwa kielezi kinaweza kuhamishwa mbele kama mada au kama fokasi. Kutokana na uhamisho huo tunafikia hitimisho kuwa kuna uhusiano kati ya sintaksia na semantiki ya kielezi kwa kuwa mazingira ambamo kielezi kinapatikana hutegemea maana ya kielezi husika. Kwa mfano, vielezi vinavyotumiwa kuisisitiza ujumbe huweza kutokea mwanzoni mwa kishazi ilhali vielezi vyenye dhima ya namna hutokea hasa baada ya kitenzi.

Hata hivyo maana mbalimbali yanayotokana na sehemu ambayo kielezi kinapatikana hazikuweza kushughulikiwa kwa kina kwa kutumia nadharia ya Sintaksia Finyizi.

Matokeo ya utafiti yanabainisha pia kuwa kuna uhusiano wa umbo na uamilifu wa kielezi. Kwa mfano virai vihusishi vinavyofanya kazi ya vielezi huwa na dhima ya mahali na wakati. Vilevile nomino zinazofanya kazi ya vielezi huwa na dhima ya wakati na mahali. Aidha, vielezi vinavyoundwa kwa kuongeza kiambishi awali /vi/ huwa na dhima ya namna na vielezi vinavyoundwa kwa kuongeza kiambishi tamati /ni/ huwa na dhima ya mahali.

Kutokana na matokeo ya utafiti, inabainika kuwa vielezi vinaweza kuainishwa kisemantiki, kisintaksia na kimofolojia. Uainishaji wa kisemantiki unadhihirisha aina nne za vielezi: vielezi vya wakati, vielezi vya mahali, vielezi vya kiasi na vielezi vya namna. Aina hizi zimetokana na dhima za kisemantiki za vielezi. Ingawa uainishaji wa kisemantiki unakubaliana na uainishaji wa watafiti wa awali, uainishaji wenyewe unaonekana kuwa na upungufu kwa kuwa kunavyo vielezi kama vile: *kimsingi, kwa hakika, kawaida, huenda, na kuliko* ambavyo vinaonekana kuwa na uamilifu wa vielezi katika kishazi lakini haviwezi kuingizwa katika vikundi vya kisemantiki ambavyo vimebainishwa. Kisintaksia, matokeo yamebainisha kuwa vielezi vinaweza kuainishwa kulingana na mazingira ambamo vinapatikana katika kishazi na hivyo kuweza kugawika katika vikundi vitatu: vielezi vya mwanzo, ndani na mwisho wa kishazi. Hata hivyo, uainishaji huu pia una upungufu kwa kuwa kielezi kimoja kinaweza kutokea katika sehemu hizo zote. Kutokana na uainishaji wa kielezi kwa kuzingatia maumbo yanayotokana na uundaji, vielezi vinagawika katika vikundi

viwili: vielezi msingi na vielezi zalishwa. Uainishaji wa kimofolojia unadhihirisha wazi vielezi ambavyo ni msingi kwa kuwa vina umbo sahili na vielezi zalishwa pia vinadhihirika wazi kwa kuwa vinatokana na kategoria zingine za maneno kupitia uambishaji. Ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha ambishi-bainishi, utafiti huu unahitimisha kuwa uainishaji wa kielezi kwa kutumia maumbo yanayotokana na uundaji una uzito zaidi.

Utafiti huu unafikia hoja ya kijumla kuwa nadharia ya Sintaksia Finyizi ina utoshelevu katika kuchanganua muundo na uamilifu wa kielezi ingawa haingeweza kushughulikia maana mbalimbali za kishazi zinazotokana na uhamishaji wa kielezi. Hata hivyo, mahitimisho yaliyoelezwa yametuchoea kutoa mapendekezo ya utafiti.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Mapendekezo ya utafiti zaidi yametolewa kutokana na matokeo ya utafiti na mahitimisho ya utafiti huu. Utafiti huu ulichanganua mofolojia, sintaksia na semantiki ya kielezi cha Kiswahili. Umbo la kifonolojia la kielezi halikushughulikiwa, hivyo basi umbo la kifonolojia la kielezi cha Kiswahili linaweza kufanyiwa utafiti zaidi.

Utafiti huu uliangazia dhima za kisemantiki za kielezi. Hata hivyo, haukuangazia maana ya vielezi mbalimbali katika miktadha tofauti ya usemi. Hivyo basi, kuna umuhimu wa kufanya utafiti zaidi kuhusu pragmatiki ya kielezi ili kubainisha iwapo kielezi kinaweza kutumiwa kama kiashiria matini na kama fani ya kimtindo katika fasihi.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Sintaksia Finyizi. Hata hivyo, nadharia hii haingetumiwa kufafanua maana ya vielezi kulingana na muktadha hivyo basi nadharia nyingine kama vile Sarufi Amilifu na Sarufi Amilishi Mfumo zinaweza kutumiwa kuchanganua muundo na uamilifu wa kielezi. Tafiti zaidi katika nadharia tofauti zitachangia kurutubisha taaluma ya isimu nadharia mbali na kuongeza maarifa kuhusu vipengele vya kisarufi vya kielezi cha Kiswahili.

MAREJELEO

- Alexiadou, A. (1997). *Adverb Placement*. Amsterdam: John Benjamins.
- Anderson, S.R. (1992). *A-Morphous Morphology*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Bassong, P. R. (2010). *The Structure of The Left Periphery in Basaa*. Unpublished M.A. Thesis, University of Yaounde I: Cameroon.
- Buell, C.L. (2005). *Issues in Zulu Verbal Morphosyntax*. Ph.D Thesis, University of California, Los Angeles (Unpublished).
- Carter, R., McCarthy, M., Geraldine, M. & Anne, O. (2011). *English Grammar Today. An A-Z of Spoken & Written Grammar*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Chomsky, N. & Halle, M. (1968). *The Sound Pattern of English*. New York: Harper Publishers.
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge: Mass MIT Press.
- Cinque, G. (1999). *Adverbs & Functional Heads: A Cross Linguistics Perspective*. Oxford: Oxford University Press.
- Cook, V.J. & Newson, M. (1996): *Chomsky's Universal Grammar*. 2nd edition. Oxford: Basil Blackwell.
- Crystal, D. (1980). *A First Dictionary of Linguistics & Phonetics*. London: Deustch.
- Ernst, T. (2004). *The Syntax of Adjuncts*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Fasano, T. (2014). *English Grammar in Review*. California: Coyote Canyon Press.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Haegeman, L. (1994). *Introduction to Government & Binding Theory*. Oxford: Blackwell.
- Hatch, E. (1995). *Vocabulary, Semantics & Language Education*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Haumann, D. (2007). *Adverb Licensing & Clause Structure in English*. Amsterdam: John Benjamins.

- Hladky, J. (2003). *A Guide to Pre-Modern English*, Masarykova University: V. Brane, Brno.
- Huddleston, R. (1984). *Introduction to the Grammar of English*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Jackendoff, R. (1972). *Semantic Interpretation on Generative Grammar*. 6th edition. Cambridge: Mass MIT Press.
- Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi na Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salam: TUKI.
- Kayne, R.S. (1994). *The Antisymmetry of Syntax*. Cambridge, MA: MIT Press.
- Kennedy, A.G. (1920). "The Modern English Verb-Adverb combination." *Stanford University Series in Language & Literature*. Stanford: Stanford University Press.
- Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B & Msanjila, Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- King'ori, A. (2005). *Movement in The Kiswahili Sentence: A Minimalist Approach*. Unpublished M.A. Thesis: Kenyatta University.
- Kombo, D.K. & Tromp, D. (2006). *Proposal & Thesis writing: An Introduction*. Nairobi, Paulines Publications Africa.
- Leech, G. & Svartvik, J. (2002). *A Communicative Grammar of English*. England: Longman Group Limited.
- Longobardi, G. (1994). "Reference and Proper Names", *Linguistics Inquiry*.
- Loogman, A. (1965). *Swahili Grammar & Syntax*. Pittsburgh Pa: Dugesne University Press.
- Massamba, D. P. B, Kihore, Y.M & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbaabu, I. (1992). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Longman.
- Mdee, J.S. (1986). *Kiswahili Muundo na Matumizi Yake*. Nairobi: Intercontinental Publishers Ltd.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.

- Michael, I. (1970). *English Grammatical Categories & Tradition to 1800*. Cambridge: Cambridge University Press
- Milroy, J.S. (1967). *Observing & Analysing Natural Language*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.
- Mohammed, H. (2013). *Syntactic Analysis of Arabic Adverbs between Arabic & English*. Unpublished PhD Thesis, University of Malaya, Kuala Lumpur Malaysia.
- Mohammed, S. A. (2013). *Mkamandume*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.
- Mohammed, M.A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mugenda, O. M. & Mugenda, A.G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: African Centre for Technology Press.
- Mwihaki, A. (2007). "Minimalist Approach to Kiswahili Syntax." *Journal of The Institute of Kiswahili Research*. TUKI.
 Mtandao: <http://www.ajol.info/index.php/ksh/article/64852>
- Njogu, N., Mwihaki A. & Buliba, A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Payne, E. (1997). *Describing Morphosyntax: A Guide for Field Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Pinkster, H. (1972). *On Latin Adverbs*. Amsterdam: Amsterdam University Press.
- Poletto, C. & Pollock, J.Y. (2004). "On The Left Periphery of some Romance Wh-Questions." In Rizzi ed., *The Structure of CP & IP – The cartography of Syntactic Structures*. Vol. 2. New York: Oxford University Press.
- Poole, G. (2002). *Syntactic Theory*. Hampshire: Palgrave.
- Potsdam, E. (1998). *Syntactic issues in the English Imperative*. New York: Garland Publishing Company.
- Pratiwi, D. R. (2014). *Identification of Adjectives & Adverbs among students*. Unpublished PhD Thesis: Pendindikan.
- Quirk, R. & Greenbaum, S. (1973). *A Universal Grammar of English*. London: Longman.

- Radford, A. (1997). *Syntax a Minimalist Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Radford, A. (2004). *Minimalist Syntax: Exploring the Structure of English*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Roux, J. C. L. (2007). A Grammatical Analysis of The Tswana Adverbial. Dhitt et Phil Thesis. Pretoria: University of South Africa (Unpublished).
- Vitale, A.J. (1982). *Swahili Syntax*. Dordrecht: Foris Publications.
- Waihiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Yin, W. L. (2002). *The Morphology, Syntax & Semantics of Adverbs in Cantonese*. Unpublished PhD Theses, University of Hongkong.

KIAMBATISHO A: DATA YA UTAFITI

Data hii inajumuisha vishazi vilivyokusanywa kutoka mazungumzo ya kawaida katika lugha ya Kiswahili na kutoka riwaya ya Mkamandume. Vishazi vimepangwa kwa kuzingatia muundo wa kielezi kimofolojia, muundo wa kisintaksia na muundo wa kisemantiki.

Maumbo ya vielezi

Katika sehemu hii, vishazi vimeainishwa katika vikundi viwili; vishazi ambavyo vina vielezi sahili na vishazi ambavyo vina vielezi changamano.

Vishazi vyenye Vielezi vyenye Umbo Sahili

Kielezi	Matumizi katika Kishazi
ajabu	Liyongo alikuwa mtu mnene <i>ajabu</i> .
kabisa	Uchumi wa nchi yetu umeimarika <i>kabisa</i> . Mkulima alinunua gari jeupe jipya <i>kabisa</i> . Ufisadi umekita mizizi nchini kabisa.
kupindukia	Karamu ya kwanza ilifana <i>kupindukia</i>
mbali	Watoto wameenda <i>mbali</i> .
mno	Gharama ya maisha mjini Mombasa ni ghali <i>mno</i> . Kusoma kwake kulimnufaisha <i>mno</i> . <i>Mno</i> ni matawi makavu shambani mwa mkamandume
ovyo	Juma amezoea kutumia gari <i>ovyo</i> .
sana	Mwizi ameumia <i>sana</i> . Ugonjwa huo ulienea <i>sana</i> . Hawa wote walionyesha juhudi kubwa <i>sana</i> katika huo mkutano.
tu	Wanatumia <i>tu</i> zile pesa. Wewe unapendeza <i>tu</i> .
zaidi	Huyu ni mkulima shupavu <i>zaidi</i> . Chakula changu ni kitamu <i>zaidi</i>
chini	Wanafunzi wameketi <i>chini</i> .
mbali	Wavuvi wamesafiri <i>mbali</i>
juu	Ndege ameruka <i>juu</i> .

Vishazi vyenye umbo Changamano

Vishazi vyenye Vielezi Vinavyoundwa kwa Kuongeza –ki, ni -na -u kwa Nomino

Kielezi	Matumizi katika kishazi
<i>kifisi</i>	Waniasia wanapora mali <i>kifisi</i> .
<i>kikondoo</i>	Alikufa <i>kikondoo</i> .
<i>korokoroni</i>	Mfungwa alitoroka <i>korokoroni</i> .
<i>kinyama</i>	Askari walimchapa mfungwa <i>kinyama</i> .
<i>kijeshi</i>	Wanafunzi hawa wanatembea <i>kijeshi</i> .
<i>kiume</i>	Maimuna anafanya kazi <i>kiume</i> .
<i>upande</i>	Mstari ule umekwenda <i>upande</i> .
<i>uokoni</i>	Wanabiashara wameondoka <i>sokoni</i> .
<i>shimoni</i>	Kijana shujaa alimtoa mtoto <i>shimoni</i> .
<i>uwanjani</i>	Asha na Juma wanacheza <i>uwanjani</i> .
<i>pembeni</i>	Samaki wa zile nchi za <i>pembeni</i> mwa duniani tamu.

Vishazi vyenye Vielezi Vinavyoundwa kutoka kwa Vivumishi

Kivumishi	Kielezi	Matumizi katika Kishazi
-baya	vibaya	Mtoto ameumia <i>vibaya</i> .
-ngine	vingine	Tulijaribu <i>vingine</i> .
-zuri	vizuri	Shamba limelimwa <i>vizuri</i> . Nguo imeshonwa <i>vizuri</i> . Nguo zote zilisafishwa na kuanikwa <i>vizuri</i> . Waashi wawili walijenga <i>vizuri</i> nyumba yetu. Ukuta umepakwa rangi <i>vizuri</i> .

Vishazi vyenye Vielezi vya Uradidi

Kielezi	Matumizi katika Kishazi
Harakaharaka	<i>Harakaharaka</i> vipanga vilitumbukia shimoni.
Hivihivi	Wanafunzi wengi hufanya kazi <i>hivihivi</i> .
Hobelahobela	Oliech alibebwa <i>hobelahobela</i> .
Hisirisiri	<i>Kisirisiri</i> babu akauza shamba.
Kwelikweli	Mahali humu mnapendeza <i>kwelikweli</i>
Nyumanyuma	Mkamandume alirudi <i>nyumanyuma</i> kwa uoga.
Polepole	Miti <i>polepole</i> yaliyumbayumba. Mwalimu anazungumza <i>polepole</i>
Vipandevipande	Kiti hiki kimevunjika <i>vipandevipande</i> .

Vishazi vyenye Vielezi vya Kionomatopea

Kielezi	Matumizi katika kishazi
bwe!	Mbwa alibweka <i>bwe!</i>
chakari!	Alikuwa amelewa <i>chakari</i> .
chumbwi!	Jambazi huyo alijitumbukiza majini <i>chumbwi!</i>
Kwe! Kwe! Kwe!	Watoto walicheka <i>kwe kwe kwe!</i>
ndi!	Mlango ulifungwa <i>ndi!</i>
tuli!	Wachezaji walitulia <i>tuli!</i>
zu	Moshi ulizuka <i>zu!</i>

Muundo wa Kisintaksia wa Kielezi

Vishazi vyenye Vielezi ambavyo vina Uwezo wa Kutokea Mwanzoni mwa Kishazi

Kielezi	Mfano katika Kishazi
juzi	<i>Juzi</i> wanafunzi walichelewa.
kimsingi	<i>Kimsingi</i> , shule zote zitafungwa.
leo	<i>Leo</i> , rais aliwasili mjini mapema sana.

Vishazi vyenye Vielezi ambavyo Vinaweza Kutokea Ndani ya Kishazi

Kielezi	Mfano katika Kishazi
sana	Wanafunzi werevu <i>sana</i> wametuzwa.
zaidi	Mti mrefu <i>zaidi</i> umekatwa.
juzi	Wanafunzi <i>juzi</i> walichelewa.

Vishazi vyenye Vielezi ambavyo Hutokea Mwishoni mwa Kishazi

Kielezi	Mfano katika Kishazi
haraka	Kwetu kumejengwa <i>haraka</i> .
jana	Askari yule shujaa alikamata wezi <i>jana</i> .
jikoni	Leta sahani yoyote hapa <i>jikoni</i> .
jioni	Wanafunzi wanatoka <i>shuleni</i> . Pahali hapa patasafishwa <i>jioni</i> .
kabisa	Chakula kimeiva <i>kabisa</i> .
kabisa	Wewe mwimbaji unapendeza <i>kabisa</i> .
kesho	Nyumba itabomoka <i>kesho</i> .
mbali	Watoto wameenda <i>mbali</i> .
mno	Kusoma kuananufaisha <i>mno</i> .
msituni	Kwanza ni kuondoka hapa <i>msituni</i> .
nje	Mnazi umepandwa <i>nje</i> .
polepole	Askari walinyatia <i>polepole</i> .
sana	Hao walionyesha juhudi kubwa <i>sana</i> .
sasa	Tutaondoka <i>sasa</i> .
vizuri	Shamba limelimwa <i>vizuri</i> . Chai imepikwa <i>vizuri</i> .
vizuri	Vitabu vile vimehifadhiwa <i>vizuri</i> .
zaidi	Huyu ni mkulima shupavu <i>zaidi</i> .
zamani	Nilikisoma kitabu hicho <i>zamani</i> .
juzi	wanafunzi walichelewa <i>juzi</i> .

Vishazi Vilivyo na Virai Elezi

juzi asubuhi	Mvua nyingi ilinyesha juzi asubuhi
mara kadhaa	Mwanafunzi yupi ameumia mara kadhaa?
mara tatu	Nimetembea Mombasa <i>mara tatu</i> .
mji wa Mombasa nchini Kenya	Watalii watazuru <i>mji wa Mombasa nchini Kenya</i> .
mjini mapema sana leo	Rais aliwasili <i>mjini mapema sana leo</i> .
saa moja asubuhi	Tutafanya mtihani <i>saa moja asubuhi</i> .
vizuri sana	Vibarua walifanya kazi <i>vizuri sana</i> .
haraka zaidi	Askari wanatembea <i>haraka zaidi</i> .
mara kadhaa	Mwalimu ametusaidia <i>mara kadhaa</i> .
hobela hobela marambili jana jioni ukumbini	Msanii alibebwa <i>hobelehobela mararambili jana jioni ukumbini</i> .
shambani mapema sana	Wakulima wameenda <i>shambani mapema sana</i> .
jana jioni	Walisoma gazeti <i>jana jioni</i> .
juzi asubuhi	Mvua nyingi ilinyesha <i>juzi asubuhi</i>
mara tatu jana	Wale wote walipokea tuzo <i>mara tatu jana</i> .
mwaka ujao	Vikombe vingi vitanunuliwa <i>mwaka ujao</i> .
sasa hivi	Jino lake litangolewa <i>sasa hivi</i> .
kwa ndege	Tulisafiri <i>kwa ndege</i> .

Vishazi vyenye dhima mbalimbali za kisemantiki

Dhima ya Kisemantiki	Matumizi katika Kishazi
mahali dhahiri	Babake anaishi <i>kampala</i> .
mahali pasipodhahiri	Juma ameketi <i>nyuma</i> .
Mwelekeo	Mbuzi wamepanda <i>mlima</i> . Magaidi wameelekea <i>mashariki</i> . Wanariadha wameteremka <i>chini</i> .
Chanzo	Wanafunzi wanatoka <i>shuleni</i> .
Hatima	Wanabiashara wameenda <i>sokoni</i> .
Umbali	Wanafunzi wamesafiri <i>mbali</i> .
Namna	Mwajuma huzungumza <i>vizuri</i> .
Ala	Mgonjwa amedungwa <i>sindano</i> .
wakati dhahiri	Mkutano utanza <i>asubuhi</i> . Barabara itakarabatiwa <i>kesho</i> . Mahafala walifuzu <i>jana</i> Muuguzi anamhudumia mgojwa <i>sasa</i>
wakati usiodhahiri	Zahanati ilijengwa <i>zamani</i> .
Muda	Mtihani utafanywa <i>kwa miezi miwili</i> .
Kiasi	Mtoto ameumia <i>kidogo</i> .

KIAMBATISHO B: KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI KUTOKA NACOSTI

THIS IS TO CERTIFY THAT:
MISS. WINNY CHELANGAT CHERUIYOT
of KENYATTA UNIVERSITY, 433-232
RUIRU, has been permitted to conduct
research in Mombasa County

on the topic: MUUNDO NA UAMILIFU
WA KIELEZI KATIKA KISHAZI CHA
KISWAHILI

for the period ending:
11th February, 2018

.....
Applicant's
Signature


Permit No : NACOSTI/P/17/39573/15626
Date Of Issue : 13th February, 2017
Fee Received :Ksh 1000




.....
Director General
National Commission for Science,
Technology & Innovation

CONDITIONS

1. You must report to the County Commissioner and the County Education Officer of the area before embarking on your research. Failure to do that may lead to the cancellation of your permit.
2. Government Officer will not be interviewed without prior appointment.
3. No questionnaire will be used unless it has been approved.
4. Excavation, filming and collection of biological specimens are subject to further permission from the relevant Government Ministries.
5. You are required to submit at least two(2) hard copies and one (1) soft copy of your final report.
6. The Government of Kenya reserves the right to modify the conditions of this permit including its cancellation without notice



REPUBLIC OF KENYA



National Commission for Science,
Technology and Innovation
RESEACH CLEARANCE
PERMIT

Serial No.A **12787**
CONDITIONS: see back page